# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 14 Agosti, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULLO):** Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Maoni ya Kamati ya Fedha Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti, kwa taarifa ya wageni wetu huyo ni Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Oh leo naona mambo ni mazito kidogo wanakuja wazito watupu.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI –WIZARA YA FEDHA, MIPANGO NA UWEZESHAJI:** Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**SPIKA:** Kwa taarifa ya wageni pia aliyewasilisha taarifa sasa hivi ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ndani ya Bunge. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 395

**Uharibifu wa Mazingira na Kampuni ya Placer Dome**

**MHE ALI KHAMIS SEIF (K.n.y. MHE. CHACHA Z. WANGWE)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kampuni ya *Placer Dome* ina mwaga maji na takataka zenye sumu aina ya *cynide* na *mercury* kwenye mto Tigithe, ambapo wananchi wa maeneo hayo wanayatumia maji ya Mto huu kwa shughuli mbalimbali na tayari watu kadhaa na mifugo imeathirika na kemikali hizo:-

(a) Je, Serikali inaweza kufanya *Environmental Impact Assessment* ya mgodi huo ili kuwanusuru watumiaji wa maji ya Mto huo kutokana na kemikali hizo?

(b) Kwa kuwa, Mto Tigithe humwaga maji yake kwenye Mto Mara na Mto Mara humwaga maji yake Ziwa Victoria. Je, Serikali haioni kwamba, samaki wanaovuliwa ziwani hawafai kwa matumizi ya binadamu kutokana na kemikali hizo na itafanyaje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Wangwe, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Dhahabu wa *Placer Dome* huko katika eneo la Gokoni Nyabigena karibu na Mto Tigithe, Wilaya ya Tarime. Shughuli inayofanyika katika eneo la Gokona ni uchimbaji udongo (Malighafi) ambao husafirishwa Nyabirama umbali wa kilomita saba. Eneo hili ni kilomita 100 Mashariki ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, *cyanide* kemikali ambayo kiasi chake kikiwa kikubwa katika mchanganyiko wa vimilika huwa ni sumu kali hutumia viwandani katika kutengeneza dawa za kuulia wadudu, plastiki, rangi, nailoni na katika uchimbaji wa madini. Kiasi kidogo cha *cyanide* upatikana kiasilia katika vyakula kama vile mihogo, ulezi, kabeji na mchicha. Hata hivyo hakuna matatizo ya muda mrefu ya kiafya kuwepo na kiasi hiki kidogo cha *cyanide.*

Mheshimiwa Spika, *Placer Dome* hutumika sana katika uchenguaji wa dhahabu *(Gold Processing)* uchenguaji hufanyika Nyabirama na mabaki ya uchafu wa uchenguaji yenye *cyanide* huwekwa kwenye kwenye bwawa maalum (*tailing storage facility*) ili kudhibiti uvujaji unaoweza kuathiri mazingira, maji yenye kiasi kidogo ya *cyanide* yanayotokana na uchafu huo nayo huhifadhiwa katika bwawa maalum kabla ya kurejeleshwa kiwandani. Bwawa limewekewa kinga madhubuti. Uangalizi wa kila mara (*Environmental Monitoring*) hufanywa ili kudhitibi uvujaji wa aina yoyote ile unaoweza kupenya chini kwa chini hadi Mto Tigithe au Mto Mara.

Kampuni ina maabara ambayo inafanya uchunguzi wa sampuli mbalimbali ili hatua za haraka zichukuliwe endapo panatokea matatizo. Uchunguzi wa muda mrefu wa

sampuli kutoka Mto Mara na Mto Tigithe umeonyesha hakuna dalili za kuwepo kwa chembe chembe (*traces)* za '*cyanide'*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Wangwe, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tathmini ya Athari kwa Mazingira (*Environmental Impact Assessment)* ya mgogi wa *Placer Dome* ilifanyika mwaka 2000 kabla ya kuanza rasmi shughuli za uzalishaji na iliwasilishwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC*) na Wizara ya Nishati na Madini. Ripoti na Mpango wa Usimamizi wa Mazingira (*Environmental Management Plan)* ilijadiliwa na kukubaliwa na wadau wote toka sekta husika.

Mwaka 2002 *NEMC* ilishauri Kampuni ya *Placer Dome* kufanya uchunguzi wa kina ili kubainisha athari kwa mazingira, wafanyakazi, na jamii inayozunguka mgodi, zinazoweza kutokea kutokana na shughuli za uchimbaji.

Matokeo ya uchunguzi huo yaliiwezesha Kampuni hiyo kuboresha Mpango wa Usimamizi wa Mazingira *(EMP)* ya kutengeneza Mpango wa Nyongeza uliozingatia ushauri huo. Mwaka huo huo ulifanyika utafiti ili kujua hali ya viumbe hai katika Mto Mara na Mto Tigithe. Matokeo ya utafiti huo hayakubainisha madhara yanayotokana na shughuli za uchimbaji yanayohatarisha maisha ya viumbe hai katika mito hiyo.

Hata hivyo Serikali inawataka wenye migodi kwa kushirikiana na wataalamu toka *NEMC* na Wizara ya Nishati na Madini, kuendelea kufanya Ukaguzi wa Mazingira *environment audit* na kubaini kama kuna athari zote, ili hatua za haraka zichukuliwe inapobidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mgodi wa *Placer Dome* hautumii zebaki *(mercury)* katika uchenguaji wa dhahabu hakuna uwezekano wa kuwepo kemikali hiyo katika maji taka yanayotokana na shughuli za mgodi huo.

(b) Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 kupitia Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria kwa kushirikiana na Shirika Lisilo la Kiserikali la Kimataifa la Hifadhi ya Mazingira na Wanyamapori na Kampuni ya *Placer Dome* ilifanya utafiti wa hali ya samaki katika Ziwa Victoria na Mto Mara. Matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa vipimo vya ubora wa samaki wa Ziwa Victoria kwa matumizi ya binadamu vipo juu ya viwango vya Kimataifa.

Aidha, maabara za kisasa zilizo kwenye viwanda vya minofu na Taasisi za Kiserikali zinatumika kupima ubora wa minofu ya samaki. Kwa kuzingatia hayo samaki wanaovuliwa toka Ziwa Victoria huuzwa kwenye masoko ya Ulaya ambako viwango vya ubora vinapewa kipaumbele. Hakuna malalamiko toka kwenye masoko ya ndani na nje ya Tanzania ndiyo maana uuzaji wa minofu ya samaki nje ya nchi bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo haya, napenda kuwahakikishia wananchi wanunuzi wa samaki kutoka nje ya Tanzania vile vile napenda kumhakikishia huyo Bwana Hubert Sauper kwamba samaki wanaovuliwa toka Ziwa Victoria ni salama kabisa hawana chembechembe cha aina yoyote zenye kuhatarisha afya ya binadamu.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa sababu Mheshimiwa waziri amekiri kuwa *cyanide* kwa kiwango kikubwa inaweza ikaleta athari. Na amekiri kuwa huko kunakochimbwa madini ni kuwa kuna hifadhi ya *cyanide* katika mabwawa. Je, Mheshimiwa Waziri hakuna njia nyingine ya kuhifadhi *cyanide* isipokuwa kuwekwa katika bwawa?

**SPIKA:** Halikusikika Mheshimiwa Mbunge. Ebu tafadhali rudia swali.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa sababu Mheshimiwa Waziri amekiri kuwa iko *cyanide* ambayo inatumiwa kwa kuhifadhia dhahabu. Na amekiri kuwa *cyanide* inahifadhiwa katika mabwawa na *cyanide* ikiwa nyingi inakuwa ni sumu, je, hakuna njia nyingine ya kuhifadhi *cyanide* isipokuwa katika mabwawa?

**SPIKA:** Yaani Waziri *cyanide* lazima itupwe kwenye mabwawa tu hakuna njia nyingine ya kuweza kuyatokomeza?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, *cyanide* ni kemikali ambayo kiasilia inakuwa na *carbon na nitrate*. Kuweza kuharibika haraka yaani ikapoteza nguvu yake ya kemikali kwa kukutana na mionzi ya jua ndiyo maana huwekwa kwenye mabwawa ambayo moja kwa moja inakutana na mionzi ya jua na kuharibika.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kuweka *cyanide* kwenye mabwawa ni katika hatua muhimu ya *detoxification* yaani kuifanya *cyanide* isiwe nafuu.

Mheshimiwa Spika, *cyanide* ni madini ambayo ni sumu sana na yakiwepo katika kiwango kidogo sana yanaweza kuleta maafa. Kwa hivi kiasi ambacho kinakuwa pale kikiingia kwenye ziwa na kuwa *detoxified* hakina madhara yoyote. (*Makofi)*

Na. 396

**Uchafuzi wa Mazingira**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA (K.n.y.MHE. SUSAN A. J. LYIMO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, mazingira ni suala mtambuka na kwamba, Serikali imejitahidi sana kudhibiti hali ya uchafu wa mazingira ikiwa ni pamoja na kuongeza ushuru kwenye mifuko ya plastiki lakini pamoja na juhudi hizo bado mifuko ya plastiki maarufu kama

Rambo inaendelea kuzagaa kwenye sehemu nyingi hasa za mijini na kuhatarisha afya za watu na wanyama wachungwao:-

(a) Kwa kuwa, historia inaonyesha kuwa, mifuko hiyo haikuwepo katika miaka ya nyuma na badala yake ilitumika mifuko ya karatasi za khaki na magazeti. Je, Serikali haioni hoja ya kuzuia kabisa mifuko ya Rambo isitumike tena hapa nchini na kurudia utaratibu wa nyuma?

(b) Kama Serikali haiwezi kuzuia bidhaa hizo za plastiki, kwa nini isinunue kinu ili mifuko hiyo pamoja na bidhaa za aina hiyo zifanyiwe *recycling*?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mwezi April 2006 Serikali ilitoa tamko la kupiga marufuku utengenezaji, uagizaji, ununuzi na matumizi ya mifuko ya plastiki laini na ile ya kufungia maji na maji ya matunda. Serikali imeongeza kodi kwenye mifuko mingine ya plastiki kwa asilimia 120.

Aidha, Shirika la Viwango liko katika hatua za mwisho katika kuweka viwango vya plastiki vinavyokubalika nchini. Serikali inahimiza utengenezaji wa mifuko mbadala kama vile mifuko ya nguo, vikapu, mifuko ya karatasi na mengineyo.

(b) Mheshimiwa Spika, aina nyingine za plastiki ngumu kama vile mifuko minene, maturubai, ndoo, mipira, zitaendelea kutumika. Tayari viwanda vingi vya plastiki vina sehemu ya kurejeleza plastiki (*recycling). (Makofi)*

Na. 397

**Mpango wa Kukuza na Kuimarisha Michezo Nchini**

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI (K.n.y. MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Rais wa Awamu ya Nne ameonyesha nia ya kukuza na kuimarisha michezo:-

(a) Je, Selikali haioni kuwa, sasa ni wakati muafaka wa kujenga kituo cha michezo nchini ili kukuza vipaji vya vijana wetu kama ilivyo nchini Senegal, Ivory Coast na kwingine?

(b) Je, ni lini Serikali itaanzisha timu ndogo ya Taifa ya mpira wa miguu ya kudumu ili iwe chemchem ya kupata timu bora ya soka nchini?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DR. EMANNUEL NCHIMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba, kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa ni wakati muafaka kujenga kituo au vituo vya michezo nchini ili kukuza vipaji vya vijana wetu kama ilivyo katika nchi nyingine mbalimbali.

Aidha, Serikali ina mpango wa kutenga shule maalum kwa kanda, zitakazomesha watoto wenye vipaji maalum vya michezo nchini. Pamoja na masomo mengine, michezo ndiyo utakuwa mchepuo maalum.

Hivi sasa tayari zipo *Sports Academies,* yaani vituo vya michezo ambako vijana wenye vipaji vya michezo, sio mpira wa miguu tu bali hata riadha, wanafanya mafunzo ya michezo katika maeneo hayo.

Mifano ya vituo hivyo ni:-

1. *Makongo Secondary School;*
2. *Rollingstone Arusha;*
3. *Tanzania Sports Academy – Arusha;*
4. Timad ya Chuo Kikuu;
5. Panguline – Charles Boniface;
6. Wakati Ujao;
7. *Morogoro Kids;*
8. *Majeshi Kids;*
9. *Don Bosco;*
10. Nguva – Tanga;
11. Tesa;
12. *New Heroes;*
13. *New Heroes;* na
14. Dayoso.

Vituo hivi vimeamua kufanya mashindano kila mwaka kwa njia ya kujitolea na kwa huba na mapenzi yao ya kupenda maendeleo ya michezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inavyo vituo viwili vya Kanda, Arusha na Songea vyenye lengo la kuendeleza wanamichezo mbalimbali.

Kuhusu kuendeleza vipaji vya watoto, Serikali tayari imeliagiza Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kuhakikisha kwamba kuanzia mwaka 2006 vyama vyote vya michezo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Mpira wa miguu viwe vinahimiza vilabu

vya michezo nchini kuwa na timu za watoto wadogo kuanzia umri wa miaka chini 6,8,10,12,14, na 18. *(Makofi)*

Mashindano kati ya timu hizo za watoto ndiyo yatakayowezesha kupata timu imara za Taifa kwa ajili ya michezo mbalimbali. Serikali pia imeagiza kila mchezo uwe na timu za Taifa tatu, chini ya miaka 14, 17 na 20. *(Makofi)*

Jukumu la kuanzisha timu ndogo ya Taifa ya Mpira wa Miguu siyo la Serikali bali ni la Shirikisho la Mpira wa Miguu *(TFF).* Kwa hivi sasa *TFF* inazo timu za Taifa kwa vijana wa chini ya miaka 17 na chini ya miaka 20. Ili kuunga mkono jitihada ya kukuza vipaji vya watoto na vijana, Serikali tayari imegharamia ujio wa kocha wa kigeni kwa ajili ya kukuza vipaji kwa vijana.

Hata hivyo Serikali inatoa wito kwa watu binafsi kujitokeza na kuanzisha *Sports ac Ademies* za kisasa nchini. Hii itasaidia sana kupata wachezaji bora. Waswahili wanao usemi usemao: "Samaki mkunje angali mbichi".

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, vituo hivyo alivyovitaja vina vifaa vya kutosha kwa ajili ya kuwawezesha vijana hao kuweza kufanya kazi zao vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI**): Mheshimiwa Spika, kwamba vituo tulivyovitaja vimekuwa vikifanya jitihada kubwa ya kuwa na vifaa mbalimbali. Jitihada za Serikali ni kuhakikisha vituo hivyo vinakuwa na vifaa vya kisasa zaidi kwa kufuatilia kwa karibu na kushirikiana nao.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutoa jawabu fasaha katika swali mama. Lakini nina swali moja la nyongeza.

Kwa sababu Serikali imetakiwa zianzishe timu za Taifa za Vijana kwa ajili ya kuendeleza mpira. Lakini Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba katika uteuzi wa Timu ya Taifa ya Tanzania kuna ukiritimba wa kutochagua baadhi ya wachezaji wa upande wa pili wa Jamhuri. Timu ya Taifa ya Serengeti iliyokuwapo hivi sasa ina wachezaji wangapi kutoka Zanzibar?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:**Mheshimiwa Spika, jukumu la kuchagua wachezaji wa Kimataifa ni la Makocha wenyewe na sio la Serikali.

Lakini ningependa kutoa wito kwa Makocha wa Taifa wanapochagua timu zao basi waangalie uwezekano wa wachezaji wazuri watoke pande zote mbili za Muungano.

Na. 398

**Maandalizi ya Fainali za Mataifa ya Afrika – 2008**

**MHE. IDDI M. AZZAN** aliuliza:_

Kwa kuwa, nchi yetu haifanyi vizuri katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa katika mpira wa miguu; na kwa kuwa, Ratiba ya Mashindano ya *Africa Cup of Nations* – 2008 imeshatolewa ambapo timu yetu ya Taifa imepangwa kundi moja na timu ngumu kama Senegal na Burkinafaso:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuiwezesha timu yetu kucheza fainali hizo Mwaka 2008?

(b) Kwa kuwa, Tanzania ina marafiki ambao nchi zao zimepiga hatua kubwa katika michezo hususan mpira wa miguu: Je, Serikali ipo tayari kuziomba nchi hizo kuipa timu yetu ya Taifa mafunzo na kucheza mechi nyingi za majaribio kwenye nchi hizo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Iddi M. Azzan, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imeweka mikakati ifuatavyo:-

1. Kupata Kocha mwenye ujuzi, sifa na uwezo wa kuimudu kazi hiyo;

2. Wachezaji wenye viwango vinavyokidhi kupatikana;

3. Kuwepo vifaa vya mafunzo na vya wakati wa mashinda;

4. Kuwepo kwa kambi ya mafunzo inayozingatia viwanja vizuri, malazi safi, na chakula kizuri (*balanced diet)*.

5. Kuwepo kwa vifaa mbalimbali vya mafunzo kama vile mipira, viatu vya mpira, raba za mazoezi, jezi na kadhalika.

6. Kupatikana kwa posho za wachezaji na masilahi mengine.

7. Kuandaliwa mashindano ya majaribio.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia wananchi kwamba masuala yote hayo yamekamilika.

(b) Serikali ipo tayari kushirikiana na nchi rafiki kuipa timu yetu mashindano ya majaribio. Hata hivyo programu ya mafunzo lazima izingatie mfumo ufuataao:-

1. Kipindi cha maandalizi (*preparation perio*d).
2. Kipindi cha mashindano (*competition period).*
3. Kipindi cha mapumziko (*resting period*).

Kwa bahati mbaya timu yetu ilianza mafunzo katika kipindi cha maandalizi chini ya makocha wetu wazalendo – Dr. Mshindo Msolla na Ali Bushir – kabla ya kukabidhiwa rasmi kwa kocha mpya wa Brazil, Bwana Maximo.

Mheshimiwa Spika, kati ya tarehe 27 Machi na 4 Aprili, 2006, timu za *Kilimanjaro Stars* (Bara) na *Mapinduzi Stars* (Zanzibar) zilicheza michezo miwili ya kirafiki. Katika mchezo wa kwanza timu hizo zilitoka sare bao moja kwa moja, na zikatoka tena sare kwa bao mbili kwa mbili katika mchezo wa pili. Baada ya michezo hiyo miwili ndipo ilipoundwa Timu ya Taifa, *(Taifa Stars)* ikijumuisha wachezaji wa pande zote mbili (za Muungano). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 1 – 7 Mei, 2006 timu ya Taifa iliingia kambini kuendelea na mafunzo na kupangiwa mechi moja ya kirafiki na *Harambee Stars* ya Kenya, lakini kwa bahati mbaya mchezo uliahirishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 19 Juni mpaka 15 Julai, 2006, *Taifa Stars* iliendelea kuingia kambini na baadaye kwenda Mauritius ambako ilicheza na Timu ya Taifa ya huko na kuifunga magoli 2 kwa moja.

Halafu *Taifa Stars* walisafiri kwenda *Seychelles* walikocheza na Timu ya huko na kufungwa mabao mawili kwa moja. Baadaye *Taifa Stars* waliendelea na mafunzo kuanzia tarehe 26 Julai hadi 1 Agosti 2006, na kupangiwa kucheza na timu ya Taifa ya Rwanda ambayo waliifunga bao moja kwa sifuri.

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 7 Agosti hadi tarehe 8 Septemba, 2006, *Taifa Stars* ilipangiwa kuendelea na Kambi yake ya mafunzo tayari kwa mechi yao ya kwanza ya *Africa Cup of Nations* na timu ya Burkinafaso chini ya kocha Marcio Maximo.

**MHE. MOHAMMED R. SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa mchezo wa mpira wa miguu kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri unatakiwa kutunzwa kwa vifaa pamoja na vitu vingine. Lakini juzi tu Uwanja wa Jamhuri Wizara ya Afya walifanya maonyesho yao matokeo yake una *pin*, kuna Bodi *Pin*, kuna misumari, *pin* nyingine.

Je, Wizara inasemaje kuhusu hilo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DR. EMMANEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya msingi kabisa ya Serikali ni kupokea taarifa na kuzifanyia kazi kwa haraka.

Taarifa hii tumeipokea tutalisimamia kuona kama kuna matatizo haya tuyashughulikie mara moja.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, swali moja dogo la nyongeza. kwa kuwa mara nyingi safari za Timu yetu ya Taifa zimekuwa ziki-*fail* kwa sababu viongozi wanaokwenda katika safari hizo ni wengi kuliko wanamichezo wahusika. Je, Serikali inalisimamiaje hili?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi tunavyoendelea msimamo wa Waziri wangu ni kuhakikisha kwamba wanaokwenda katika shughuli za michezo ya Kimataifa hasa wengi wao wawe wale wanaohusika kushiriki katika michezo hiyo kama wachezaji.

Kwa msimamo wa Waziri unazingatiwa na unaheshimiwa na Waziri wangu ataendelea kuusimamia.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO**: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono majibu ya Mheshimiwa Waziri. Lakini lazima tuone kwamba hawawezi kwenda wachezaji bila ya kuwa na viongozi na Makocha. Kwa hiyo, muhimu kuwe na wachezaji kuwe na viongozi ili kuweka nidhamu na kuongoza watu hao. Lakini ni vyema pia kwamba wachezaji wawe wengi zaidi kuliko viongozi wa michezo.

Na. 399

**Huduma ya Nishati ya Umeme.**

**MHE. LEKULE M. LAIZER (K.n.y. MHE. OMAR S. KWAANGW')**aliuliza:-

Kwa kuwa huduma za nishati ni kichocheo kikubwa katika shughuli za uchumi na maendeleo na kwa kuwa kuna kituo kikubwa cha umeme wa gridi ya Taifa (*Substation)* Babati: na kwa kuwa eneo la Halmashauri mpya ya Mji wa Babati linahitaji sana kusambaziwa umeme.

(a) Je, Kituo cha umeme wa gridi (*substation)* kilichopo Babati kina uwezo gani na kiasi gani cha uwezo unaotumika maeneo yote yanayotumia kituo hicho?

(b) Je, Serikali kupitia Shirika la *TANESCO* ina mpango gani wa kusambaza umeme kwenye vijiji vya karibu na vyenye shughuli za kiuchumi vya Managha, Himiti, Haraa na Bonga ambavyo vyote vipo katika barabara kuu ya kaskazini (*The Great North Road*)?

(c) Je, Serikali kupitia mpango wa MKURABITA inaweza kuwawezesha wananchi kwa kuwakopesha wale wote watakaojiunga pamoja na kutaka kuunganishwa umeme ili walipe kwa awamu mara baada ya kupata umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Shaaban Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kituo cha umeme cha gridi cha Babati kilijengwa kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na kukamilika mwaka 1999. Kituo hicho hugawa umeme kwa vituo vidogo vya Kondoa, Mbulu na Karatu ambapo njia za umeme za kilovoti 66 zimejengwa kati ya Babati na Kondoa na pia kati ya Babati, Mbulu na Karatu.

Kituo cha Babati kina uwezo wa kutoa *MW 343.4* na kinasambaza umeme katika vituo vya Babati, Karatu, Kondoa na Mbulu. Vituo hivyo ni pamoja vina matumizi ya juu ya umeme wa *MW 4.95.*

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kusambaza umeme katika Vijiji vya Managha, Himiti, Haraa na Bonga chini ya mradi wa *Energizing Rural Transformation (ERT)* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

(c) Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wananchi kulipia huduma hii ya umeme, litakuwa jambo la busara baada ya MKURABITA kukamilisha shughuli zake, wananchi watumie hati watakazopewa katika kupata mikopo au dhamana kutoka Taasisi za Fedha kama vile Benki na Vyama vya Kuweka na Kukopa.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ningependa kuuliza maswali mawili yafuatayo:-

Kwa kuwa mji wa Babati ni Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara na kwa kuwa mji wa Babati unakua kwa kasi sana. Je, Serikali iko tayari kuendana na kasi hiyo ya Babati kusambaza umeme katika mitaa yote pamoja na majengo yanayojengwa Babati?

Swali la pili, kwa kuwa kuna miji ya Makao Makuu ya Wilaya zilizoko nchini hasa zilizoko mpakani je, Serikali iko tayari sasa kuipatia miji hiyo umeme kama Namanga, upande wa Namanga Kenya wana umeme lakini Tanzania hatuna umeme. Wako tayari sasa kusambaza kutafuta kila njia ili miji iliyoko mpakani wapate umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kuna Mpango kabambe wa *ERT* ambao lengo lake kuu ni kuhakikisha kwamba maeneo mengi ya vijiji vya Tanzania vikiwemo vile

alivyovitaja na maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Laizer kupata umeme katika kipindi cha mwaka 2005 – 2010.

Ningependa kumhakikishia kwamba kasi ya ukuaji wa eneo la Babati Serikali imezingatia na tutahakikisha kwamba kadri ya uwezo wetu tutafikisha umeme katika maeneo yote ambayo yanaweza yakapata umeme.

Ningependa pia kumhakikishia Mheshimiwa Laizer kwamba uko mpango wa kuhakikisha kwamba eneo la Mpakani hasa lile la Namanga litapata umeme katika kipindi cha 2005 – 2010.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini ningependa kuuliza kwamba kwa kuwa *TANESCO* Songea kwa muda wa miaka mitatu mfululizo imeweka katika bajeti yake mpango wa kupeleka umeme kijiji cha Peramiho na kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri ametueleza kwamba mpango huo sasa utakuwa unatekeleza.

Je, katika kijiji cha Peramiho mpango huo utakuwa katika awamu za kwanza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama vile ambavyo nimeshawahi kulieleza Bunge lako Tukufu, eneo la Peramiho linategemea kupata kipindi cha mwaka huu.

Na. 400

**Utekelezaji wa Sera ya Nishati**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa umeme utokanao na nguvu za maji umeonyesha kutokuwa endelevu katika nchi yetu; na kwa kuwa ilani ya uchaguzi ya CCM imependekeza kuanza kuendeleza vyanzo vya *Gas* na makaa ya mawe:-

(a) Je, vyanzo hivyo viwili vitaainishwa vipi katika sera nzima ya nishati katika muda mfupi na mrefu?

(b) Je, mradi wa Mchuchuma utaanza kutekelezwa lini na kwa utaratibu gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Benedict Mwalyosi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ludewa ina madini mengi yakiwemo makaa ya mawe ya Mchuchuma, madini ya chuma yaliyoko Liganga na kadhalika, Kama

ilivyoelezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Serikali itaelekeza nguvu zake katika kuendeleza gesi ya asili na makaa ya mawe katika uzalishaji wa umeme.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali iliunda timu ya wataalamu chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko yakuangalia namna ya kutekeleza mradi huo kwa ufanisi, haraka na kama bei nafuu. Timu hiyo imeshamaliza kazi yake na Serikali sasa inatafakari namna ya kushughulikia mradi huu katika kipindi cha 2005-2010 kama ilivyo ainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005.

**MHE. PROF RAPHAEL R. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu hayo ya Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. La kwanza kwa vile Wizara zinazohusika na miradi hiyo mikubwa ya Liganga na Mchuchuma inajitahidi sana kutekeleza Ilani ya CCM ya kuhakikisha kwamba miradi hii inaanza kutekeleza katika kipindi hiki; na kwa vile katika hotuba mbalimbali za Wizara husika wametueleza kwamba juhudi zinafanywa ili kubaini makampuni yatakayoshughulikia utekelezaji wa miradi hii miwili, na vile vile wamesema juhudi zinafanywa kutafuta wabia wa kuanza kutekeleza miradi mama itakayohusisha chuma na makaa ya mawe ya Mchuchuma.

Je, tunaweza tukapewa *milestones* kwamba katika miaka minne na nusu iliyobaki katika mwaka wa kwanza, wa pili na watatu ni shughuli zipi zitakuwa zinafanyika ili tuwe na uhakika kwamba kweli ifikapo 2010 kutakuwa na kazi zitakuwa zimetelezwa kuhusiana na miradi hii miwili.

Swali la pili, kwa kuwa sasa inaelekea Serikali inataka kweli kutekeleza miradi hii katika miaka hii minne na nusu; na vijiji vinavyozunguka makaa ya Mchuchuma na migodi ya Liganga wameishi miaka mingi sana wakiambiwa ardhi ile wasiitumie kwa sababu watahamishwa bila fidia. Je, kwa vile sasa juhudi zinaelekea kwamba wataanza kutekeleza miradi nikawaambie nini wananchi wa Ludewa kuhusu fidia za wananchi hawa kwa sababu miradi hii inaanza kutekelezwa?

**SPIKA:** Kuhusu la kwanza nadhani kulingana na jibu sidhani kama Serikali inaweza kuwa na *milestones* wakati imeteua timu ya wataalam ndiyo iwape taarifa Serikali. Kwa hiyo, mimi naliona liko nje kabisa la swali msingi, labda kama Waziri ana ufafanuzi ila la pili la fidia ni sahihi.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri sana ni kwamba ni kweli kwamba Serikali inaangalia utaratibu wa namna ya kutekeleza mradi huu na Wizara zinazohusika ikiwemo ya Fedha, Nishati na Madini, Miundombinu, Viwanda na Biashara na Mipango Uchumi na Uwezeshaji tumekutana tunatazama namna bora zaidi ya kushughulikia mradi huu na wakati ukifika Serikali itatoa taarifa.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge asubiri kwamba Serikali itatoa taarifa juu ya namna bora ya kuuendeleza mradi huu na hizi ndizo ambazo sehemu ya salamu ambazo

anaweza kuzichukua akawapelekea wananchi wa Ludewa katika kipindi hiki cha 2005-2010 kama ambavyo Ilani ya Uchaguzi ya CCM imeainisha.

La pili kama ilivyokawaida katika miradi yote ambayo Serikali inatekeleza au au inasimamia pale ambapo wananchi na mali zao wanaathirika kutokana na ujenzi wa mradi wowote taratibu za kawaida na za kisheria zinafuatwa katika kuhakikisha kwamba wananchi hao wanalipwa fidia zao na katika mradi huu haitakuwa tofauti. Wakati utakapofika wananchi wataarifiwa na taratibu husika zitafuatwa kuhakikisha kwamba mali halali za wananchi hazidhulumiwi katika utekelezaji wa mradi huu.

Na. 401

**Kampuni Binafsi Kununua Pamba**

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1995 Serikali ilizidhamini Kampuni binafsi kununua pamba kutoka kwa wakulima Tarafa za Songwe na Kwimba Wilayani Chunya; na kwa kuwa wamiliki wa kampuni hizo waliacha ghafla kutoendea na kununua pamba na wakati huo huo wakahama nchini na kwenda nje kabla ya kuwalipa wakulima fedha zao zilizotokana na mauzo ya pamba:-

(a) Je, Serikali haioni ni vyema kuwalipa wakulima hao fedha zao ili waondokane na usumbufu wa kufuatilia malipo hayo Mkoani Mbeya bila mafanikio?

(b) Kwa kuwa kumbukumbu zote kuhusu hali hiyo ziko Mkoani Mbeya. Je, Serikali itachukua hatua gani za kuhakikisha kuwa wamiliki wa kampuni husika wanatafutwa na kuchukuliwa hatua za kisheria?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a), (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kati ya miaka ya 1994/1995 na 1998/1999 wakati pamba ilipokuwa inalimwa katika Tarafa za Songwe na Kwimba Wilayani Chunya makampuni binafsi yalikuwa yakinunua pamba ya wakulima kupitia Vyama vyao vya Ushirika wa *MBECU* na *CHUDICU*. Makampuni hayo ni *Ralli Brothers*, *SM Holdings*, *Mbeya Textile*, *Intake Corporation* na *Golden Impex.* Wanunuzi hao waliacha kununua pamba baada ya kilimo cha zao hilo kusitishwa mnamo mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kuwa Vyama vya Ushirika vya *MBECU* na *CHUDICU*, ambavyo vilikusanya pamba kwa wakulima

vilikabiliwa na madeni makubwa na ya muda mrefu na hivyo kushindwa kuwalipa wakulima wa pamba wa Tarafa za Songwe na Kwimba fedha zao za mauzo ya pamba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tangu wakati huo vyama vingi vya Ushirika vimekumbwa na hali ya kuwa na madeni sugu, mwaka 2005 Serikali iliamua kuyachukua kwa nia ya kuyalipa au kuyafuta madeni sugu ambayo yalikuwa yanadaiwa na vyombo vya fedha pamoja na wakulima.

Wakulima wanaodai fedha zao kutoka Chama Kikuu cha *MBECU* ambacho sasa kinajulikana kama *Mbeya Ileje Cooperative Union (MICU)* ya kiasi cha shilingi milioni 291/- na wale wanaodai kutoka *CHUDICU* kiasi cha shilingi milioni 602 wataweza kulipwa madeni yao pindi taratibu za Serikali za kuhakiki zitakapokamilika. Malipo hayo yatawahusu pia wakulima kutoka Tarafa za Songwe na Kwimba Wilayani Chunya.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekiri yenyewe kwamba ni kweli kwamba hawa wakulima wamekuwa wakifuatatilia haya malipo yao tangu mwaka 1995 na kwa kuwa sasa hizi Serikali imeamua kuwalipa kwa kuanza na uhakiki nakumbuka kabisa kwamba uhakiki huo ulianza mwaka jana mwishoni mwa mwezi wa kumi na mbili na sasa hivi ni miezi minane uhakiki haujamalizika. Je Serikali haiwezi ikatamka ni lini uhakiki huo utakamilika ili wakulima hawa wapate malipo yao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kazi hii ya uhakiki imeanza kipindi hicho alichokisema Mheshimiwa Mbunge na kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba uhakiki wa madeni haya unatakiwa ufanyike kwa makini, kwa sababu madeni yenyewe yanahusu vipengele vingi, kuna madeni yanatakiwa yapambanuliwe ambayo yalitokana na uzembe au ubadhirifu. Hayo yanaweza yasiingizwe katika utaratibu wa malipo. Lakini hata yale yatakayobainika kwamba yanastahili kulipwa yanatakiwa vile vile yathibitiwe na hatimaye yapate uhakiki kikamilifu. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi ninavyozungumza suala la uhakiki limeshakamilika kutoka kule Mkoani isipokuwa kazi ya uhakiki katika ngazi ya Mkuruguzi Mkuu muda si mrefu itakamilika na suala hilo litafikia tamati.

Na. 402

**Tatizo la Maji – Mlowo na Tunduma.**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alipokuwa kwenye kampeni za kugombea nafasi ya Urais Wilayani Mbozi hapo tarehe 31/8/2005 aliahidi kutatua tatizo sugu la maji katika Miji ya Mlowo na Tunduma; na kwa kuwa suala la kuwapatia

wananchi maji ni agenda kubwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2005 - 2010.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais inatekelezwa mara moja na kuwapatia wananchi wa maeneo hayo maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Wizara yangu kwa kushirikiana na Wilaya ya Mbozi imeweka mkakati wa kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais. Programu ya Kitaifa ya usambazaji wa maji vijijini ni mkakati ambao Serikali imeunda na utekelezaji wake unaanza mwaka huu wa fedha 2006/2007 kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mlivyoelezwa wakati Mheshimiwa Waziri wa Maji alipokuwa akiwasilisha Bajeti ya mwaka 2006/2007. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri husika tutaziingiza ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais ikiwemo hii Tunduma na Mlowo katika progamu niliyotaja hapo awali pamoja na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika katika mwaka huu wa fedha 2006/2007, Wizara yangu imetenga kiasi cha shilingi milioni 20 kwa ajili ya kufanya utafiti wa vyanzo vya maji katika mji wa Tunduma. Pia juhudi za kupata vyanzo vya maji ya kutosheleza mji wa Tunduma zimeanza kufanyika ambapo uchunguzi na upimaji wa bwawa la Mto Lukumba umefanywa na Wilaya ya Mbozi. Aidha uchunguzi na usanifu wa mradi wa maji kwa mji mdogo wa Mlowo nao wamepangwa kufanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007, kupitia mpango wa kitaifa wa maji safi wa mazingira vijijini.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali na Wizara kwa majibu mazuri, lakini nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya maji katika Miji wa Tunduma na Mlowo na kwa kweli kwa Wilaya nzima ni ya muda mrefu sana; na kwa kuwa Serikali imekuwa inaahidi mara kwa mara kutatua matatizo katika miji hiyo bila mafanikio na kwa kuwa sasa mwaka huu Serikali imeonyesha kuwa na mipango mizuri. Je, Waziri atakuwa tayari kuja yeye mwenyewe Mbozi kuzungumza na wananchi hawa akiwahakikishia ahadi hizi za Serikali kwamba sasa zitatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, tumepokea huo mwaliko na tuko tayari aidha mimi au Waziri wangu mmoja wetu atakwenda huko kuongea na wananchi, ahsante sana.

Na. 403

**Tatizo la Maji Manispaa ya Kigoma**

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Manispaa ya Kigoma – Ujiji inapata maji kutoka Ziwa Tanganyika na kwa kuwa kumekuwa na tatizo la upatikanaji wa maji kwenye mabomba yaliyopo katika Manispaa hiyo hali inayosababisha akinamama na wanafunzi wanaoishi *hostel* kuamka alfajiri kwa lengo la kutafuta maji mitaani au Ziwa Tanganyika na hivyo kuchelewa shuleni na kwenye sehemu zao za kazi: -

(a) Je, Serikali ya Awamu ya Nne itawasaidiaje akinamama na wanafunzi hao?

(b) Je, ni lini akinamama na wanafunzi hao watapata usingizi mnono wa asubuhi na kuepukana na adha hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** atajibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo: -

Manispaa ya Kigoma – Ujiji ina wakazi wapatao 175,000 na wanaongezeka kwa wastani wa asilimia 7.5. Chanzo kikuu cha maji ni Ziwa Tanganyika. Mahitaji ya maji ni mita za ujazo 16,600 kwa siku ikilinganishwa na mita za ujazo 10,000 zinazozalishwa kwa siku kwa hivi sasa. Aidha, mfumo wa majisafi uliopo ni wa siku nyingi na umechakaa, hivyo hautoi huduma ya kuaminika wakato wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi za *Nordic* - *Nordic Development Fund* (*NDF*) na Jumuiya ya Nchi za Ulaya (*EU*) pamoja na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (*KfW*) chini ya mfuko wa *ACP-EU Water Facility* watagharamia miradi ya uboreshaji wa huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka na usafi wa mazingira katika miji 7 ukiwemo mji wa Kigoma Ujiji, kwa gharama ya takribani Shilingi bilioni 8.7. Kati ya fedha hizo Shilingi bilini 4.0 zitatumika kugharimia maandalizi ya mradi wa Kigoma *Urban Water Supply and Sanitation Development* sambamba na miradi ya kuzuia uchafuzi wa Ziwa Tanganyika *(pollution Control*), uondoaji maji ya mvua (*Storm Water Drainage*) na ukusanyaji taka ngumu (*Solid Waste Management*).

Mradi huu utatekelezwa kama sehemu ya mpango mkubwa unaojulikana kama *Lake Tanganyika Integrated Regional Development Programme* unaoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Maandalizi ya mradi huu yatahusu kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa majisafi na majitaka na kuitisha zabuni ya kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya uchunguzi huo. Ripoti ya uchunguzi huo itaainisha gharama na hatua zitakazotakiwa kuchukuliwa ili kukidhi mahitaji ya majisafi na usafi wa mazingira katika

Mji wa Kigoma hadi mwaka 2025. Mkataba wa ufadhili tayari ulikwisha kusainiwa na mradi utatekelezwa katika mwaka 2006/2007.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza hapo mwanzo kuhusu mfuko wa *ACP-EU*, fedha za *ACP-EU Water Facility* kiasi cha Shilingi bilioni 3.8 zitagharamia utekelezaji wa miradi wa muda mrefu wa uboreshaji wa miundombinu ya majisafi na majitaka katika miji saba ikiwemo Kigoma – Ujiji. Shughuli zitakazofanyika ni pamoja na ukarabati wa chanzo cha maji, kufunga dira za maji, ukarabati na upanuzi wa matandao wa mabomba ya majisafi na kuanza ujenzi wa majitaka. Taratibu za maandalizi ya kusaini makubaliano ya ufadhili *Financing Agreement* zinaendelea na utekelezaji utaanza mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Serikali kwamba miradi hii itakapokamilika, tatizo la ukosefu wa maji katika Manispaa ya Kigoma – Ujiji litatoweka na wakazi wa Manispaa hiyo wakiwemo wanafunzi, akinamama na wasichana watapata majisafi na salama na ya kuaminika kwenye makazi yao.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona naomba niongeze dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa kuamka alfajiri kutafuta maji si salama kwa wanafunzi hao pamoja na akinamama. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuhusu usalama huo kwa kuweza kuwasaidia hao wanawake na wanafunzi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kutafuta maji na zaidi wakati wa jioni au asubuhi sana ni hatari na si salama kwa wanawake au kwa wasichana ambao wanaweza wakaenda sehemu kama hizo. Lakini kama nilivyoeleza katika jibu langu la awali kwamba taratibu zinafanyika katika kuhakikisha kwamba maji yanapatikana. Hata hivyo sehemu ambazo zilizoathirika zaidi katika mji wa Kigoma ni sehemu ya *Block Q*, Masanga, Businda na sehemu ya Kagera ambayo haipati maji kwa sababu ya mabomba ya *PVC* yaliyoibiwa na watu ambao si waaminifu. Napenda kutoa wito kwamba tunaomba wakazi wa Kigoma Mjini na Ujiji yale maji madogo ambayo yanagawiwa kwa kaya yaweze kutumiwa vizuri ndiyo njia pekee ya kuweza kuhakikisha kwamba hata zile sehemu walizo na shida ya maji wanaweza wakapata maji.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma unavyo vyanzo vya maji tofauti na Ziwa kama vile mito. Je, Serikali itakubaliana nami kutumia njia mbadala vya mito iliyoko Mkoani Kigoma.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Kigoma kwa hivi sasa kuna miradi ya chemchem ambayo tayari inatumikika. Miradi hii iko minne ikiwemo chemchem ya Kibirizi, Rutare, Bushabani na chemchem ya Nyakageni. Hizi ni baadhi ya chemchem zinazotumika Mkoa wa Kigoma. Hali kadhalika kuna visima vifupi vitano ambavyo sasa hivi viko katika majaribio ambavyo vitasaidia kuongeza maji katika Mkoa wa Kigoma ambavyo vinafadhiliwa na Shirika la kuhudumia Wakimbizi Duniani.

Na. 404

**Utengenezaji wa Barabara ya Masumbwe – Bukoli**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Masumbwe – Mbogwe – Bukoli inayounganisha Bukombe na Geita kwenye eneo la Bukoli ni ndefu na ni mbaya mno kiasi ambacho Halmashauri ya Wilaya haiwezi utengenezaji wake: -

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuitengeneza barabara hiyo ili iweze kutumika ipasavyo na wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mbunge wa Bukombe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Luhahula alivyoeleza kwenye swali lake, barabara hiyo ipo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Bukombe. Ninamshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri husika ili waiweke barabara hiyo kwenye mipango yao ili iweze kutengenezwa kwa kutumia vyanzo vyake vingine vya fedha ikiwa ni pamoja na fedha za Mfuko wa Barabara *(Road Fund Board)* na hivyo kupunguza kero ya usafiri kwa wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Shinyanga ipo tayari kutoa ushauri wa kitaalam kama utahitajika.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu lakini nina swali moja ya nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa barabara hii ilikuwa inaunganisha Wilaya ya Geita- Mbogwe – Bukombe Kahama na Nzega na haijatengenezwa tangu wakoloni waondoke na kwa kuwa barabara hii pamekuwa pakitolewa ahadi na wagombea nafasi ya Ubunge katika Bunge hilo kwa miaka 20 iliyopita na sasa nilipokuwa napita kwenye kampeni waliniambia kwamba kama sitatengeneza barabara hii usije kugombea tena mwaka 2010.(*Kicheko*)

Je, Serikali iko tayari kuna mimi sigombei tena mwaka 2010; na kama haiko tayari kuona mimi sigombei mwaka 2010 Serikali iko tayari kushirikiana na Wilaya ya Bukombe kuitengeneza barabara hii kwa sababu ina urefu wa Km 50? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MHANGA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda sana Mheshimiwa Mbunge agombee tena kwa mara ya pili na ndiyo maana nilisema awasiliane na Wilaya na sisi tuko tayari kutoa ushauri wowote wa kitaalam. Lakini kama ambavyo wamekuwa wakifanya kwenye Mikoa na Wilaya nyingine Sina hakika kama barabara hii Wilaya ya Bukombe imeomba ipandishwe daraja kama ambavyo imefanyika kwenye maeneo mengine.

Kama tulivyoeleza hapa Bungeni baadaye mwaka huu tutaangalia ni barabara zipi za Wilaya zinafaa kupandishwa daraja kufikia za Mkoa. Kama barabara hiyo ipo basi tutaiangalia, lakini kwa sasa ukitaka kutoka Bukombe kwa maana ya kupita kwenye barabara za Mkoa zinazosimamiwa na (*TANROADS)* tunahudumia barabara inayotoka Kahama –Busoka kwenda mpaka Masabi mpaka Buyange ambako huko huko Bukoli.

Lakini Halmashauri ya Wilaya Bukombe ndiyo hiyo inatokea Bukombe kwenda mpaka Buyange na Bukoli. Kwa hiyo, kama nilivyosema mimi nadhani Serikali ni hiyo, Wilaya pamoja na Wizara zote ni Serikali na tunajitaji mgombee ili tutekeleze Ilani ya uchaguzi.

Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa tuendelee kuwasiliana pamoja na Wilaya yake ili barabara hiyo iwe katika hali nzuri. *(Makofi)*

Na. 405

**Uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Mji wa Musoma**

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI (K.n.y. MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Musoma umepewa hadi ya kuwa Manispaa na kwa kuwa ni kawaida kwa Serikali kuboresha kwanza miji yenye hadhi hiyo ya Manispaa:-

Je, Serikali ina mpango wowote wa kuboresha kiwanja cha ndege cha Mji wa Musoma?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwa kutambua umuhimu na mchango wa viwanja vya ndege katika kuboresha na kuinua Sekta ya Utalii, Madini na Uvuvi kwa maendeleo ya wananchi kwa ujumla Wizara ya Miundombinu inafanya yafuatayo ili kuboresha kiwanja cha ndege cha Musoma.

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini (*TAA*) hutumia wastani wa Shilingi milioni 90.0 kwa mwaka kwa ajili ya gharama za kutunza na kuendesha kiwanja cha Musoma. Gharama hizo ni kwa ajili ya:-

(i) Kukata nyasi, kuzibua mitaro ya maji ya mvua na kuziba mashimo kwenye njia ya kurukia na kuegeshea ndege na kufanya matengenezo madogo madogo ya majengo;

(ii) Kulipa mishahara ya wafanyakazi gharama za utawala na kuendesha ofisi; na

(iii) Matengenezo ya magari pamoja na vifaa vya zimamoto.

Katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA*) imetenga shilingi milioni 130 kwa ajili ya upanuzi wa jengo la abiria na hasa ukumbi wa watu mashuhuri *(VIP Lounge)* na pia ujenzi wa uzio ili kuimarisha usalama kiwanjani.

Gharama ya ukarabati miundombinu kwa kiwango cha lami na kuboresha majengo ya kiwanja hicho inakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 5.2. kutokana na ufinyu wa Bajeti, Wizara ya Miundombinu inaendelea kutafuta fedha ili kukamilisha mradi huu kwa viwango vinavyotakiwa.

Kwa sababu hiyo Wizara imekiweka kiwanja cha Musoma katika orodha ya viwanja vinavyotafutiwa wafadhili nchini chini ya mpango wa miaka kumi wa uendelezaji miundombinu nchini.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo: -

Ule uwanja wa ndege wa Mji wa Musoma, kwanza uko katikati ya Mji na kutokana na hali hiyo, si rahisi sana kupanuliwa licha ya mahitaji makubwa yaliyopo ya ndege kubwa za mizigo kama minofu ya samaki pamoja na mizigo mingine.

Lakini vile vile, uwanja huu kwa kuwa upo katikati ya Mji unasababisha mahali ambapo watu wangeweza kupita katika muda wa dakika tano wanatumia hadi saa moja nzima kwa ajili ya kuzunguka. Ningependa kujua, je; ule mpango wa kuhamisha ule uwanja wa ndege umbali wa kilometa 15 kutoka pale ulipo bado upo? Kama upo, huo mpango unatarajia kuanza lini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Manyingi kwamba, uwanja ule hivi sasa uko katikati ya Mji, lakini ulipojengwa haukuwa katikati ya mzunguko wa Mji. Hii ni kama kawaida ya wananchi kujenga maeneo ambayo uwanja upo na mfano halisi ni Bukoba na Dodoma.

Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, mpango wa kuhamisha uwanja huu wa Musoma kwenda eneo lingine upo, lakini utatekelezwa pale fedha za kutosha zitakapopatikana kwa ajili ya kujenga.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na pia maswali yenyewe yamekwisha. Ninayo matangazo.

Kwanza, napenda niendelee kutambua uwepo wa Bibi Ngasongwa, mke wa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Karibu sana na tunashukuru unaendelea kuwepo hapa kumpa nguvu mzee. *(Makofi)*

Katika *Public Gallery* wapo wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari ya Nkuhungu ya Mjini Dodoma. Nadhani wapo mkono wa kushoto.

**MBUNGE FULANI:** Hawapo.

**SPIKA:** Hawapo eeh, mnatakiwa msimame. Ahsante sana, ahsante. Tunawashukuru sana, karibuni sana, sana. *(Makofi)*

Pia, kuna wageni wa Mheshimiwa Zabein Mhita na Mheshimiwa Paschal Degera, ambao ni Madiwani 50 kutoka Wilaya ya Kondoa.

Waheshimiwa Madiwani, karibuni sana tunafurahi sana. Miongoni mwao wapo Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kondoa, Bwana Filimini Hondo na Katibu wa CCM wa Wilaya hiyo Mheshimiwa Omari Mkiwa. Ahsante sana, karibuni sana Waheshimiwa madiwani. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Teddy Kassela-Bantu, ni Madiwani wawili, Ndugu Chuma na Ndugu Izengo na Katibu wake Ali Mwinyimvua (Katibu wa Mbunge).

Kutoka Igunga, Mheshimiwa Rostam Azizi, Mbunge wa Igunga anao wageni wake Madiwani 15 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Igunga na wataalam saba, wale pale wanatupungia mikono. Karibuni sana Waheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Diana Chilolo, anao wageni wake ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalum kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Singida Vijijini, wako 12 na viongozi wa UWT wawili, jumla 14, wale pale. Karibuni sana. *(Makofi*

Looh, hizi orodha jamani zinaanza kuwa ndefu!

Mheshimiwa Stanley Kevella ana wageni wake kutoka Njombe Magharibi, naomba wasimame. Baadhi ni viongozi na baadhi ni jamaa zake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwataarifu kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na mkutano wa Wabunge wote. Madhumuni ya mkutano huu ni kupeana taarifa mbalimbali na mkutano wenyewe utafanyika katika ukumbi wetu wa zamani. Kwa hiyo, wale Wenyeviti wote waliotoa taarifa za mikutano ya saa saba ningewaomba wapange upya kwa sababu haitapendeza wakati wa mkutano wetu sisi sote kwa mambo ambayo yanahusu Bunge zima wakati huo huo iendelee mikutano mingine ya Kamati.

Labda pekee nawaomba Wajumbe wa Kamati ya Uongozi *(Steering Committee)* ya Bunge na Tume ya Huduma tukutane kwa dakika chache kwenye *Speakers Lounge* ya zamani mkutano utakapokaribia tu kuanza. Ni jambo fupi sana, tuingie hapo kwanza halafu tujumuike na wenzetu. Ni kwa muda wa dakika chache sana.

Waheshimiwa Wabunge, niseme tu hapa sasa, matokeo ya Uchaguzi wa *Commonwealth Parliamentary Association* yatatangazwa huko tukiwa pamoja kule katika ukumbi wa zamani.

Mheshimiwa Gideon Cheyo Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi anaomba Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi wakutane saa tano asubuhi leo, chumba namba 428.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwafahamisha tu kwamba, Wabunge wenzetu walemavu wamesafiri kwenda New York kwenye mkutano. Ni Waheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mheshimiwa Riziki Said Lulida na Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji ambaye kwa mazingira yake amesindikizwa na msaidizi wake. Nadhani mnaelewa hali halisi ilivyo. *(Makofi)*

Nilikuwa natangaza hili tu kuonyesha kwamba wenzetu hao kwa sababu wana matatizo maalum mtambue tu wako safarini na tuzidi kuwaombea wakae huko salama. Ni siku 11, leo hadi tarehe 25 Agosti, 2006. Tunawaombea waweze kurudi salama.

Napenda pia nitangaze kwamba, kesho kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge, tutaweka oro ya majina ya Wabunge takriban 88 watakaosafiri nchi za nje kwa S*tudy Tours.* Tumeanzisha utaratibu huu ambao kwa Kiswahili cha sasa wanasema *kukosha macho.* Yaani kwenda sehemu mbalimbali kuona tu wenzetu wanafanyaje shughuli hizi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, orodha ni ndefu mno na niseme tu najua mnaweza kuwa mnapanga ziara za Majimbo ama shughuli nyingine. Sasa, bila kujua mambo haya mawili yanaweza yakagongana. Kwa hiyo, ndiyo maana natoa taarifa hiyo, kesho tutaiweka hiyo orodha kila Mheshimiwa Mbunge anayeondoka kwenda safari ajue ni lini. Lengo ni kwamba, kati ya kesho kutwa na Bunge litakaporejea tena labda mwisho wa mwezi wa kumi ziwe zimefanywa ziara 11 za Wabunge wanane wanane, ndiyo inakuja hiyo idadi ya 88.

Kwa hiyo, naomba mtazame kwa Katibu wa Bunge ili kila mbunge ajue. Wale watakaoona hawamo, utaratibu huu siyo wa kulipua, ni utaratibu endelevu na tutaendelea nao hadi 2010. Kwa hiyo, zamu zao zitakuja baadaye. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, juzi Jumamosi kulikuwa na mchezo wa mpira wa miguu na mchezo wa *netball* baina ya timu zetu na timu za Viongozi wa Dini hapa Dodoma. Matokeo ni kama ifuatavyo: Nikianza upande wa *netball*, timu machachari kabisa ya Wabunge Wanawake iliwafunga Viongozi wa Dini *point* 17 kwa 10. Kwa hiyo, naona wembe ule ule wa Kongwa unaendelea hadi huku. *(Makofi)*

Upande wa mpira wa miguu mambo nayo ni mazuri tu. Timu ya Waheshimiwa Wabunge iliwafunga timu ya Viongozi wa Dini magoli manne kwa bila. Kwa niaba yenu wote, napenda kuwapongeza sana, sana timu zetu hizi. Mheshimiwa Mohammed Rajab

Soud ambaye anashiriki sana katika kuzinoa, anaomba kwamba mazoezi yaendelee, tusibweteke na huu ushindi tulioupata. Ahsante sana Mheshimiwa Mohammed Rajab. *(Makofi)*

Leo jioni kuna hafla kabambe ambayo ni chakula cha jioni na burudani za aina mbalimbali katika ukumbi wetu hapa hapa. Kwa mara ya kwanza utatumika huu. Kamati ya Mheshimiwa Jenista Mhagama imefanya kazi nzuri sana. Hii ndiyo ratiba ambayo mtaipata wakati fulani na hii ndiyo *menu card* (hapa Spika aliionyesha *card* husika). Mambo yanakwenda kwa viwango, siyo ovyo ovyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mgeni rasmi atakuwa mpendwa wetu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngonyai Lowassa na tunachukua fursa hiyo hiyo ya hafla hii ya kuagana kwa kumaliza Mkutano wa Nne wa Bunge hili. Pia kumwaga rasmi Mheshimiwa Spika Mstaafu, Pius Msekwa. Kutakuwa na matukio mengi mazuri mazuri tu. Pengine saa saba pia nitatangaza ili tuone utaratibu kwa sababu kadi inasema tuanze saa 1.30. Sasa mnaelewa hapo kuna kikwazo fulani, lakini itabidi tuangalie tufanyeje ili hilo liwezekane. *(Makofi)*

Hapo ndiyo mwisho wa matangazo. Katibu shughuli zinazoendelea kwenye *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007
### Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea nilikuwa nimeshauriana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu jioni, sikuweza kutangaza chochote. Nitaomba saa saba tuamue ili Bunge liweze kurejea saa kumi na kumaliza shughuli zake saa moja kasorobo kwa sababu kwa kuanza saa moja unusu shughuli itaisha saa tano unusu. Sasa, tukianza saa mbili na dakika kadhaa, shughuli yenyewe ina mpangilio, ina hotuba na kadhalika tutafika zaidi ya saa sita, kitu ambacho si kizuri. Kwa wadogo zangu kama Mheshimiwa Khalifa, haina tabu, lakini kwa baadhi yetu itakuwa shida kidogo. Kwa hiyo, saa saba nitawahoji ili tuweze kuanza saa kumi na kumaliza saa moja kasorobo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu alikwishaita, sasa orodha yangu ya wachangiaji sijui tena nimeiweka wapi. Wahudumu wameondoa ile orodha ya wachangiaji, walikuwa wamebaki wawili. Sasa naomba tu wasimame.

Mheshimiwa Shah, utaanza wewe halafu Mheshimiwa Serukamba atamalizia.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia mawili/matatu katika kujenga, juu ya hoja ya Wizara ya

Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, ambayo ndiyo Wizara inayopanga mipango yote na kuratibu maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na wataalam wao wote wa Wizara hiyo kwa kuandaa hotuba nzuri iliyoandikwa vizuri na mikakati mizuri katika kipindi hiki cha mwaka 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasimama hapa ili nami niseme tu kwamba, labda wao hawakushiriki kiundani katika kupanga mipango ile ya 2006/2007 kwa sababu matarajio ya 2006 yalianza kuandaliwa toka 2005. Basi labda niseme tu kwamba, mwaka huu ndiyo tayari umeishamalizika, lakini mwakani ndiyo tunaanza kwa mipango ya nchi nzima ambayo wao wenyewe watashiriki katika kuiandaa na kuipanga mipango hiyo kwa maana ya Wizara zote ambazo zitakuwa zinapeleka Bajeti zao katika Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Wizara hii itaangalia, baadaye itarejesha na kupeleka kwenye Wizara ya Fedha na kuangalia hali ya huyu sungura atakayepatikana mwaka huu katika makusanyo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea niseme kwamba, jana usiku nilisikia kwenye Vyombo vya Habari kwamba sasa tumeishafikia makusanyo ya zaidi ya Shilingi bilioni 220 kwa mwezi. Kwa hiyo, hiyo ni dalili nzuri na sasa nchi yetu haiko tena kwenye sungura. Sungura wetu kageuka kondoo aliyenona na ninaamini mwakani hali ya malalamiko yetu, maoni yetu na taarifa zetu tunazozitoa basi mambo yatakuwa mazuri. Kwa hiyo, ninachosema ni kuiomba Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ikae vizuri iandae mipango na ielewe kwamba kuna Wizara nyingi zinazopeleka mipango yao kwao. Tutakapopata mapato hayo ambayo ninaamini mpaka mwisho wa mwaka yatakuwa makubwa, tutakuwa tumeondokana na kero nyingi. Naomba nitumie fursa hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutuongezea katika Mikoa yetu kutoka Shilingi milioni 500 hadi kufika Shilingi bilioni moja kwa ajili ya mpango wa kuendeleza hawa wajasiriamali wetu na kuweza kuondokana na hii kero na adha ya umaskini. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nampongeza kwa taarifa niliyoipata ambayo imetoka alipokuwa kule Tarime, kwa kuwapa hamasa ya kuwaangalia vizuri hawa wanaokusanya mapato. Naomba Mheshimiwa Rais awe na moyo huo wa kuwaangalia hao wanaotukusanyia mapato, lakini pia wasije wakasahauliwa na wale wanaofanya kazi katika mazingira magumu kama walimu na wauguzi wetu hasa waliopo vijijini na wao waangaliwe. Kwani na wao wanafanya kazi nzito na za tabu hasa kwa wanaokaa vijijini. Kwa hiyo, wao pia waangaliwe kwa motisha kama hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba nitazungumzia habari ya Jimbo langu la Mafia. Sikusimama mwanzoni kwa sababu kila Wizara ambayo ilikuwa ikitoa hotuba yake Mafia tuna tatizo nalo si kila Wizara ambayo unaweza ukazungumza na ukawa unaomba kitu. Mafia tuna matatizo ya pembejeo kwa upande wa kilimo, tuna matatizo ya uhaba wa watumishi afya, tuna matatizo ya upungufu wa walimu, kila idara utakayokwenda Mafia tuna matatizo nayo. Kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii kupitia

Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na kuwaambia kwamba katika mipango watakayoipanga mwaka wa 2007/2008, basi wakae watuangalie vizuri watuonee huruma sisi watu wa Mafia, adha tunazozipata ni kubwa sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru tu huu mpango ambao tayari Wizara ya Miundombinu imeuandaa. Basi naomba utekelezeke kweli, yasije yakawa tena ya kipindi kilichopita, mnatupangia hivi, baadaye pesa inatoka inakwenda kwenye miradi mingine! Mtakuja kusababisha Taifa mwakani liwe katika mtihani.

Hawa Waheshimiwa Wabunge wanaolalamika, wanalalamika kwa dhati na sisi tunaotoa maoni haya mjue kwamba tuna matatizo. Hatuongei kwa kujipendekeza kwamba wananchi wetu watusikie, tunaongea kwa uchungu na sisi ndiyo wawakilishi wao.

Mheshimiwa Spika, kila Wizara ilipokuwa ikitoa taarifa zake ilikuwa inasema: "Basi kwa kuwa mwaka huu sungura wetu mdogo, 2007/2008 na kuendelea hali itakuwa nzuri." Kwa hiyo, naomba sana hili liangaliwe hasa kwa upande wa maendeleo katika Jimbo letu la Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila mwaka Kamati ya Ushauri ya Mkoa inakaa na kila tunapokaa mara mbili au tatu huwa tunajadili matatizo ya Mafia upande wa miundombinu, gati, barabara na uwanja wa ndege. Sasa kuna siku niliongea na Mheshimiwa Waziri wa Mipango Mheshimiwa Dr. Ngasongwa, akaniambia: "Labda hamkai na kuongelea kwenye *RCC.*" Lakini napenda kusema kwamba, kwenye *RCC* tunaongea na kila *RCC* lazima suala hili lizungumzwe.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumwomba Mheshimiwa Waziri kama kuna uwezekano, sisi Viongozi wa Wilaya ya Mafia kwa kushirikiana na Mkoa wetu wa Pwani na Viongozi wa Mkoa, tupo tayari twende ofisini kwake na makabrasha yote tuliyokaa na kuyaandika na kusema matatizo haya ya gati, uwanja wa ndege na vifaa vya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Waziri, naomba labda tuje kwako au tunaomba wewe ufanye ziara. Tunaomba uwaambie watendaji wako Wizarani waje, au wewe mwenyewe amua uje Mafia uangalie hali ilivyo. Labda utakapoangalia, hali utakayoiona itaweza kuwa rahisi kukubali yale tunayoyasema na baadaye kuyapeleka katika Wizara ya Fedha ili fedha hizi ziweze kutoka na bahati nzuri hata mkiangalia, tumetoka kwenye Shilingi bilioni 150 mpaka sasa tunakaribia mpaka Shilingi bilioni 220. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi kuna uzito gani katika pato la mwezi mmoja mkatenga pato la siku mbili tu kwa maana ya Shilingi bilioni kumi na mbili (12,000,000,000/=) kwa mwaka huu tukamaliza tatizo la gati na uwanja wa ndege ili tumalize kabisa matatizo? Tena ikiwezekana sidhani kama tutakuja tena kule au mtatuona kulalamika lalamika au kusema, ni kitu kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana Mheshimiwa Rais amewaambia watu wa Tarime atatoa Shilingi bilioni 9 kwa ajili ya uendelezaji wa maji, namshukuru sana. Kasema vile baada ya kuona tatizo na kero iliyopo kule sehemu za Tarime, lakini sisi upande wa usafiri jamani maji chumvi yanawasha. Maji chumvi unaposhuka yanawasha, yanaumiza, tuoneeni huruma, tumechoka kujitosa kwenye maji chumvi. Wazee wetu wanaumia, kuna mapanga, kuna kitu kinaitwa *ulumba,* kama ikitokea bahati mbaya ukikanyaga utalia kama mtoto mdogo.

Pia, kuna taa wadogo wadogo, miiba yao ni mikali inaumiza. Hebu hii fanyeni kuwa ni mara yetu ya mwisho kusema mwaka huu kuhusu mambo ya gati. Hebu na ninyi fanyeni vichwa vyenu vichoke kusikiliza gati ya Mafia na uwanja wa ndege wa Mafia. *(Makofi)*

Waheshimiwa, nawaombeni sana jaribuni kuchoka sasa kusikiliza mipango hii ya Mafia kila siku gati, gati, uwanja wa ndege, uwanja wa ndege, vifaa, hebu chokeni safari hii. Tutoleeni hilo balaa, tupeni pesa liishe na haya mambo yapate kumalizika. Tunaona haya kila siku kusimama na kusema jambo moja tu. Japokuwa matatizo yako mengi, lakini kwanza tuondoleeni haya, hayo mengine yataondoka *automatically*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kusema, tatizo langu hilo ni kukumbushana tu. Naomba sana mwakani mtusaidie haya mambo yaishe na naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ili tuweze kuendelea na shughuli zetu za kimaendeleo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita mchangiaji anayefuata, nilipitiwa sikutoa tangazo kwamba Mheshimiwa Capt. George Mkuchika, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo ya Ulinzi na Usalama wakutane saa tano asubuhi hii chumba Namba 227, jengo la utawala.

Pili, *engineers* upande wa mitambo, leo simu zinaruhusu. Kwa hiyo, nadhani labda mmesahau kusaidia kuweza kuzima simu hizi.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nami naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kuunga mkono hoja hii iliyoko mbele yetu. Hoja imetolewa kwa ufundi mkubwa na kaka yangu Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilivyochukua kitabu hiki na kukisoma, kuna jambo dogo tu ambalo nadhani ni muhimu tulielewe kwa ajili ya baadaye. Ninaamini hiki kitabu kilicholetwa ni *document* halali kabisa ambayo tunaijadili hotuba muhimu ya mipango ya nchi. Ukienda kwenye kitabu, nyuma kuna ramani ya maeneo maalum ya uwekezaji hadi mwaka 2020. Hapa ilinipa tabu kidogo, sijui kama ni makosa ya uchapishaji ama haya ndiyo mawazo yenyewe ya mpaka tutakapofika 2020.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye kitabu hiki kuna vidoti pale. Kuna kidoti cha bluu, cha kijani, chekundu na cha njano. Chekundu kinasema ni maeneo maalum ya utalii. Ukiangalia utalii umewekwa kwamba uko Arusha, Kilimanjaro, Zanzibar, Dar es Salaam na Morogoro. *(Makofi)*

Kweli nchi hii tunataka tukubaliane kwamba mpaka kufika 2020 hakuna maeneo mengine yenye utalii! Nadhani labda kitabu kimekosewa na kama kweli haya ndiyo mawazo ya mpaka 2020, napata wasiwasi kidogo. Ukienda Rukwa najua iko Katavi, lakini bado mwandaaji wa kitabu hiki hakuona umuhimu wa kuonyesha Rukwa ni sehemu inayoweza kuchangia katika utalii wa nchi hii. Kigoma tuna Gombe na Mahale.

Ukienda kwenye *roster* ya watu wanaotaka kuja kutoka Marekani kuangalia Gombe na Mahale imejaa. Ukitaka ku-*book* leo kwenda kuangalia *chimpanzee* utapata nafasi mwaka kesho.

Lakini mwandaaji wa kitabu hiki bado hakuona umuhimu kwamba haya nayo ni maeneo ya utalii. Jamani, nadhani sasa tuondoke kwenye kufikiria kwamba utalii uko Kaskazini peke yake. *Planners* wetu msituangushe. Nchi hii Mungu ametujaalia tuna kila kitu tunachoweza kukifanya kikawa utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani labda Mheshimiwa Waziri atatumbia kwamba ni makosa ya uchapaji. Kama ni makosa ya uchapaji, basi wenzetu wawe makini. Hii ni dalili ya kulipua mambo kwa kujua kwamba kikienda kitapita tu, kwa hiyo mnaleta chochote. Hii ni dalili ya ulipuaji ambapo siyo vizuri tukau-*entertain*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hapa kuna maeneo ya viwanda. Maeneo ya viwanda yemewekwa maeneo yale yale ambayo kuna viwanda, maeneo mengine hakuna kabisa. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba, hao wachumi wetu tafadhalini sana, hii nchi ni kubwa.

Singapore wanasema wamefanikiwa kuendelea kwa sababu ya *geographical location* ya nchi yao. Tanzania na sisi nao Mungu ametusaidia tunayo *advantage,* tuna *geographical location,* lakini *second advantage* tuliyonayo nchi hii ni amani. *This country* Mungu ametusaidia tuna amani. *This is another advantage.* Sasa niwaombe *planners* wetu watumie *our geographical position* sisi kuwa na amani kuleta maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nasema ili tuweze kutoka hapa tulipo, watakaotuondoa hapa ni *planners* wetu. Niwaombe sana *planners* wetu tuondoke kwenye *traditional way* ya kufanya *planning*, dunia inabadilika kila kukicha. *(Makofi)*

Leo tunazo *challenge* kubwa tuna *globalization, how do we address ourselves* kwenye *challenge* za dunia kama tunaendelea na *style* hii hii ya ku-*plan* tutakuwa tunabadilisha lugha kila siku na mtu akituambia sasa *okay* tumemaliza miaka mitano, tuambie tumefika wapi, hakuna atakayeweza kusema. Kwa hiyo, tumefika wakati

*planners* wetu waanzie kufikiria nchi hii kuna maeneo ambayo hatuwezi ku-*invest* tena *any more*. Lakini kuna maeneo ambayo tukiyafungua nchi hii itafaidika. Mimi nasema labda tutafute *focal points* za *economy* za nchi hii *which I can say* unaiachaje Kigoma katika *planning* za nchi hii?

Mheshimiwa Spika, siyo kwa sababu natoka Kigoma, lakini kwa sababu Kigoma *geographically* iko *position very well*. Kigoma inapakana na Kongo, Kigoma inapakana na Burundi, Rwanda, Zambia kwa hiyo, kwa vyovyote vile ukasema unataka *market* wale watu, ukiangalia Kongo ilivyo Kongo *exist point* yao ni Kigoma. Lakini tusipoyaandaa mazingira vizuri hawatakuja, watatafuta *alternatives routes* hata kama ni za mbali, siyo lazima *planners* wetu tupange vizuri kuhusu reli. Reli yetu lazima iwe *competitive* tuweze kushindana na nchi za jirani.

Lazima tuhakikishe mipango yetu hii ya barabara inakwenda kwa kasi ili tuweze ku-*tap* huo uchumi wa majirani zetu. Kigoma pale tuna Kiwanja cha ndege, Kiwanja cha Ndege ni muhimu sana kwa maana ya usafiri wa watu kwenda kwa wenzetu ili tuweze kuitumia hiyo, kuleta maendeleo yetu. Kuna suala la umeme ni *agenda* hizi ili *investors* waweze kuwa *attracted* kwenda kule. *(Makofi)*

Lakini pia *focal point* nyingine ya nchi hii iko Mtwara, hatuwezi kuiacha Mtwara na Ruvuma bila kutafuta namna ya ku-*tap* uchumi wa *the other place*. Lazima twende Musoma kwa sababu Musoma *and other side of Musoma* iko Kenya, lazima twende Kagera, hizi ndiyo *new opportunity* zilizopo kwa *growth* ya uchumi wa nchi hii. *Planners* wetu wanafanya nini, *planners* wetu wamejipangaje kuweza ku-*capture* hizi *potential* mpya zilizopo za nchi hii. Kama ndiyo *planners we have* ndiyo hawa ndiyo wanadhani kwamba bado hata utalii lazima uende Kaskazini *then we are heading to tribal*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka nichukue nafasi hii, bahati nzuri ukisoma kitabu hiki wameelezea vizuri kuhusu *TIC*. Mimi nasema umefanyakazi nzuri sana *TIC* ningeomba sasa *TIC* iongezewe nguvu, ipewe uwezo wa kifedha iweze kufanya zaidi inavyofanya sasa ili kwa kweli waweze kufanya kazi nzuri kwa sababu kama bajeti zikishahohehahe tusiwategemee vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nilitaka nichukue nafasi hii kuongea kidogo kuhusu suala la uwezeshaji. Uwezeshaji ni dhana pana sana. Tunafanyaje ili kuwawezesha Watanzania? Mimi nasema moja ya *area* lazima tuhangaike nayo ni kwenye kubadilisha sheria. Kwa mfano nilikuwa naangalia kwenye *tourism industry* leo moja ya biashara kubwa *tourism industry* iko kwenye uwindaji, watu wanapewa *blocks.* Lakini tungeweka sheria tukasema ili mtu apewe *blocks* ya kuwinda kama ni *foreigner* lazima kuwepo na *component* ya mtu wa ndani. *By doing that* tutainua uchumi wa watu wa ndani, hatuwezi kuendelea kwa watu wa nje. Kwa hiyo, lazima tubadilishe sheria kwamba wewe unakuja ku-*invest* Tanzania ili iwe rahisi kwa maoni yangu mimi tukupe kufanya biashara hii biashara lazima uwe na *shareholding* ya mtu wa ndani. *So* maana yake ni suala la kubadilisha sheria tu. Lakini *empowerment* kama hatuhangaiki na kubadilisha sheria, *empowerment* hii ya nchi hii haitawafanikisha walio wengi.

Kwa hiyo, lazima tuseme leo tunauza, tunafanya *privatization* tumeshamaliza huko tulivyovibakisha mimi nasema kama kuna shirika kwa mfano wafanyakazi wamesema tuko tayari na kweli wakaonyesha wana *shareholding* na watu wengine wanaweza wakafanya nadhani *priority* iwe kwa vyovyote hawa, kwa sababu hawa tutakuwa tumewainua Watanzania walio wengi. Hatuwezi kwenda tu kwamba anakuja huyu ana mtaji *fine* haji na mtaji lakini ili mtaji uweze kupata hii kazi uwe na hawa Watanzania ndiyo namna ya kuwaokoa Watanzania wetu kwenye uwezeshaji. Naomba sana suala la sheria tuliangalie, *planners* wetu wajitahidi kwenye suala la sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nilikuwa naangalia ni suala la *education, planners* wetu lazima tujiandae kwenye *education* kwa sababu dunia ya leo ili tupate maendeleo *we need development of high quality, competent, discipline and global competitive human resources.*

Mheshimiwa Spika, sasa ili tuweze kuwapata hawa lazima *education system* zetu ziwe *demand driven,* tuaangalie *demand* ya sasa katika *education system* inataka nini, tukifika hapo tutaweza ku-*compete* na dunia ya leo. Kwa sababu dunia ya leo inakwenda mbio kweli kweli, kwa hiyo, lazima tujiandae. *(Makofi)*

Lakini pia nilikuwa nataka niwaombe *planners* wetu hasa kwenye *institutions* zinazozunguka hiyo Wizara ya Mipango, tuondoke tuache tuwape watu tu-*set targets* ili baada ya miaka mitano kama ni kiongozi wa shirika fulani aje atuambie na kweli akituambia tuelewe tumefanya nini. Lakini kama tunakwenda hatu-*set target* watu watadhani ni *business as usual* unaamka asubuhi unakwenda ofisini mimi ni *director general* narudi sina *target* ya ku-*meet* lazima tuwe *strictly* watu waweze ku-*deliver, planners* wetu wakishamaliza ku-*plan* tunakwenda kwenye *implementation* lazima kwenye *implementation* watu wawe na *targets*.

Mheshimiwa Spika, tutakuambia tuna mipango ya kujenga barabara kwa miaka hii mitano, anayesimamia barabara wala hasumbuki, haraka tuliyonayo sisi wanasiasa yeye hiyo haraka hana. Tunataka kupeleka umeme sehemu fulani, haraka tuliyonayo sisi yeye anayetekeleza hiyo haraka hana. Lakini tukimpa *targets* nina hakika tutakwenda pamoja na tutaweza kutekeleza Ilani ya Chama chetu.

Mimi naomba *planners* wetu watusaidie, maana hakuna nchi iliyoendelea bila *planners,* ukisoma historia ya *Malaysia is about planning* ndiyo nchi ile imefika pale ilipo kwa hiyo, naomba sana *planners* wetu tujaribu kufikiria kutafuta *new focal points* za *economy* za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sikuwa na mengi ya kusema nilikuwa nasisitiza tu hayo, naomba sana tutengeneza mazingira ya *private sector* kwa hali ya sasa ya dunia ili nchi iweze kwenda *private sector* lazima tuandae mazingira waweze na wao kuwa *competitive* kwenye hili soko la dunia hii. Maana yake tutengeneze *incentives* za *private sector* ndiyo *private sector* itaweza kukua tusipowapa *incentives* bado hawaweza ku-*competes*.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na mimi naunga mkono hoja hii nashukuru sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongezi kwa kazi nzuri na juhudi zinazofanywa na Waziri Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Salome Mbatia, Katibu Mkuu Dr. Bukuku pamoja na wataalam wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika sehemu chache: -

(i) Maeneo yanayopewa kipaumbele (ya mwanzo) katika kuazisha *SEZ* katika Mikoa ya Kusini na Nyanda za Juu Kusini ni Mkoa wa Ruvuma tu umeachwa, Mtwara na Lindi ipo. Lakini pia unaendeleza bandari ya Mtwara bila bandari ya *Mbamba Bay,* ni kwa tija ipi? Katika majibu ya Waziri wakati wa kujadili hotuba yake mwezi Juni, 2006 alisema Ruvuma ipo chini ya Mpango wa *Mtwara Corridor* lakini pia Mtwara, Lindi, Mbeya na Rukwa ipo katika *Mtwara Corridor*. Naomba sasa Mkoa wa Ruvuma uwe *listed* katika Mikoa itakayoanzisha *SEZ.*

(ii) Kauli ya Mheshimiwa Rais juu ya kuweka juhudi/mipango ya makusudi kuendeleza Mikoa sita ikiwemo Ruvuma, hakuna kama inavyoonekana katika hotuba ya Waziri. Ni vyema wananchi wakaambiwa ni hatua gani Serikali inachukua kuhusu kauli hii.

(iii) Kuhusu maeneo ya *SEZ,* nilipata bahati ya kuona maeneo ya *EPZ* Kenya. Maeneo yaliyotajwa ni makubwa, sekta binafsi imehusishwa sana na Serikali inatoa fedha nyingi kwa mamlaka husika. Nashauri Wizara ingejiandaa kwa mambo hayo hasa katika kutambua maeneo na kuyatenga sasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali kuanzisha Mradi wa Kutoa Mikopo Midogo (*Small Entrepreneurs Loan Facility – SELF)* kama jitihada zake za kupunguza umaskini wa kipato kwa wananchi, bado *SELF* haijajitangaza vya kutosha ili kujulikana na wananchi. Kwa mfano, katika Mkoa wa Morogoro ambako kuna ofisi ya *SELF,* tungetegemea kila Wilaya za Mkoa huu ziwe ama na ofisi au *agent* wa shughuli za *SELF.*

Mradi huu ungesaidiana na mifuko mingine ambayo ipo ili kutoa mikopo nafuu yenye masharti nafuu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya uzalishaji mali. Kwa upande wetu sisi wanasiasa (Wabunge) tumeweka hamasa kubwa kwa wananchi ili waanzishe Vyama vya Kuweka na Kukopa. Kama vyama hivyo *SACCOS* ni vidogo, ni salama zaidi kwa *SELF* kufanya biashara na *SACCOS* kwa sababu ni dhahiri fedha zitakuwa salama zaidi kwani *SACCOS* zinajua tabia za wateja wake na dhamana ya mikopo itakuwa inatokana na hizi *SACCOS.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono jitihada za Serikali katika kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi *(Mwananchi Empowerment Fund - MEF),* ni wazo zuri kuwa Serikali imeliona hili kwamba katika hali ya kawaida wananchi wengi wanashindwa kukopa kutokana na kukosa dhamana.

Mheshimiwa Spika, wananchi wakiunda vikundi vyao vya kiuchumi mara nyingi huwa wanachaguana wenyewe kwa kuzingatia vigezo vitano vya kukopesha yaani *capacity, capital, condition, collateral* na la msingi kuliko yote hayo ni *character*. Wao wanafahamiama, huo mfuko kama utashughulikia vikundi vizuri, basi utakuwa upo kama kinga tu na kwa kiasi kikubwa na hakutakuwa na *defaulters* wengi.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya uwekezaj ni sharti yaandaliwe yakiwa na miundombinu yote inayohitajika kwa uwekezaji kutegemeana na shughuli inayokusudiwa. Katika Wilaya yangu na Wilaya jirani ya Ulanga, pamoja na kwamba mazingira ya Wilaya hizi ni mazuri kwa kuwekeza kwenye kilimo, lakini Wilaya hizi zinakosa miundombinu muhimu kama barabara za kudumu kipindi chote, umeme, maji na huduma za simu. Kama tuko makini katika kuendeleza kilimo kwa kuwavutia wawekezaji, mashamba makubwa yatakayopimwa na kugawiwa na Wizara ya Ardhi sharti yawe na miundombinu iliyotajwa hapo juu.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, kuhusu mapendekezo ya kurekebisha sheria ya uwekezaji ya mwaka 1997, chini ya Muswada wa sheria wa mwaka 2006 kama ilivyopendekezwa kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha alipokuwa akiwasilisha bajeti ya Serikali ya mwaka 2006/2007 kwa mtazamo wangu ni dhahiri kabisa kwamba kuna mkanganyiko katika mfumo mzima unaoendana na sheria kifungu 26(1)(b) cha sehemu ya ix.

Katika Sheria hii stahili zilizotajwa zilizingatia muda wote wa uwekezaji. Katika marekebisho haya ya sasa muda wa stahili umepunguzwa hadi miaka mitano, mbaya zaidi ni muda huo wa miaka mitano unaanza siku ile unapopata cheti kutoka *TIC,* miradi mingi mikubwa ambayo huhitaji kujenga majengo, kufunga mitambo/mashine na kadhalika, inachukua muda mrefu, inawezekana miaka mitatu hadi mitano kabla ya uzalishaji iwapo sheria itakuwa kama ilivypoendekezwa basi mradi utakapokamilika na kuanza uzalishaji na kama miaka hiyo mitano itakuwa imepita mwekezaji atashindwa kufanya kazi katika mazingira yanayotabirika. Mabadiliko haya yanapingana sana na sera yetu ya uwekezaji.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa cheti *(TIC)* wawekezaji mara mradi unapoanza uzalishaji kwa miaka mingine mitano?

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Spika, kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha yote, kutupa umri, afya na uwezo wa kuchangia mawazo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri mwenyewe, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri na mimi natanguliza kusema naunga mkono hoja 100%.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya akinamama wa mkoa wa Pwani tunashukuru sana kwamba mradi wa *SELF* umefika, tumenufaika kwa kiasi fulani na mradi huu. Pamoja na kunufaika bado tuna matatizo nao tena matatizo ni makubwa kwani bado wanawake walio vijijini kabisa haujafikia sababu zinazotolewa eti ni usalama wa kufikisha fedha hizo, pia ufatiliaji wake wa mikopo hiyo ni mgumu. Sasa kweli majibu haya yanafanana na nia ya mradi huu au hawa wachache na wakiwa watendaji waone taabu, kushinda taabu wanayopata wanawake walio wengi huko vijijini? Lakini la kukera zaidi baadhi ya Wilaya, ya mikoa iliyotajwa huo huo mradi haupo kabisa na bado Wizara ipo kwenye kutaka kuendeleza mradi huu mikao mingine. Mfano hai Mafia haupo kabisa, na mbaya zaidi Wilaya hii hata na *NGO* nyingine zenye shughuli zinazofanana na *SELF* hazipo. Sasa sijui utakuwa tayari basi angalau *SELF* kwa jitihada yako kuwaeleza watendaji waweze kwenda Mafia na zile Wilaya ambazo zimo ndani ya mikoa tajwa ambazo *SELF* haijafika kabla ya kwenda mikao mipya.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Mheshimiwa Waziri, napenda kukukaribisha uje uwasikie na kuwaona wana Mafia, kwani naamini ukiwano na ukiwasikia utakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuwasaidia. Narudia kusema naunga mkono hoja na kuwatakia kazi njema kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nami nitumie fursa hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa kuandaa bajeti ya mwaka huu wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa Wizara hii ni nyeti sana na muhimu kwa wananchi, Taifa letu hasa katika hatua zake za kuandaa mipango na mikakati mbalimbali ambayo ndiyo dira ya Taifa letu kwa kipindi cha mwaka wa fedha, mipango inayoandaliwa ya kiuchumi, uwezeshaji ndicho kiashiria pekee kinachoonyesha njia ya kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri sasa nchi yetu ipo kwenye mikakati mbalimbali ya kupambana na umaskini wa wananchi wake, misingi hii ni mizuri kabisa na ni mwitiko wa mipango mbalimbali ya kidunia ambayo pengine imo katika harakati ile ile ya kuondoa umaskini mipango kama ile ya *Millenium Development Goals (MOGs) R10 + 10 Beiging Plat Form, CEDAW* na hata ile ya Afrika kama vile *New Partnership for African Development (NEPAD).*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri basi kama tunataka kuondoa umaskini basi yatupasa na hasa kwa Wizara kuhakikisha mikakati inayoandaliwa ilenge vijijini na mikakati hii iwe ni le inayoendana na sera za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala kupambana na umaskini limekuwa likihubiriwa kinadharia zaidi badala ya utekelezaji wa kivitendo, bado sioni mantiki juu ya ulinzi na matumizi ya rasilimali zetu tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, maandalizi yanayofanywa na Wizara juu ya uwezeshaji nayo ni ya zima moto mno bado tunahitaji chombo mbadala ambacho kifanye kazi mbadala wa Wizara. Mipango iliyobuniwa isiachwe hewani bali mipango hiyo mizuri kama vile MKUKUTA, MKUMBITA, MKURABITA na mingine mingi lazima kiwepo chombo cha uratibu na sio mipango hii kukabidhiwa kwa Halmashauri za Wilaya na pengine kudakwa na baadhi ya *NGOs* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, bado napata taabu juu ya uwekezaji unavyoendeshwa kwa nini maeneo nyeti ambayo tuna uwezo nayo kwa kuyaendeleza sisi wenyewe yanapewa wawezeshaji wa kigeni? Ningeshauri wawekezaji walio wengi hasa wageni sasa waelekezwe katika kuwekeza katika kilimo, Tanzania bado tunayo ardhi ya kutoka itakuwa busara sana kwa wawekezaji kuwekeza katika kilimo naamini nchi yetu tutasahau njaa, ajira kwa vijana itaongezeka na Pato la Taifa litapanda. Naunga mkono hoja.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono mia kwa mia hotuba ya Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, aliyowasilisha Bungeni leo ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2006/2007.

Pia nampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa kumteua Waziri na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, kwani wote kwa pamoja ni wasomi wazuri wenye uzoefu mkubwa katika Serikali na Chama. Pia Katibu Mkuu Dr. Enos Bukuku na Naibu wake Dr. Stergomena Tax Bamwenda, Wakurugenzi na wafanyakazi wote nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii.

Mchango wangu ninatoa hasa kwenye upande wa uwekezaji, tuwe macho na wageni, tujitahidi sana kuwawezesha wazalendo wazawa ambao ni waaminifu. Hii itatusaidia zaidi kukuza ajira na kutokuhamisha uchumi wetu kwenye nchi za nje mfano Uingereza, Canada au Afrika Kusini. Mzalendo huyu mzawa hata kama atakosa uaminifu uchumi wetu hautaenda nje ya nchi. Hawa watu wageni wanaweza kutusaidia pale tunapoona wazalendo hawana ujuzi, elimu na utaalamu hapo inabidi tuwaombe kuwekeza pamoja na wazawa wazalendo.

Mheshimiwa Spika, pia hao wazalendo wawezeshwe hasa kwenye mitaji ya Mabenki na vyombo vya fedha. Pia Serikali iwawezeshe kupata masoko ya ndani na nje ya nchi.Mfano wenzetu Wajapan Kampuni ya *Toyota,* Serikali inawezesha Kampuni hii kwa masoko hata kama Kampuni hii ni binafsi. Nasema hivyo kwa vile nilikuwa kule kimasomo na Serikali ya kule ilitusaidia sana kupata elimu hiyo. *The Corporate Management for Africa.*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Naibu Waziri Mheshimiwa Salome Mbatia, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri na ambayo imewasilishwa kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi sasa nianze kuchangia bajeti hii kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nianze kuipongeza Serikali kwa kuleta Sera ya MKUKUTA ambayo lengo lake ni kuwawezesha wananchi kuondokana na umaskini. Naishukuru Serikali kwa kuendesha semina mbalimbali kwa viongozi na watendaji wa ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali sasa iweke mkakati wa kuanza kutoa semina kwa wanawake na vijana na kadhalika ili kuwawezesha waweze kuendesha miradi yao vizuri kuliko ilivyo sasa wanaendesha kwa kubahatisha tu hawana taaluma yoyote ili waweze kutekeleza wito wa MKUKUTA. Wananchi wetu hasa waliopo vijijini hawana kabisa taaluma ya uendeshaji miradi yao.

(b) Kuhusu Mfuko wa Maendeleo**,** naipongeza Serikali kwa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo kupitia Benki ya Dunia kusaidia Halmashauri zetu zilizopata hati safi. Naomba masharti yalegezwe kwani Halmashauri nyingi zinakosa fedha hizi kwa ajili ya kutotimiza vigezo vyote, kwani vipengele vingine sio vya muhimu sana. Hali hii isiwasababishie wananchi wa maeneo mengi ambao wako kwenye mikoa ambayo bado ipo nyuma sana kimaendeleo.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu uwekezaji kwenye raslimali, naipongeza Serikali kwa kutambua rasilimali ambazo tunazo humu nchini na naipongeza kwa kuona umuhimu wa kuruhusu wawekezaji kuwekeza, bali naishauri Serikali kutoa kipaumbele kwa wazalendo (Watanzania) kuwekeza kabla ya wageni kupewa kama wapo ili fedha yetu isitoke nje na kunufaisha Watanzania.

(d) Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyabiashara ndogo ndogo, nawapongeza sana Watanzania wanaochacharika katika kuendesha biashara ndogo ndogo. Naiomba Serikali iwasaidie Watanzania hawa kwa kuwapa elimu na kuwakopesha ili kukuza mitaji yao ili biashara zao ziweze kwenda vizuri.

(e) Kuhusu Miradi ya *TASAF,* napenda kuishukuru Serikali kwa kuanzisha Mifuko mbalimbali ya kuendesha Miradi ya Maendeleo ikiwa ni pamoja na *TASAF*. Hata hivyo naishauri Serikali kuteua waratibu wenye uwezo na waaminifu ili fedha hizi ziweze kufanya kazi zilizokusudiwa na Serikali pamoja na wahisani wetu. Vile vile usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hii uwe na karibu sana.

(f) Mheshimiwa Spika, kuhusu ukusanyaji wa takwimu, mpango wa Serikali wa kukusanya takwimu mbalimbali uwe wa mara kwa mara kwani mabadiliko ya takwimu

hutokea mara kwa mara mfano idadi ya watu, vijana, mifugo na kadhalika. Hii itatusaidia kuweka mipango yetu ya maendeleo vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa nitamke rasmi kuwa naunga mkono hoja hii.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo maalum ya viwanda hadi mwaka 2020. Jambo hili ni muhimu sana ili maendeleo kamili yapatikane, kinachosikitisha ni kuwa Mikoa ya Kusini na hasa Mkoa wa Ruvuma hakuna mpango wowote wa kunzisha viwanda, tumekosa nini sasa? Chakula kutoka Ruvuma, tumbaku kutoka Ruvuma, Kahawa kutoka Ruvuma. Viwanda hakuna, maendeleo gani haya?

Mheshimiwa Spika, ile kauli ya Mheshimiwa Rais ina *impact* gani kwa mikoa hii? Rais alisema na kuagiza kuwa sasa maendeleo yaelekezwe Mikoa ya pembezoni kama Ruvuma, Rukwa, Mtwara, Lindi, Kigoma na kadhalika. Sasa mpango huu wa kutoleta viwanda Ruvuma inashabihiana vipi na kauli ya Rais wetu? *Are you serious?* Hadi miaka ishirini ijayo hakuna mpango wa viwanda, kwa hiyo tuhame? Kwa nini Morogoro, kwa nini Arusha, kwa nini Tanga? Ruvuma je?

Mheshimiwa Spika, naomba nihakikishiwe juu ya marekebisho ya mpango huu ama sivyo nitaendelea kuamini kuwa sisi ni Watanganyika na wao ni Watanzania. Keki hii ya Taifa naomba maelezo ya kina. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wao wote kwa kazi nzuri mnayoifanya. Sina matatizo makubwa na Wizara yake ila naomba kauli yake juu ya mambo nitakayoyaandika.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi wanategemea kilimo katika kuinua uchumi. Wengine wachache wanategemea viwanda vidogo na wachache zaidi wanategemea viwanda vikubwa ukiangalia kilimo cha Mtanzania bado ni duni sana kwa mantiki kuwa hakimsaidii kujenga uchumi bora ilizingatiwa na idadi ya Watanzania wengi kinachangia asilimia 5.7 tu ya Pato la Taifa. Umefika wakati ambapo Serikali lazima ibadilishe mikakati yake, lengo kuu sasa liwe ni kuwasaidia wananchi waanze kulima kisasa. Pia Serikali isaidie kuanzisha Benki ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuboresha kilimo ni lazima ichukue hatua za makusudi kumaliza barabara ambazo imeshaanza kuzijenga kwa mfano Dodoma-Manyoni - Singida - Shelui, barabara ya Kusini na zingine ambazo hazijaanza. Kwa mfano barabara za Minjingu-Singida kupitia Babati, Babati - Iringa kupitia Dodoma na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kumwomba Mheshimiwa Waziri aanze kuzifikiria barabara za kukuunganisha Mikoa mbalimbali. Kwa mfano barabara

inayounganisha Mikoa ya Kanda ya Ziwa, Shinyanga, Mwanza Mara, Kagera na nchi za jirani na Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Tanga kupitia Iramba Mashariki. Kikwazo cha kuunganisha Mikao niliyoitaja ni kukosekana kwa daraja la Mto Sibiti.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri akihitimisha hotuba yake atamke juu ya mipango thabiti ya barabara ikiwepo daraja la Mto Sibiti.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa unahitaji mipango madhubuti ili uweze kuibua rasilimali zake kwa ajili ya maendeleo ya Mkoa na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara haijatoa mipango ya kusaidia Mkoa huu uweze kuendelea katika viwanda. Mfano, tunayo machimbo ya mkaa ya mawe. Naelewa hakuna chohote mahali popote kinachozungumzia machimbo hayo.

Mheshimiwa Spika, biashara ya mpakani soko la mazao na mifugo Kasesya na Kasanga kati ya nchi jirani za Zambia na Kongo hakuna mahali popote inapozungumzwa. Ipo rasilimali ya samaki. Katika Ziwa Tanganyika na Rukwa, samaki wanavuliwa na nchi jirani za Kongo, Zambia na Burundi, lakini sisi Mkoa wa Rukwa hakuna mipango ya maana ya kuvuna rasilimali hii kwa ajili ya kuondoa umaskini wa wananchi wangu wa Kalambo. MKUKUTA, MKURABITA na mengine yanayozungumzwa na Wizara hii bado haijaweza kuwafikia wana Rukwa na Jimbo la Kalambo ili kuondoa umaskini wao, Wilaya Nkasi, Mpanda na Kigoma wanalalamikia jambo hilo hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchumi wa kijiografia, Tanzania imekaa vizuri kuchota uchumi wa Kongo, Zambia na Burundi kupitia Bandari ya Kasanga bila matatizo yoyote. Je, ni mipango gani Wizara hii ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji imeandaa ili kuchota uchumi wa Kongo? Mheshimiwa Rais aliahidi barabara ya Tunduma - Sumbawanga na Sumbawanga - Kasanga ijengwe kwa kiwango cha lami ili tuchote uchumi wa Kongo, aliahidi pia Bandari ya Kasanga iboreshwe kwa minajili hiyo hiyo.

Sasa mipango ya Wizara hii kwa maandalizi ya kubeba mizigo, *processing* ya Shaba Kasanga, uvuvi wa kisasa, *processing* mazao ya kilimo, upatikanaji wa umeme na kadhalika. Inasikitisha kuona kuwa Mkoa, Wilaya na Jimbo la Kalambo ni wasindakizaji wakati wana *potential* ya jiografia ya kiuchumi, lakini yatima wasio na mlezi Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mipango.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara kwa kuandaa bajeti nzuri . Pia na mawasilisho mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Naipongeza Wizara nzima kwa utendaji na uendelezaji wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu ubinafsishaji, nadhani katika ubinafsishaji wananchi wapewe upendeleo maalum. Hii ni kwa sababu hawa ndio wenye uchungu na maendeleo ya nchi hii.

Tatu, maendeleo ya nchi nzima sawia. Nashauri jitihada zifanywe ili maendeleo yasambazwe sawia nchi nzima. Miradi igawiwe kwa kuzingatia maeneo/Mikoa ambayo ina maendeleo ya *facilities* duni ili tusonge mbele kama Taifa kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, zifanywe jitihada za kusambaza viwanda nje ya Dar es Salaam, kurundika viwanda Dar es Salaam kunafanya hata kuwe na msongamano wa maisha Dar es Salaam, watu na magari. Wizara hii ina uwezo wa kuvutia viwanda vijengwe katika maeneo yaliyochaguliwa na nne, kuhusu uwezeshaji, hili liwekewe mkazo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa mipango mizuri na kazi nzuri.

Naomba nimnukuu Mheshimiwa Waziri kuhusu mashamba ya *NAFCO* Basotu ambayo yalibinafsishwa lakini mashamba mawili ya Gawal na Warret yalirejeshwa kwa wananchi kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Hanang. Naipongeza Wizara kwa uamuzi huu ulionufaisha wananchi wa Wilaya ya Hanang ambao wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa ardhi. Kutokana na uhaba huo watu walio karibu na Mlima Hanang wamekosa eneo la kulimia baada ya mazingira ya Mlima Hanang kukumbwa na uharibifu mkubwa. Pia tuna vijana wengi hawana ajira hasa ukizingatia Wilaya ya Hanang ni Wilaya ya kilimo na hapana shughuli nyingine ya kiuchumi, tatizo ambalo Wilaya imejikuta kupewa mzigo wa madeni takriban shilingi bilioni 1.5 ambalo uwezo wake kifedha haiwezi kuhimili.

Naomba Wizara ichukue mali inayohamishika iweze kuuza ili fedha zitakazopatikana ziweze kutumika kulipia madeni niliyotaja. Uwezo wa Halmashauri ya Hanang ni mdogo kusimamia uuzaji wa mali za mashamba. Ninachopendekeza mfilisi aliyeuza mali za mashamba mengine ya Basotu aweze kupewa kazi hiyo kwani ana uzoefu nayo.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru na kuwapongeza tena, nitafurahi kama Waziri atajibu hoja yangu wakati wa majumuisho.

**MHE. JUMA. A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema nikianza kumpongeza Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa kuwasilisha vizuri hotuba ya Wizara yake. Pia nawapongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote wa Wizara hii kwa yote mazuri yaliyofanywa kwa kipindi cha mwaka 2005/2006.

Napenda kushauri yafuatayo, kwanza, Tanzania ina kila aina ya vyanzo vya uchumi kama vile Gesi, Madini, Samaki wa kila aina kuanzia wale wa Bahari ya Hindi hadi Maziwa Makuu. Vyanzo hivi vinatosha sana kuondoa Tanzania kwenye kundi la aibu la kuitwa nchi maskini. Ni vema Serikali ikachukua hatua za makusudi na zenye lengo la kuondokana na unyonge wa umaskini wakati raslimali tunazo nyingi mno.

Pili, nimepitia hotuba yote ya bajeti hakuna panapotamka lolote kuhusu ukanda wa uchumi wa Mtwara yaani *Mtwara Corridor*. Hali hii tujifunze nini? Ni lini Serikali itaanza kutenga na kutekekeleza uendelezaji wa mipango au miradi ya uchumi iliyoko katika ukanda huo ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga na kadhalika.

Tatu, mabenki kuchangia sana katika kukuza uchumi wa nchi. Utaratibu uliopo hapa kwetu Tanzania wawekezaji wa mabenki wamepewa uhuru wa kuamua wao wenyewe wapi kwa kuwekeza. Matokeo yake kwa hali ya *infrastructure* ya baadhi ya maeneo wawekezaji hao hawaendi huko mfano Wilaya za Tandahimba, Namtumbo na kadhalika licha ya kuchangia na kuwa na rasilimali za uchumi kwa nchi yetu bado hatuna mabenki. Wananchi hulazimika kwenda mbali kutafuta huduma hizo,ni maoni yangu kuwa ni vema sasa mkakati ukaanzishwa ili kuhakikisha angalau benki kwa kila Wilaya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nne, kuna tatizo la upungufu wa watalaam katika fani ya utumishi katika ngazi za Wilaya nchini ambako ndiko Watanzania wengi waliko na hata vyanzo vya uchumi ndiko viliko. Ni ushauri wangu kuwa ni vyema Serikali ikaanzisha mpango/mkakati wa watalaam wa uchumi kupelekwa Wilayani au vijijini kwani kwa kuwepo kwao kule kutasaidia na kurahisisha uibuaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali iongeze kasi ya kufungua vituo vya uwekezaji kwa haraka hasa kwa Mkoa wa Mtwara kwani ina rasilimali ya bahari na gesi ya *Mnazibay*. Kuwepo kwa rasilimali hizo kutakuwa kivutio kwa wawekezaji. Naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nilikuwa nimechelewa kuipata karatasi hii maalum, nilikuwa nimeshaandika kwenye karatasi niliyoambatanisha hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ukubali kuupokea mchango wangu. Awali ya yote napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri na hotuba yake iliyotolewa leo hii tarehe 11 Agosti, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepatwa na mshangao mkubwa kuona kuwa Wizara hii bado haijaona kabisa umuhimu wa kuwepo kwa viwanda katika mkoa wa Ruvuma kama njia pekee ya kumkomboa mwananchi wa Ruvuma, ambayo analima sana mahindi, maharage, tumbaku, korosho, maembe, machungwa, ndizi, matunda Mungu, *peaches,* kahawa na maarufu kwa uvuvi wa samaki hasa Mbasa ambao ni watamu sana. Hali hii inanirudishia hisia kuwa Wizara yako imeamua kutengeneza pepo katika baadhi ya

maeneo bila kujali maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais ya kuikomboa mikoa iliyopo pembezoni. Wote mnafahamu juu ya mpango wa Taifa wa kupeleka umeme wa gridi mkoani Ruvuma, umeme wa kilovolti 132 ambao tayari umeshafanyiwa tathmini.

Mheshimiwa Spika, hali hii ya kutokuwa na mpango wa kuweka viwanda eneo la mkoa wa Ruvuma ni kukwamisha juhudi za Serikali na hatimaye wananchi wa Tanzania. Aidha, inaeleweka kuwa umbali wa kutoka Ruvuma kwenda Mtwara au Iringa ni mrefu. Hali kadhalika mkoa wa Ruvuma upo mpakani kiasi cha kuweza kuuza mazao yake nchini Malawi nchi ambayo ipo *locked.* Hivi kweli miaka 14 wananchi wa Ruvuma wawe wanaangalia tu? Bora hata mngetamka kiwanda kimoja tu cha samaki na matunda tungeona angalau kuna ukweli ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipotembelea Liuli wakati wa kampeni alikiri na akaahidi umuhimu wa kuendeleza utalii katika Ziwa Nyasa, Ziwa safi, lenye *cliff* nzuri na *best diving places*. Tunawashauri mtembelee siku moja ili mjionee *what you are missing.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri atamke wazi mpango wake aliouonyesha kwenye jalada (ramani ya Tanzania utafanyiwa marekebisho na kuafikiwa Mikoa iliyoachwa pamoja na Ruvuma. Ahsante sana.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, wananchi wanaoishi katika mwambao wa Ziwa Nyasa na hasa Wilaya Ludewa hawana namna yoyote ya kujiendeleza kiuchumi au kuongeza kipato chao isipokuwa uvuvi katika Ziwa Nyasa kutokana na mazingira ya miteremko mikali ya milima ya *Livingstone* inayoteremka moja kwa moja mpaka Ziwani. Maeneo haya ni mazingira mazuri kufikiriwa kwa utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kuongeza Kipato *(NIGP)* kama ilivyoelezwa katika ukurasa 37 wa hotuba ya Waziri pamoja na Sera ya Taifa ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kama inavyopendekezwa ukurasa 57 (sehemu ya 60). Serikali kupitia mbinu mpya na za kisasa za uvuvi kuwapa vifaa bora na vya kisasa ili kuwawezesha.

Mheshimiwa Spika, wakati sheria ya mazingira ya mwaka 2004 inaagiza pamoja na mambo mengine kuwa mikakati na mipango yote ya maendeleo hapa nchini yafanyiwe tathmini ya mazingira ya kimkakati yaani *Strategic Environmental Assessment (SEA)*kwa nini Wizara hii inaendelea kubuni na kutekeleza mikakati na sera mbalimbali kama vile mkakati wa kubinafsisha mashirika ya umma kama *TRC, NIC, TAZARA, SEZ* na kadhalika bila kufanya tathmini ya mazingira ya kimikakati kama sheria inavyoagiza? Matokeo yake ni pamoja na mikakati hii kutofanikiwa na kuliingizia Taifa hasa ambazo zingeweza kuepukika.

Kwa kuwa miradi mikubwa ya Mchuchuma na Liganga Wilayani Ludewa inatarajiwa kuanza kutekelezwa katika kipindi hiki cha miaka mitano (2006/2007-2009/2010), Serikali haioni busara katika kuanzisha au kufungua Ofisi ya Kanda Mkoani Iringa kama ilivyofanya huko Mwanza na Kilimanjaro kwa ajili ya kuwahudumia wawekezaji katika miradi hiyo na inayohusiana na hiyo?

Mheshimiwa Spika, vigezo vilivyotumiwa kuchagua kijiji cha Mbola Mkoani Tabora kuwa kijiji cha Milenia hazieleweki. Kipindi kimoja cha mvua, kilimo cha mahindi katika maeneo ya Miombo vyote hivi vinaacha nje maeneo yenye kipindi kimoja cha mvua yenye miombo na yanayolima mahindi Kusini mwa Tanzania na Nyanda za Juu za Kusini, uchaguzi huu wa Kijiji cha Mbola haukuwa wa kisayansi.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wao kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo wa kuinua uchumi wa nchi pamoja na kutoa nafasi ya kukuza ajira.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na kuanzishwa kwa mfuko wa dhamana wenye lengo la kutafuta tatizo la kupata huduma za kifedha. Naiomba Wizara kuutangaza Mfuko huu ili wananchi waufahamu vizuri na waweze kuutumia hasa wafanyabiashara ndogo ndogo/wadogo ambao ni wengi sana nchini. Nashauri Wizara iendelee kuanzisha Baraza la Uwezeshaji ngazi ya Mkoa na Wilaya na Wabunge wawe wajumbe wa Baraza hilo katika ngazi ya Mkoa na Wilaya. Aidha napendekeza *TASAF* ni vyema ikahamishiwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, mwisho suala la kufufua viwanda vya korosho hapa nchini nalo linahitaji msukumo mkubwa wa kutoka Wizara hii kama alivyoizungumzia katika mpango mkuu wa Taifa.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwake na kwa ushindi wa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na kumpongeza Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, kwa hotuba yake na kusimamia vyema Wizara.

Mheshimiwa Spika, mipango ya uchumi wetu Tanzania ni muhimu na unategemea elimu, semina, uongozi imara na kujali maslahi ya Tanzania yetu. Naomba Serikali itoe uwezo wa kifedha kuwezesha Wizara na Waziri na Naibu Waziri na watendaji wake wasimamie na kutekeleza kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni na kwa niaba yangu, naunga mkono hoja asilimia zote.

**SPIKA:** Ahsante sana nakushukuru sana Mheshimiwa, sasa ni ile ngwe ya Waheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri. Kwa mpangilio huo kuweza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Salome Mbatia kwa dakika 20, wameigawa ile saa moja na robo waliyonayo dakika 20 Naibu Waziri na dakika 55 Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima kubwa naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa

kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CCM, kwa kura nyingi zenye heshima iliyotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, naendelea kumshukuru kwa kuniteua mimi Naibu Waziri mwanamke wa kwanza katika Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Naomba nimuahidi Mheshimiwa Rais kufanyakazi kwa utii, juhudi na maarifa, ushirikiano na uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze vile vile Mheshimiwa Mzee Yusuf Rajab Makamba, kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Naomba vile vile niipongeze timu mpya ya makatibu wa *NEC* wa CCM kwa kuteuliwa katika nyadhifa zao mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Rostam Aziz kipekee ambaye ndiyo niliyemkabidhi kijiti cha Ukatibu wa *NEC* Uchumi na Fedha. Ninamtakia mafanikio makubwa ili naye baadaye aweze kukikabidhi kijiti hicho salama wakati ukifika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niwapongeze Wenyeviti wapya wa Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, pamoja na Mheshimiwa Job Ndugai, kwa kuchaguliwa na kuanza kazi yao vizuri. Aidha, nina deni kubwa kwa akinamama wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kunichagua kwa kura nyingi asilimia 94.5 kwa mara nyingine kuendelea na Ubunge. Ninawaahidi kuwa nitakuwa mtumishi wao mwaminifu na ninaendelea kuwashukuru na nitawajali na kuwaheshimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, kwa kunifundisha kazi na kuwa kaka mkubwa kwangu na rafiki katika utendaji kazi. Mheshimiwa Waziri, nitaendelea kuwa mwaminifu na msikivu na mwanafunzi mzuri kwako. Aidha, ninawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, wakiongozwa na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wao wa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kuchangia hoja iliyo mezani ya hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2006/2007 kwa kujibu baadhi ya hoja za Wabunge kama ambavyo nitafanya sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumegawanya hoja za Waheshimiwa Wabunge, pamoja na majibu katika makundi makubwa saba. Makundi haya ni pamoja na kundi la kwanza, kuhusu hoja na majibu yaliyohusu sera za jumla, kundi la pili, ubinafsishaji, uratibu na udhibiti wa mashirika yaliyobinafsishwa, tatu, uwekezaji, nne, uboreshaji wa miundombinu, tano, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, sita, ujenzi wa uwezo wa takwimu na saba, utekelezaji wa mipango, programu, mikakati ya kitaifa tuliyojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba, nianze kwa kusema kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge, ilikuwa ni michango mizuri sana. Kwa kweli hapa kama ni masuala ya kiwango, viwango vilikuwa ni vya hali ya juu na kwa namna hii tunapata changamoto kubwa sisi tulio Serikalini ili tuweze kufanyakazi kwa makini zaidi kwa maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, sasa katika kundi la kwanza la sera za jumla, Waheshimiwa Wabunge, waliochangia hoja hii ni pamoja na Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Kabwe Zitto. Hoja ya kwanza kuwepo na ufuatiliaji wa mwenendo wa kiuchumi kwa namna ambavyo itawezesha uchumi wa Tanzania kuhimili mabadiliko ya thamani ya fedha za kigeni. Kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, upo utaratibu wa kufuatilia viashiria muhimu vya uchumi ikiwa ni pamoja na mwenendo wa mabadiliko ya thamani ya fedha za kigeni. Inapobainika kuwa mabadiliko hayo ni makubwa kwa kiasi cha kuathiri mwenendo wa uchumi wetu upo utaratibu wa Benki Kuu ya Tanzania kuingilia soko la fedha za kigeni yaani *inter bank foreign exchange market* ili kutengamaza thamani ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine katika kundi hili ni kwamba iweje sekta ya viwanda inachangia asilimia 9.5 katika Pato la Taifa wakati sekta ya kilimo inayobeba asilimia 80 ya Watanzania inachangia asilimia 5.7 tu ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo haichangii 5.7% tu ya Pato la Taifa. Katika kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2005 tulichowagawia Waheshimiwa Wabunge, mwezi Juni, 2006 wakati tukiwasilisha kwenu Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2005 ukurasa wa 18 jedwali namba 4 (b) linaonyesha baada kuwa mchango wa sekta ya kilimo ni asilimia 45.6 na kwa hakika ndiyo sekta yenye mchango mkubwa katika pato la Taifa zaidi ya sekta nyingine zote.

Mheshimiwa Spika, katika hoja za kundi (b) yaani ubinafsishaji, uratibu na udhibiti wa mashirika yaliyobinafsishwa Waheshimiwa Wabunge, waliochangia hoja hii ni pamoja na Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Godfrey Zambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ni kwamba matatizo yanayoikabili *ATCL* na yale ya mikataba ya uongozi wa *TANESCO* yapate ufumbuzi wa haraka. Tunafarijika kusema kwamba Serikali iko katika mchakato wa kuyatafutia ufumbuzi matatizo haya. *(Makofi)*

Hoja nyingine inasema muda wa ukodishaji wa *TRC* miaka 25 ni mrefu mno, kwa nini mali zisizo za msingi za *TRC* zinauzwa wakati shirika linakodishwa? Muda wa ukodishaji wa *TRC* kwa miaka 25 unazingatia wastani wa uzoefu wa Kimataifa wa muda wa ukodishaji wa masuala kama haya. Pamoja na urefu wa muda huo kutakuwa na tathmini kila baada ya miaka mitano na mali zinazouzwa na ni *core assets* kama hoteli,

hospitali na zahanati hazihusiani moja kwa moja na biashara ya uendeshaji wa reli. Lakini hata hivyo fedha zinazopatikana huwa zinaingia katika Mfuko wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja kwamba kwa mujibu wa taarifa idara ya usimamizi wa bima nchini *NIC* inaongoza kuwa na *market share* kubwa kwa nini Serikali imechukua uamuzi wa kuliuza shirika hili? Kuanza mwaka 1992 Serikali iliamua kujitoa katika shughuli za biashara na kuipa sekta binafsi nafasi ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi za Taifa. Aidha, Serikali imeamua kukuza ushindani katika biashara ya bima ili kuleta ufanisi na huduma bora kwa wateja. Serikali, itachukua tahadhari gani katika kusimamia na kuhakikisha kuwa Mkataba wa *Rights* unatekelezwa kwa mujibu wa makubaliano. Majadiliano baina ya Serikali na Kampuni ya *Lights* bado yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko kutoka kwa wakulima kwamba toka mwaka 2004/2005 hadi 2005/2006 mmiliki wa Kiwanda cha Mtibwa kwa makusudi alikataa kununua miwa ya wakulima wakati tayari imeshakatwa. Serikali ilifuatilia suala hili ili kubaini ukweli na ili iweze kushauriana na mwekezaji ipasavyo. Hata hivyo utaratibu wa *out growers* unataka pawepo na mkataba kati ya mmiliki na *out growers* wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kwa nini bei ya bidhaa kama sukari toka Mtibwa inakuwa ya juu kuliko inayotoka nje? Sukari ni mojawapo ya bidhaa ambazo wazalishaji wa nchi zilizoendelea hupewa ruzuku ya kuwawezesha kuhimili ushindani katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu unachangia sukari ya Tanzania kuonekana ni ya bei ya juu. Tatizo hili linafanyiwa kazi katika majadiliano ya biashara ya Kimataifa. Sababu nyingine ni pamoja na kiwango kidogo cha uzalishaji yaani *low production and low economies of scale* wakati ambapo viwanda vyetu vinatekeleza mipango ya kupanua uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, ajira katika sekta ya viwanda nchini ni watu 126,052 mwaka 1995 na katika mwaka 2005 imeshuka hadi watu 88,713 tu. Ikaulizwa pia kuwa Serikali iwaeleze Watanzania ni kweli uuzaji wa viwanda umeongeza ajira au umezidi kuwafanya wasiwe na ajira na kwa nini kumekuwa na punguzo kubwa kiasi hicho cha ajira katika sekta hii?

Mheshimiwa Spika, baadhi ya idadi ya ajira mwaka 1995 ilikuwa ni ya kitakwimu. Wengi wa wafanyakazi hao walikuwa wamepewa likizo ya muda mrefu kufikia hadi muda wa miaka mitatu, bila malipo. Mifano hai ni viwanda vya *UFI, URAFIKI, Tanzania Elimu Suppliers, Polytex, Mutex, Tanzania Bank Cooperation, Kilimanjaro Hotel, NASACO* na kadhalika, baada ya ubinafsishaji ilipungua lakini ilikuwa ya halisi. Wafanyakazi wapo kazini na wanalipwa mishahara. Kabla ya ubinafsishaji viwanda vingi havikuzingatia uwiano baina ya wafanyakazi na mtambo unaokubalika Kimataifa na tija ya wafanyakazi ilikuwa ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano wafanyakazi wanne wa Kiwanda cha Urafiki walikuwa wanahudumia mitambo ambayo inahudumiwa na mfanyakazi mmoja kwenye kiwanda cha aina hiyo nchini China. Kiwanda cha *SPM* kiliajiri wafanyakazi 1300 ambapo idadi halisi iliyokubalika na kiwanda ilikuwa ni wafanyakazi 800 tu. Hivyo, ilibidi Serikali yenyewe kupunguza wafanyakazi 500 kama sehemu ya mkakati wa kupata mwekezaji. Aidha, Kampuni ya Viatu ya Bora kwa mfano iliwaajiri watumishi kwa ajili ya kucheza ngoma. Aidha, katika maeneo ambapo mashamba makubwa ya miwa na chai yamebinafsishwa kumekuwa na ongezeko la wakulima wadogo wadogo wa miwa na chai waliojiajiri yaani *out growers* wanaouza mazao yao kwenye makampuni yaliyonunua mashamba makubwa na hivyo kujipatia kipato.

Mheshimiwa Spika, katika kundi la uwekezaji Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni pamoja na Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Mohamed Sinani, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, hawa ndiyo wamechangia hoja zinazohusu uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja inasema juhudi zaidi zinapaswa kufanyika kuhakikisha kuwa uwekezaji nchini unafaidisha wananchi na rasilimali za nchi zinalindwa. Pamoja na matatizo yaliyojitokeza kuhusu uwekezaji, kwa kiasi kikubwa uwekezaji nchini umeleta faida kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kukuza ajira, kuongeza uzalishaji na huduma, kuanzishwa kwa *down stream business activities* kwa mfano viwanda vya *TBL,* ulimaji wa shahiri, mahoteli kwa mfano Kilimanjaro, kuibua bidhaa za huduma inazonunua katika soko, mawasiliano kwa mfano kampuni za simu za mkononi zimerahisisha mawasiliano na kuchangia kukuza biashara, kuchangia mapato ya Serikali kupitia kodi mbalimbali, kukuza teknolojia, kupata fursa katika masoko *(access markets),* kukuza uwezo wa kibiashara, kuanzisha mifumo ya usambazaji bidhaa *(supply changes na value changes)* na kuundwa kwa vikundi vya uzalishaji yaani *cluster information*. *(Makofi)*

Aidha, Serikali itaendelea kuchukua hatua ili kuhakikisha kuwa rasilimali za nchi yetu zinalindwa kwa kutumia sheria, kanuni na vyombo mbalimbali vya udhibiti.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine inasema kwamba uwekezaji umejikita katika Mikoa michache. Hali ya uwekezaji nchini inafuata mfumo na mtandao wa miundombinu uliopo kwa kuzingatia kuwa mfumo wa miundombinu tuliyorithi haukuwa na mtandao mkubwa, Serikali imeamua kuboresha na kupanua ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje katika maeneo mbalimbali lengo likiwa ni kuunganisha nchi na kuibua fursa mpya za kiuchumi na za kimaendeleo. Serikali inadhamilia kuwepo maendeleo yanayohusisha wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, lingine kuwa kasi ya kufufua vituo vya uwekezaji vya Kanda iongezeke, pia wawekezaji wapelekwe katika Mkoa wa Ruvuma. *Tanzania Investment Centre* imeongeza kasi ya kufungua vituo vya Kanda, tayari kuna Ofisi ya Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kusini iliyopangiwa kuwa na ofisi Mtwara itafunguliwa hivi karibuni ndani ya mwaka huu wa fedha. Kanda hii kama mnavyojua vile vile itajumuisha Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kwamba kwa nini hakuna mpango wowote wa kuanzisha viwanda kule Ruvuma? Serikali haianzishi viwanda kama ilivyokuwa nyakati za uchumi hodhi, badala yake Serikali inatunga sera, kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika Mikoa yote ukiwemo Mkoa wa Ruvuma. Serikali itaendelea kuweka mazingira bora katika Mkoa wa Ruvuma ili kuwavutia wawekezaji katika Mkoa hususan katika sekta ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine inasema wawekezaji walio wengi hasa wa kigeni waelekezwe katika kuwekeza katika sekta ya kilimo. Tayari Serikali imeweka vituo vingi katika sekta ya kilimo na pia inatekeleza programu ya *District Agricultural Development Program (DADP)* chini ya programu hii kuna mikakati ya kutayarisha miundombinu ili kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, pia tunawashauri Waheshimiwa Wabunge, kuwahamasisha wajasiriamali ili kutumia fursa zilizopo, pamoja na juhudi nyingine Serikali imefanya marekebisho ya sheria ya ardhi ambayo inavutia zaidi wawekezaji katika sekta hii.

Aidha, kwa kuwa wawekezaji huchagua maeneo ya kuwekeza kwa kuzingatia vigezo vya kiuchumi na kibiashara, Serikali itaendelea kutangaza fursa zilizopo katika sekta ya kilimo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi la wachangiaji sasa ni (d) yaani katika kundi la uwezeshaji. Waheshimiwa Wabunge, waliochangia hoja hii ni pamoja na Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Juma Killimbah na Mheshimiwa Kabwe Zitto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ilisema Serikali iharakishe kuanza kazi kwa barabara la uwezeshaji ili mipango yote ya uwezeshaji ipitie katika barabara hiyo. Baraza la Taifa la Uwezeshaji lilikwishaanzishwa na kuanza kutekeleza majukumu yake mnamo mwezi Novemba, 2005. Aidha, Sekretarieti ya Baraza hilo ipo katika hatua za mwisho za kuanzishwa na mipango yote ya uwezeshaji itaratibiwa kupitia chombo hiki.

Hoja nyingine ni kwamba Wizara ianzishe mabaraza ya uwezeshaji katika ngazi za Mikoa na Wilaya na Wabunge wawe wajumbe wa Mabaraza hayo. Utaratibu wa mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi umeshaandaliwa na katika utaratibu huu patakuwa na Kamati za Mikoa na Wilaya na Waheshimiwa Wabunge, watakuwa wajumbe wa kamati hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *SELF* iliahidi kupeleka shilingi milioni 800 Mkoa wa Ruvuma, badala yake zimepelekwa shilingi milioni 55 tu. Mradi wa *SELF* hauna utaratibu wa kutoa mikopo kwa kuweka viwango vya mikopo kwa kila Mkoa. Mikopo hutolewa kwa asasi za fedha zinazotimiza masharti na vigezo baada ya kufanyiwa tathmini.

Mheshimiwa Spika, hadi Juni, 2006 asasi nne za Mkoa wa Ruvuma zimekopeshwa jumla ya shilingi milioni 123. Asasi hizo ni pamoja na *Songea Rural Teachers SACCOS* shilingi milioni 40, *Mbinga Kurugenzi SACCOS* shilingi milioni 50, *Mahanje SACCOS* shilingi milioni 18 na *Pride Tanzania Ruvuma Branch* shilingi milioni 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa za shilingi milioni 500 kwa ajili ya uwezeshaji na ajira kwa kila Mkoa ziwekewe utaratibu maalum. Utaratibu maalum wa kuhakikisha kuwa walengwa wananufaika umekwishaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo zitatolewa kwa wajasiriamali kupitia mfumo wa kibenki na kwa kuzingatia makubaliano kati ya mabenki na Serikali ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo yenye masharti nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumo wa utekelezaji na mfumo wa kitaasisi, kanuni za utekelezaji na mtiririko wa fedha kati ya Serikali, taasisi za kifedha, asasi za huduma za fedha na wajasiriamali, umeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, mabenki na asasi za huduma za fedha zitakazotumika na mikopo itakayotolewa itazingatia hali halisi, mahitaji na vipaumbele kwa kila Mkoa. Mikopo italenga zaidi maeneo ya uzalishaji mali yenye kukuza ajira, kukuza uchumi na kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu, Serikali iwasaidie wafanyabishara wadogo wadogo kwa kuwapa elimu na kuwakopesha kwa kuwakopesha ili kukuza mitaji na biashara, Serikali imeandaa mradi wa biashara ndogo, za kati na kuimarisha ushindani wenye lengo la kuimarisha ushindani, upatikanaji wa mikopo na kuimarisha mazingira ya biashara ikiwa ni pamoja na kuwapatia elimu ya ujasiriamali.

Aidha, mpango wa MKURABITA utawasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo kwa kurasimisha biashara zao na hivyo kuwawezesha kukopa katika taasisi na asasi za fedha. Pia Serikali imetenga shilingi bilioni 21 kuwakopesha wafanyabiashara wadogo wadogo kwa masharti nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi lingine la wachangiaji lilichangia chini ya Ujenzi wa uwezo wa takwimu, Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ni pamoja na Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Juma Njwayo na Mheshimiwa Devota Likokola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ichapishe na kusambaza *Tanzania in figures.* Ofisi ya Takwimu ya Taifa imekuwa ikichapisha kitabu kiitwacho *Tanzania in figures.* Kwa mwaka 2005 kimesambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge siku ya Ijumaa tarehe 11 Agosti, 2006.

Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kisaidie kutoa wataalam wa kutosha ili kutafsiri mipango ya maendeleo katika ngazi mbalimbali hasa vijijini. Wizara yangu inakubaliana na hoja ya Waheshimiwa Wabunge na kwamba hii ndiyo dhamira ya Wizara. Hii imejidhihirisha katika hotuba yangu ya Bajeti ambayo imebainisha upanuzi wa miundombinu ya chuo ili kiweze kuchukua wanafunzi wengi zaidi. Azma hii itaendelea, hata hivyo sambamba na juhudi hizi nashauri Halmashauri za Wilaya,Miji, Manispaa na Vijiji kuwa na utaratibu wa makusudi wa kudhamini wanafunzi waweze kuchukua mafunzo katika Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini na Vyuo vingine vya aina hii na kuwaajiri wataalm wenye fani ya mipango.

Mheshimiwa Spika, Serikali ianzishe mpango wa wataalam wa uchumi kupelekwa Wilayani na vijijini. Mpango wa kuboresha Serikali za Mitaa yaani *Local Government Reform Programme* ambao unatekelezwa na Serikali, unashughulika pamoja na mambo mengine ujenzi wa uwezo wa wataalam mbalimbali waliopo kwenye Serikali za Mitaa na kuwaajiri wataalam wapya kwenye maeneo yenye upungufu ikiwemo fani ya Wachumi. Aidha, Serikali inaendelea kupanua na kuboresha Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kilichopo Dodoma ambacho huandaa wataalam wa mipango wanaosimamia na kuratibu mipango ya maendeleo katika ngazi ya Wilaya, Kata na Vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe na mkakati wa kuelimisha jamii juu ya MKUKUTA na malengo yake. Serikali iliandaa mkakati wa mawasiliano wa MKUKUTA sambamba na maandalizi ya MKUKUTA wenyewe. MKUKUTA huu ulizinduliwa rasmi mwezi Julai, 2005 hatua ambayo ilifuatiwa na uzinduzi wa kampeini juu ya uhamasishaji na uelimishaji wa MKUKUTA na malengo yake. Mkakati wa mawasiliano umeainisha njia mbalimbali za kuwafikishia ujumbe makundi mbalimbali ya jamii. Njia hizi ni pamoja na matumizi ya redio, televisheni, magazeti na majarida. Njia nyingine ni pamoja na mikutano, makongamano na matumizi ya vikundi vya sanaa, michezo, muziki na kadhalika.

Aidha, mkakati wa mawasiliano umeweka mpango wa kazi wa uhamasishaji na uelimishaji. Badhi ya hatua hizi ni pamoja na kutumia matukio muhimu ya Kitaifa kama vile sherehe za Nanenane, mbio za Mwenge na kadhalika. Mkakati wa mawasiliano umeweka utaratibu wa ushirikiano kati ya Serikali na wadau wengine. Wadau hawa ni pamoja na asasi zisizo za Kiserikali, Serikali za Mitaa na vyombo vya habari. Serikali inaendelea kuboresha uwezo wa uelewa wa asasi hizi kwa lengo la kupanua kampeni ya MKUKUTA. Lengo ni kuwa na timu nzuri ya waelimishaji itakayoweza kuwafikia watazamaji wengi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia baadhi ya hoja, naomba sasa nimpishe Mheshimiwa Waziri naye aweze kuja kukamilisha hoja hii. Naunga hoja hii mkono. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sisi leo kukusanyika hapa katika Mkutano huu wa Nne na kikao cha leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza bila kuonyesha kuchoka wakati nilipokuwa nawasilisha hoja yangu hapa Bungeni siku ya Ijumaa.

Aidha, naomba kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa hoja hii kwa maandishi au kwa kuzungumza hapa Bungeni lakini vile vile wakati wakichangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Adam Malima, Mbunge wa Mkuranga na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na vile vile Msemaji Mkuu wa Upinzani kuhusu Wizara hii, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, kwa michango yao hapa Bungeni. Mwenzangu, Naibu Waziri vile vile namshukuru sana kwa kunisaidia kujibu baadhi ya hoja ambazo kwa kweli amejitahidi na mimi kwa kweli namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja yangu kwanza kwa kutoa kauli hapa Bungeni walikuwa 11 na Waheshimiwa waliochangia kwa maandishi walikuwa 18 na waliochangia hoja hii wakati wakichangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu walikuwa 16. Kwa hiyo, naomba niwatambue kwa haraka haraka.

Kwanza waliochangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dr. Wilbroad P. Slaa, Mheshimiwa Mohamed Sinani, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa John Lwanji na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah. *(Makofi)*

Waheshimiwa wafuatao ndio waliochangia kwa kauli kwenye hotuba yangu ambao ni Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiw Martha Umbulla, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Peter Serukamba na mwisho wake Mheshimiwa Salome Mbatia, Naibu Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Halima Kimbau na Mheshimiwa John Lwanji. Wote hawa nawashukuru kweli kweli kwa michango yao. *(Makofi)*

Sasa mwenzangu ameanza kwa kutoa maelezo kuhusu zile hoja tulizozigawa, tulizozigawa A mpaka G na amefikia F sasa. Kwa hiyo, mimi nitaendeleza kuanzia F na mchango wa hoja hizi zinahusu Sera, Programu na mipango ya maendeleo na Waheshimiwa waliochangia ni kwanza Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza utayarishaji wa mipango maalum kwa kuharakisha maendeleo *(Tanzania Min-Tiger Plan 2020)* umetumia alama gani, kiasi gani cha gharama, je, wataalam wetu walishirikishwa katika mchakato wa maandalizi haya. Maelezo yetu ni kwamba gharama halisi ya matayarisho ilikuwa dola za Kimarekani 233,200 ambazo alipewa Mshauri Mtaalam ambaye aliandika mradi huu ambaye aliomba kuandika mpango huu ni *Japan Development Institute* ya Japan, ikiongozwa na Profesa Shoichi Kobayashi. Lakini wataalam wetu wote walishiriki ambao walishirikiana na huyu mtaalam katika kuandaa mpango huu na siyo tu wataalam hata sisi Wabunge tulishiriki kama mtakumbuka tarehe 9 Julai, 2005 tulifanya semina pale Bungeni katika Ukumbi wa zamani kuhusu mpango huu na ushauri wenu kwanza mliunga mkono mpango huu lakini pili mlituagiza kwamba tuutekeleze kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana mapema mwaka huu tukaleta Sheria hapa Bungeni na mkaipitisha Sheria ya Fedha mwezi Februari. Ile ndiyo ilikuwa utekelezaji wa huu mpango. Hoja nyingine je, mazingira haya tuliyokuwa nayo ya kisasa yanafanana na huko yalikotokea masuala haya ambayo yanaonyesha katika mpango huu? Ndiyo mazingira ya nchi yetu kwa sasa yanafanana na yale yaliyokuwepo katika nchi za Kusini Mashariki mwa Asia wakati huo. Hali hiyo ndiyo inatufanya tujifunze kwao kutoka katika hizi *Tiger Economies.* Lakini hata hivyo hatuigi, tunafuata baadhi ya mambo, mambo mengine tutafuata hali yetu halisi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi ilishirikishwa katika utekelezaji wa mpango wa *SEZ.* Jibu ndiyo, kwa kweli *SEZ* inatekelezwa na sekta binafsi, sisi Serikali tutakuwa tunaandaa tu mazingira, kama tunavyoandaa mazingira pale Mabibo Dar es Salaa kwa jina maarufu la *William Benjamin Mkapa, Special Economic Zone* vinginevyo ni sekta binafsi ndiyo inayoandaa kazi yote ya kuendeleza *SEZ.* Mipango gani imewekwa ili kuendeleza mikoa sita ya pembezoni, yaani Tabora, Lindi, Ruvuma, Rukwa, Kigoma,

Mtwara kama Mheshimiwa Rais alivyoagiza. Serikali inatekeleza mipango na programu mbalimbali ya Kitaifa kwa mikoa yote. Lakini ni kweli vile vile kwamba Rais ameagiza mikoa hii tuipendelee zaidi kwa sababu iko nyuma. Kwa hiyo, kwa mfano ndugu yangu hapa Mheshimiwa Peter Serukamba, amezungumzia utalii Kigoma. Kwanza ile ramani usiijali, ile ramani kwa kweli ni makosa. Imekuja pale kwa makosa. Kwanza siyo sahihi mpaka inaonyesha pembeni kabisa mwa Ziwa Tanganyika, siyo sahihi. Kwa hiyo, imekuja kwa makosa na mimi naomba radhi kwa kuleta hii ramani mbele yenu. Pili, Ziwa Nyasa tumepanga vizuri, Nyasa ina mpaka mzuri. Iliyokosewa ni ya Ziwa Tanganyika. Lakini kwa suala la utalii, mimi kama Waziri wa zamani wa Maliasili na Utalii tulishakubaliana, tulishaandaa *Tourism Master Plan* na Kigoma imo katika mpango ule wa *Master Plan* kwa hiyo usijali yale tuliyoyaweka pale. Wala hata ya viwanda usiyajali, yale ni mwanzo tu lakini shabaha yetu Kigoma itapata kipaumbele. Kwanza kama tulivyosema barabara ile ya kutoka Tunduma kupitia Sumbawanga, Mpanda mpaka Uvinza - Kigoma, barabara ile tutaendelea kuitilia mkazo na kuitengeneza kwa kiwango cha lami. Lakini ya pili tunakubaliana kwamba barabara nyingine ya Manyoni - Igalula - Tabora mpaka Kigoma kupitia Urambo nayo itatengenezwa kwa kiwango cha lami.

Sasa hivi tuna bidii ya kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga barabara ya kudumu katika Mto Malagarasi na Serikali ya Korea imeonyesha nia ya kutusaidia na hili tunaendelea kulichangamkia. Kwa hiyo, Kigoma tunaendelea kuifungua zaidi pamoja na kwamba kuna mpango amesema Waziri hapa wa Nishati na Madini kwamba tutajenga katika mwaka huu wa fedha msongo utakaofika Kigoma kutoka Tabora kama sehemu ya *national power grid.* Kwa hiyo, Kigoma hatuipuuzi, tunaiundia mazingira mazuri ili iweze kupiga hatua. Lakini vile vile kuna mashamba pale ya michikichi. Kwa mambo mawili. Kwanza kwa ajili ya kupata mafuta kutokana na michikichi. Lakini vile vile kwa ajili ya kama sehemu ya *by fuel production.*

Kwa hiyo, jambo hili tunalishughulikia kikamilifu. Kwa hiyo, hakuna Mkoa sasa hivi tutaupuuza. Tutakwenda Tabora vile vile tutakwenda Rukwa, kama tulivyosema kuhusu barabara na Lindi na Mtwara na Ruvuma. Yote haya yamewekwa katika mpango ya kuendelezwa na *Min Tiger Plan* itafika kote huko. Ni muhimu niliseme hili na nimkumbushe hapa Mheshimiwa Cynthia Ngoye, kwa kazi nzuri aliyoifanya pale Kilimanjaro kama Mkuu wa Mkoa pale kwamba yeye ndiye alikuwa chimbuko la kuvutia hata kile kituo. Kwa hiyo, namwona hapa Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, *RC* wa Tanga hiyo ndiyo kazi aliyofanya mwenzenu kuvutia, ndiyo yeye chimbuko. Kwa Mkoa wa Mwanza vile vile alikuwa Mheshimiwa Daniel Njoolay, ndiyo aliyevutia pale. Kwa hiyo, mimi nakuombeni Waheshimiwa Wabunge msiseme Serikali itakuja lini, semeni sisi tumeshaanza hapa, Serikali mje. Hiyo ndiyo msingi huo na mimi naomba sana kumpongeza Mheshimiwa Cynthia Ngoye kwa kazi aliyofanya na naomba vile vile nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu alipokuwa pale Mbunge tu Kilimanjaro tu alikuwa anakuja mara kwa mara kunihimiza suala hili kama Mbunge, kwamba eeh, bwana mtafanya nini kule? Wakati huo nilikuwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Kwa hiyo, hili suala Wabunge lazima tuchangamkie, tusidai lini watakuja wawekezaji. Kwa sababu sasa wawekezaji lazima tuwe na wa aina mbili, wawekezaji wa ndani, kwa maana ya ndani ya Mkoa pale ndani, kuna watu wanaweza kuwekeza pale vizuri tu. Mu-*mobilize those people* kwanza, halafu ya pili, mu-*mobilize country wide,*

halafu tatu, hawa wa Kimataifa. Lakini tukitaka kungojea wa kimataifa tu wakati pale ndani hatujengi u-*capacity* ya kuwekeza hatuwezi kufikia matarajio yetu.

Kuhusu miundombinu waliochangia ni Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Juma Njwayo. Serikali ikamilishe utaratibu wa kuipatia *TIB* mtaji wa kutosha kwa lengo la kuijengea uwezo kiutendaji. Naam, Serikali imekwishafanya maamuzi makubwa tu, kuimarisha *Tanzania Investment Bank* na yenyewe sasa ndiyo itafanya kazi zote kwa maana ya kuwa *supporter investment* katika *agriculture* na viel vile katika *industrial sector.* Kwa hiyo, hili tunafanya vizuri shabaha yetu tuwe na mtaji wa bilioni 50. Tumeanza mwaka wa jana wa fedha na shilingi bilioni 7.5. Mwaka huu tunaongeza bilioni 17.5. Kwa hiyo, tayari pale bilioni 25. Kwa hiyo, kama mtu ana mradi tayari karibu, fedha ziko ambazo ziko pale zinasubiri.

Serikali isaidie mikoa ya mipakani, pembezoni ili ipate maendeleo endelevu na ya haraka. Hili nadhani nimekwisha lijibu. Hakuna haja ya kujibu tena. Nafikiri tumelitolea maelezo mazuri. Uchumi ulio na sekta kubwa ya kilimo bila sekta kubwa ya biashara unahitaji, Serikali kuingia kati yaani *state intervension.* Hili nalo tunalifanya na tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge katika hoja hii na ndiyo maana Serikali imetoa MKUKUTA. Kwanza tumetoa dira, pili sasa tumetoa MKUKUTA na halafu tunakuja na mpango wa *Tanzania Min Tiger Plan* kwa shabaha ya kujenga uwezo ili sekta hizi ziongezeke kukua kwa haraka zaidi. Vile vile tuna mkakati kukuza sekta binafsi ndani ya nchi ili iweze kuwa injini ya ukuaji wa uchumi wa Taifa letu kama Sera ya sasa ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kuna nyongeza kidogo hapa ya uwekezaji ambayo ameitoa ndugu yangu Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Kinondoni kwamba *Finance Bill* inapingana na Sheria ya uwekezaji hususan suala la *feasical stability* ambapo iwapo Serikali itatakiwa kuwafikiria wawekezaji waliopo nchini wakati wa mabadiliko ya Sheria ya Fedha na kama mabadiliko hayo yataathiri vivutio vilivyokuwepo wakati wa kuwekeza. Suala hili linahusu *feasical stability* ambalo ni kweli ni lazima tuliangalie kwa makini tunakubaliana na wewe kabisa. Tunawasiliana na Wizara ya Fedha kuhusu hiki kifungu 19 (ii) cha Sheria ya Uwekezaji kiainishwe na Sheria ya fedha ili tukiri kuleta *stability* maana tusipofanyahivyo kwa kweli kama ulivyotushauri inaweza ikaleta matatizo katika msingi wa kuvutia wawekezaji. Hoja ya Mheshimiwa Halima Kimbau, kwa niaba ya akinamama wa Mkoa wa Pwani, tunashukuru sana kwamba mradi wa *SELF* umefika. Tumenufaika kwa kiasi fulani na mradi huu. Lakini bado yapo matatizo makubwa kwani wanawake bado walioko vijijini hawajafikiwa. Hili tunalikubali, uwezo wetu bado siyo mkubwa sana. Lakini vile vile kuna ukweli vile vile usalama wa fedha za mradi ni muhimu na ili kwamba tutambue umuhimu wa fedha ni za mkopo lazima tuzirudishe, ili wenzetu wengine wakope. Hatuna rasilimali ya kutosha kwa watu wote kukopeshwa kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, wale wanaoanza kukopeshwa basi lazima na wenyewe warudishe mikopo hiyo na ndiyo maana tunatilia mkazo mikopo hii kwenda *SACCOS,* kutumia *SACCOS* zaidi na kwa hiyo, nakuombeni natoa wito mfanye bidii kwamba muunde *SACCOS* itakayopata mikopo hiyo.

Kuhusu Wilaya ya Mafia ambayo ameizungumzia sana Mheshimiwa Halima Kimbau na Mheshimiwa Abdulkarim Shah, kwanza nataka nikubali kwamba mimi nitakuja mwenyewe. Nitakuja Mafia na nilishakwenda kule zamani nilipokuwa Maliasili pale. Sasa hivi nitakwenda tena. Kwa kweli hoja zile za msingi alizosema Mheshimiwa Abdulkarim Shah, gati, kiwanja cha ndege ni muhimu kwa mahali kama kisiwa kile. Kwa maana mbili, kwanza kwa usafiri wa wananchi lakini pili, kwa kuendeleza utalii maana Mafia ni kisiwa maarufu kwa utalii pia. Kwa hiyo, mimi nitakwenda kuona na nitashirikiana nanyi kuandaa mipango ambayo inasthaili kuandaliwa. Lakini pamoja na kwamba mnataka kuja ofisini kwangu, ruksa vile vile. Maana Ofisi ile ni yenu. Msiogope njooni kabisa.

Mheshimiaw Spika, F, nyongeza hizi maana wameleta asubuhi. Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Abdulkarim Shah, haya maelezo mengine nimeshayatoa, lakini nataka kusisitiza kama nilivyosema pale mwanzo kwamba maeneo ambayo hatukujiandaa sisi wenyewe kama wananchi hatuwezi kupata wawekezaji kwa haraka. Lazima tujiandae sisi wenyewe. Kwa hiyo, mimi naomba kote kule Ruvuma, Ludewa, Mbinga tujiandae na Serikali itakuwa tayari kufika huko mara uwezo wa kifedha utakapokuwa umepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi amehoji vigezo gani vilivyotumika katika kuchagua kijiji cha Mbola, kule Tabora. Kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ni kwamba kijiji kile cha Mbola kilichoko Mkoa wa Tabora kimechaguliwa kwa kuzingatia kuwa ni mfano wa mahali ambapo juhudi hizi zote za kuondoa umaskini zinaweza zikafanikiwa. Kwanza hali ya hewa yake, hali ya kilimo chake, lakini zaidi nadhani ni hali ya umaskini wa kijiji kile maana mimi nimefika pale. Unaweza kuuona umaskini uliopo pale. Kwa hiyo, *what we are trying to do* tunajaribu kufanya pale ni kuleta yote yale, kwa mfano kushughulikia suala la afya. Chandarua kwa mfano, watapewa bure, chandarua chenye dawa wote katika kijiji kile walale ndani ya chandarua ili kukabili tatizo la malaria.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kutakuwa na zahanati pale itajengwa kwa ajili ya kushughulikia masuala ya matibabu. Kutakuwa na shule ya msingi itajengwa, ama itapanuliwa iko lakini itapanuliwa na kuwajengea walimu nyumba za kuishi maana tatizo letu hapa kubwa ni kwamba tunajenga madarasa, hatujengi nyumba za walimu na sehemu nyingine hata vyoo hatuvijengi. Sasa watoto watakwenda wapi, kwa hiyo, hapo tutafanya yote kwa pamoja na *project* hii inafadhiliwa na *UN*. Hoja yake ni nini? Hoja yake ni kuthibitisha kwamba kama ukifanya vitu vyote hivi pamoja utaweza kufikia shabaha zako za kuondoa umaskini. Ndiyo maana yake.Pale hata kilimo kitakwenda pale na watapewa mbolea, watapewa dawa, watasaidiwa trekta na kadhalika. Kwa hiyo, ili ku-*combine* kwamba kazi hizi zote zikifanyika kwa pamoja basi unaweza kufikia lengo hili na hoja si kwamba ni pale tu hata kwangu kule Morogoro viko vijiji vya namna hiyo. Hoja ni wapi tuanze.

Kwa hiyo, tumeanza pale mimi naomba tushukuru sana kwamba wametusaidia wale wenzetu kutuwezesha kufikia lengo hili. Sasa labda nitoe maelezo kidogo kuhusu

hoja aliyozungumza Mheshimiwa Peter Serukamba pale ya *planning* na *geographic location* ya Tabora kama ni msingi mzuri wa uchumi wa kijiografia. Nakuunga mkono katika hili *a hundred percent* na sisi kama Serikali na sisi kama nilivyosema kwamba tutaboresha miundombinu, miundombinu nimeishaitaja. Lakini vile vile *SEZ* iko, itakuwepo pia Kigoma. *EPZ* vie vile katika mambo haya mawili, ama moja itakuwa *SEZ* ama *EPZ* kwa nini, kwa sababu ya kukamata uchumi wa jiografia ambao Kigoma ni tajiri kwa maana kwanza inapakana na nchi jirani ya *DRC,* ya Rwanda ya Burundi. Kwa hiyo, hili tulisimamie vizuri lakini tatizo *of course* tuboreshe miundombinu hii la sivyo huwezi kumpeleka mwenye kiwanda pale kabla hujamboreshea miundombinu na ni matumaini yangu kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano kazi kubwa kwa ajili ya Mkoa wa Kigoma ni kuboresha miundombinu ile yote niliyoitaja ili iweke mazingira mazuri ya uwekezaji katika mkoa wa Kigoma. Sasa muda hautatosha kwa hiyo, tutarukaruka kidogo katika kutoa maelezo. L akini tumekubaliana pale ofisini kwamba tutakupeni hii karatasi, tumeshaliandaa karibu na kumaliza tutakupeni. Ili majibu yote yatakuwemo humu ambayo kwa majina tena na michango yenu. Kwa hiyo, msisononeke kwamba Ngasongwa huyu katuruka kutujibu. Lakini muda hautoshi.

Sasa nilijibu moja hili ambalo alilileta katika hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kwamba kwa nini *Tiger Economies* kwa nini ninyi mmechagua *Tiger economies.* Neno *Tiger Economies* ni jina maalum linalotumika kuelezea uchumi katika nchi za Asia ya Mashariki na Afrika ya Kusini. Kwa nini? Kwa sababu *tiger* ni mnyama ambaye ana sifa mbili kubwa. Moja ana nguvu sana, lakini pili ana kasi. Sasa mfano, kule Uingereza mapinduzi ya viwanda ilichukua miaka 100 kukamilika. Marekani ilichukua miaka 70 mpaka 100. Sasa ona katika *Tiger Economies* ni wastani wa miaka 30 mpaka 40. Waka-*transform economy* zile ndiyo tunazoziona sasa. Wale wenzetu wale kwa mfano *South Korea,* Thailand, Malaysia, India, China 30 - 40 *ago* walikuwa kama sisi. Lakini wamezi-*transform* kwa *concept* hii ya *tiger economies* ambayo mkazo wake ni nini ni *export promotion* na ndiyo tunayoifanya sisi hapa *export promotion.* Kwa hiyo, mafunzo haya ni mazuri kwa sisi Tanzania na tumeshauriwa na wataalam wengi tu kwamba tukitumia *model* hii ya uchumi tunaweza kufikia kama hawa wenzetu kwa muda mfupi wa miaka 20-25 inayokuja. Ndiyo maana *Tanzania Min Tiger Plan 2020* ingawa dira inazungumza 2025. Unaona tofauti yake. Tunafikiri tunaweza tuka-*shorten* kidogo kwa miaka mitano. Sasa hii inahitaji nidhamu kwa sisi wote kufanya kazi kwa bidii sana.

Mheshimiwa Spika, hii *concept* ya *tiger economy* si ya Asia hata kule Ulaya, kule Ulaya wanaita *sale tic tiger economy* huyu mnyama bado anaunganishwa hata kule, kwa ajili ya kuleta maendeleo na nchi, hizi zipo, Ireland kwa mfano, Island, Denmark zimepiga hatua haraka haraka, Finland nchi ambazo zimepiga hatua haraka haraka katika muda mfupi, *the least is endless,* kwa hiyo naomba niishie hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Serikali iangalie namna ya kukopa wahisani, benki ya dunia na wengineo ili kuongeza nguvu katika maendeleo ya nchi, sawa kabisa, sisi katika Serikali tumeunda kitu kinachoitwa Mkakati wa Taifa wa Madeni, ambao ulianza mwaka 1999 na mkakati huu ndio unatuwezesha sisi kukopa na ndio maana *IMF* na *World Bank* na Benki ya Maendeleo ya Afrika, ndio wanaotusaidia ama kutufutia

madeni, ama kutuongeza mikopo zaidi. Kwa hiyo, tunataka tuwe na nidhamu ya kukopa, kutokana na mkakati huu wa madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Adam Malima, Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Fedha na Uchumi, baadhi ya mashirika yameuzwa kwa haraka haraka na kwa bei ya chini kuliko thamani halisi. Hapana, mashirika mengi yaliuzwa kutokana na kuwa na hali mbaya kiutendaji, ndio ukweli wenyewe, sasa ukiyapeleka yale kwenye soko, soko ndio inakupa bei hiyo, unaweza kupenda zaidi, lakini hali zake mbaya, huwezi kupata bei nzuri. Ndio maana hakuna mtu aliyekuwa anafanya kusudi, tena Mwenyekiti wenu wa Kamati hii ndio aliyekuwa anatekeleza wakati huo, anajua kabisa kwamba aliuza si kwa sababu bei poa, hapana aliuza kwa sababu soko ndivyo lilivyoweza kuruhusu, kwa hiyo, hili naomba tuelewane hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Mohamed Missanga na Mheshimiwa Eustace Katagira, wote wanazungumzia suala hili la ubinafsishaji wa *TRC,* tuwe waangalifu ili makosa yaliyojitokeza awali yasirudiwe, ubinafsishaji wa *TRC* uwe wa makini kuepuka yaliyotokea kwenye mashirika mengine. Hoja nyingine katika ubinafsishaji wananchi wapewe upendeleo maalum kwa vile ndio wenye uchungu wa maendeleo ya nchi yao, yote haya tunayaafiki na yote haya tumeyafanya. Kwa mfano haya mazungumzo tunayofanya na *Light Sub India,* bado majadiliano yanaendelea, kama alivyosema Naibu Waziri, lakini tuko *very clear* kuhakikisha maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namna moja ya maslahi ya Taifa kwanza ni kuhakikisha kwamba ile reli inaanza kutumika kuanzia Dar es Salaam na hiyo tumekubaliana nao, tutaacha kuanzia Dodoma, tutaanza tangu Dar es Salaam. Lakini la pili tutakarabati njia, ile njia itakarabatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, tutahakikisha itakuwa na uwezo zaidi, sasa hivi hapa ina uwezo wa *latrine 80,* tunataka tufike mpaka *latrine 115* na 120. Kwa hiyo, maslahi ya Taifa tunayasimamia tunayazingatia, mtupe fursa tufanye kazi hii vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa William Shellukindo, amezungumzia pia suala la mchakato wa kubinafsisha *NIC,* nalo lenyewe tunalifanya kwa uzuri, ushauri tumeupokea lakini tutazingatia, ushauri huu tutafanya kwa uzuri bila kupoteza maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Kuhusu ubia, Serikali inazingatia na itaendelea kuzingatia ushauri huu, katika mashirika 322 yaliyobinafsishwa, mashirika 178 walipewa Watanzania kwa asilimia 100, kwa asilimia 100 walipewa Watanzania na mashirika 28 tu ndio yaliyobinafsishwa kwa asilimia 100 kwa wageni. Kwa hiyo, sio kweli kusema kwamba tulipeleka mali hizi kwa wageni zote hamna, mashirika 28 tu ndio yalikwenda kwa wageni kwa asilimia 100 na mashirika haya yaliyobaki 116 kuna ubia, Watanzania na wageni, kwa hiyo, hili tunalizingatia na mimi naomba tukubaliane kwamba hatufanyi mambo bila kuzingatia maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Kuhusu kampuni ya *Light*, itawekeza kwa kiasi gani na katika maeneo yapi? Sasa hili siwezi kulijibu sasa, lakini nimekudokezeeni mambo ambayo tunayatilia mkazo kwa

ajili ya maslahi ya Taifa. Kwa sababu majadiliano bado yanaendelea, kwa hiyo, tutakapokamilisha majadiliano, basi tutaweza kulieleza Bunge hili mambo gani tumeafikiana na kampuni hii ya *Lights of India.* Labda niongezee tu hapa kwamba kampuni hii ya *Lights of India,* ni kampuni yenye uzoefu mkubwa, ina kodisha, inaendesha reli kwa kukodisha, sio kwetu tu, Msumbiji hapa wanafanya hao hao na mambo yao ya Msumbiji kwa *rate* sasa yanakwenda vizuri, wanafanya hao hao wako pia *Light America* kule hawa *Lights of India,* kwa hiyo, msipate hofu, sisi tumewachagua hawa makini na tutaendelea kusimamia ili malengo yetu kama tulivyowapangia.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, amesema anazungumzia ubinafsishaji wa *TAZARA,* anasema jamani, mhakikishe kwamba Serikali ya Kichina inashirikishwa, naam, ndio tulivyo na tunavyofanya, Wachina tumezungumza nao na tunakubaliana nao na kampuni moja ya Kichina, maana ni *private sector* hii, sio tena Serikali ya Kichina hapana, *private sector* kampuni ya Kichina itakuja kushirikana nasi katika kukodisha *TAZARA* na kuiendesha kwa ufanisi zaidi. Kwa hiyo, hili ndugu yangu usipate hofu.

Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mbunge wa Hanang, amezungumzia mashamba mawili ya Gawal na Warret, kwanza nataka kumuahidi kwamba mimi pia nitafika kule, nikaone mwenyewe mashamba yale yako namna gani na nitakwenda na wataalam na ili tuweze kujua nini tukifanye pale, tufanye kama anavyotushauri yeye kwamba zile mali tuziuze, mashamba tuwaachie wananchi au namna nyingine yoyote ile, lakini *Inshallah* tutafika na mimi nitapenda kwenda na Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kule kwenda jimboni kwake, kwa sababu najua na yeye anatoka Morogoro pia. Kwa hiyo, atakwenda na pangu Ulanga Magharibi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Benson Mpesya, Serikali iipatie Manispaa ya Mbeya, ekari 1600 kwenye eneo la shamba la Iwambi ili litumike kwa ajili ya ujenzi wa viwanda. Hili tutalitazama vile vile, hatuwezi kuamua hapa lakini tutakwenda tutaona hali halisi kwa sababu ujenzi wa viwanda ni jambo jema, kwanza sisi Serikali tunajenga kiwanja kikubwa pale cha Songwe na moja ya sababu ya kujenga kiwanja kile ni kama muundombinu mzuri wa kuvutia wawekezaji na wawekezaji hao ni katika viwanda, katika maua pengine, katika viazi vile mviringo, yote haya tunayazingatia. Kwa hiyo, hili jambo jema tutakwenda kuliangalia vizuri tuone tutaamuaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Estherina Kilasi, Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia mashamba wakulima wadogo wadogo wanaolima kando kando ya mashamba ya *NAFCO* kule Mbarali, ili wasiendelee kuharibu mazingira na vyanzo vya maji na badala ya kubinafsisha mashamba hayo, kwa watu wachache. Sasa hili nataka niliweke vizuri na Mheshimiwa Estherina Kilasi, anajua mimi nilishaliweka vizuri hili, nataka kuweka vizuri hapa kwa kusema kwamba kwanza mashamba yale makubwa, lazima yaende kwa wawekezaji wakubwa, maana ndio sera yetu sera yetu ya chama chetu katika Ilani ya CCM bahati nzuri na mimi nilikuwa mjumbe mle, Mwenyekiti wetu alikuwa Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru, hapa, tuna sera mbili pale, tuna sera ya mashamba makubwa na sera ya mashamba madogo ya wakulima. Kwa hiyo, yale makubwa yatakwenda kwa wakulima wakubwa, ili tupate ile *benefit* ya kutumia mashamba makubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini mashamba madogo tutawapa wakulima wadogo wadogo na hawa tumewawekea, kwa mfano Gwilo. Gwilo pale kuna shamba tutali-*develop* pale, tumetenga pale mwaka huu wa fedha shilingi milioni 750 na hekta 400, tunawatengea hii kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo. Kule Uturo, tumewatengea shilingi 1.6 bilioni kwa mwaka huu wa fedha, ili tutengeneze hektar 1000 kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo. Kimani na Mbuyuni, tumetenga kwa mwaka huu wa fedha shilingi milioni 700 kwa ajili ya kutengeneza hekta 500 kwa ajili ya wakulima wadogo na la mwisho ni Lwanyo kule, Lwanyo majina haya ya Kisangu yana matata kidogo, lakini nadhani mnanielewa Lwanyo kule shilingi bilioni 1.6 nazo kwa hekta 500 na pale tutaandaa bwawa, tutajenga bwawa ambalo ndilo litakuwa msingi wa umwagiliaji pale na tunazingatia yote, tutazingatia in *environmental impact assessment* ili kujua hatuleti vurumai, lakini vilevile tunahakikisha kwamba maji lazima baadaye yafike kwenye Mto Ruaha, ili yaje Mtera, maana tunayahitaji maji yale kule Mtera kwa ajiri ya ku-*generate* umeme. Kwa hiyo, hili lote tutalifanya na mimi nina hakika tutafanya vizuri, lakini vile vile nimemuahidi Mheshimiwa Estherina Kilasi, kwamba nitakwenda pia, nitakwenda kuona kule. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Utakwenda naye pia?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Ndio itakuwa vizuri zaidi, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kuna ndugu yangu mwingine hapa kauliza swali zuri sana Mheshimiwa Godfrey Zambi, alikuwa tu akichangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa wote walikuwa wanachangia hotuba ya Waziri Mkuu na naijibu kwa sababu najua ukimchangia kwa bosi pale lazima ujibu, usipojibu kwa bosi tena unapata matatizo, kwa hiyo, ndio maana najibu, hawa wote walichangia kwa bosi, najibu kwamba sera ya Serikali ni kuendeleza kilimo, ni pamoja na kuendeleza mashamba makubwa na vile vile mashamba madogo. Sasa mashamba madogo, watu wa Mbozi hawa tulishawapa matatu walishachukua, hasa kwa ajili ya kahawa na wamevamia mengine matano, sasa pale Mbozi, *let me be frank*, pale Mbozi hakuna uhaba wa ardhi, habari nilizokuwa nazo mimi ya kwamba wanatumia *arable land,* wanatumia asilimia 66 tu na *arable land* iliyobakia asilimia 34 bado iko, kwa hiyo, hakuna *shortage of land* hivyo wavamie mashamba ya Serikali. Kwa hiyo, naomba na nataka lieleweke kwamba lazima sera hizi zote tuzitekeleze kwa pamoja sambamba au *simultaneously,* kwa hiyo, hili tuliweke vizuri.

Mheshimiwa Adam Malima, anasema mamlaka za *SEZ* mbona hazijaanzishwa, hapana, tumeshaanza kuzianzisha, kwa mfano ile ya *EPZ,* imeshaziduliwa na meneja mkuu wake kesha teuliwa, ya kwetu tunafanya *process* tumefikia mbali, tutapata *CO* halafu mambo yatakwenda, lakini utekelezaji wake hausimami, tunaendelea kutekeleza maana yake kwa sababu ndani ya Wizara tuna wataalam ambao wanasimamia utekelezaji wa jambo hili kwa wakati wote. Kwa hiyo, usipate hofu sana hatutatekeleza kama tunavyotarajia kutekeleza.

Mheshimiwa Devota Likokola, mkoa wa Ruvuma wapatiwe wawekezaji, tumelijibu hili, nimelijibu kwa ujumla na kutoa mfano wa Kilimanjaro na Mwanza. Kwa hiyo, ukienda kule na Mheshimiwa Monica Mbega, yuko hapa, namwomba afanye kama alivyofanya mwenzake Mheshimwa Hilda Ngoye, tena wako jirani, kwa hiyo, mzungumze pale na wote ni akinamama, akinamama ambao mimi nawaheshimu sana, *very dynamic* kwa hiyo, naomba mkae pamoja muelewane namna ya kuvutia wawekezaji. Mheshimiwa Andrew Chenge, kasema wakishindwa basi yeye atawasaidia na mimi namuunga mkono katika jambo hili atawasaidia vizuri. Kwa hiyo, hili tumeliweka vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mohamed Sinani, kutoka Mtwara, anasema Serikali iwashawishi wawekezaji wawekeze katika mkoa wa Mtwara, kwanza Wizara yangu kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania yaani *Tanzania Investment Centre,* kwa kushirikiana na uongozi wa mkoa wa Mtwara wamefanya warsha, tena hii ilifanywa chini ya wakati huo mkuu wa mkoa Mheshimiwa Isdory Shirima, tulifanya na mimi nilikwenda pale katika sherehe, wakati huo nilikuwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Kwa hiyo, sasa tutaendelea nalo na mimi naomba sasa mjizatiti mfanye nyingine ya pili, msichoke katika suala la kuvutia wawekezaji hapana kuchoka, *it's a continuous job,* kwa hiyo, mkifanya tena, tena wakati huo bosi wa *TIC* alikuwa Mheshimiwa Spika hapa, Spika wetu ndiye aliyekuwa bosi, kafanya kazi nzuri sana. Moja ya kazi yake nzuri aliyofanya ni pale *TIC* ametuachia kazi nzuri sana, tunakupongeza sana Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuendelee.

Lakini la pili kwa Mtwara, tuna *Mtwara Development Corridor* ambayo ina *ankra projects. Ankra projects* ya kwanza ni barabara, kutoka Mtwara mpaka *Mbamba Bay.* La pili reli, kutoka Mtwara - *Mbamba Bay* mpaka Manda kule kwa Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi. Lakini tatu, *ankra project* zingine ni zile za Mchuchuma na Liganga, zote hizi tunazisimamia, tunazishughulikia. Kwa mfano ya barabara tumepiga hatua sana, kwa sababu tumefikia sasa *design level* kwa hiyo, tunapiga hatua, kwa hiyo, mimi naomba watu wa Mtwara tena msilalamike tena tunafanya mambo mazuri tu na mimi barabara ile nitatembelea vile vile kutoka Dar es Salaam - Mtwara, mpaka *Mbamba Bay* nataka nifike na mimi nione matatizo yako wapi kama mpangaji wenu maana mimi ndio *chief planner* wenu, kwa hiyo, lazima nitafika huko na tutaona mambo yanakwendaje. Kwa hiyo, *Mtwara Corridor* ni kitu muhimu, daraja lile la kuunganisha Tanzania na Msumbiji limeanza kujengwa, mambo yanakwenda vizuri. Lakini vile vile mradi wa kuchimba gesi nao unapiga hatua nzuri sana, Waziri wa Nishati na Madini sasa ametueleza vizuri *progress* tulikuwa nayo pale, kwa hiyo tunakwenda na mimi nitakwenda kuiona na leo nakutana nao pia *ATOMAS* saa tisa kasoro robo, wameniomba nionane nao, kwa hiyo naendelea kuonana nao, naendelea kupiga debe, kwa ajili ya maendeleo ya Mtwara. Lakini kituo tutafungua mwaka huu, najua Mheshimiwa Mohammed Abdulaziz, pale angetaka kiende Lindi, lakini sasa tumeshafanya uamuzi kiende Mtwara, kwa hiyo, tutaenda Mtwara. Lakini tutakuwa na cha mkoa kwa ajili ya Lindi, tutatafuta huo uwezekano kwa hiyo, usivunjike moyo na wewe ndugu yangu tunaelewana siku nyingi, kwa hiyo, hatuwezi kufanya mambo bila kuyafanya vizuri. Lakini kuna wapitaji wengine kwa Mtwara, kuna jamaa wa *OJI Paper* na *Maruben* wanataka kutoka Japan, wataka kuanza maandalizi, wameshaanza maandalizi ya mradi wa upandaji wa miti kwa ajili ya kutoa *wood chip* kwa hiyo, ninyi watu wa Mtwara,

mradi unakuja na huu sio wa Mtwara tu ni pamoja na Lindi vile vile, kwa hiyo, kazi inakwenda vizuri, lakini vile vile kuna kampuni ya *IC Net Limited* ya Japan, inafanya utafiti kwa ajili ya kukuza uzalishaji wa ufuta, zao la ufuta, watakwenda Mtwara na Lindi lakini vile vile watafika nchi mzima. Kwa hiyo, sasa hii ni taarifa nzuri kwa Wabunge kujihamasisha wenyewe ili tufikie mahali pa kukaribisha wawekezaji ili waje wawekeze katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima niruke kidogo kwa sababu makaratasi haya ni mengi na siwezi kufanya yote isipokuwa baadhi tu nitajibu jibu hapa na baadaye nitawapa karatasi ili mjisomee mambo tuliyoyafanya. Hili la Mheshimiwa Devota Likokola la *SELF* kesha lijibu mwenzangu ndio sababu sikulirudia, lakini nataka kumjibu ndugu yangu Mheshimiwa Job Ndugai wa Kongwa, ambalo alilitoa wakati wa Waziri Mkuu pale kwamba lengo la fedha za uwezeshaji ziwe watu wa hali ya chini ambao hawakidhi masharti na mikopo ya benki. Jibu letu ni kwamba fedha za uwezeshaji zimelenga kuwafikia wajasiriamali wa mijini na vijijini, wote watapata, hasa wenye kipato cha chini, utaratibu wa kuwatambua na kuwafikia kuanzia ngazi ya Taifa hadi Kata na vijiji unaandaliwa na huu kesho nadhani leo, leo mtaelezwa kwa undani kabisa suala hili. Kwa hiyo, mvute subira kidogo mtaelezwa kwa undani zaidi, ndugu yangu pale Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, ndio atalielezea vizuri hili na mimi nitakuwepo vile vile kwa sababu tunafanya kazi yetu kwa pamoja. Fedha zilizotengwa za shilingi milioni 500 kwa ajili ya uwezeshaji, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, anasema ziwekewe utaratibu maalum, hili nalo nimelijibu kwamba sitaki kulisoma hapa sasa hivi tutalitoalea maelezo mazuri wakati huo wa saa saba na nusu leo, kwa hiyo tutaelewana tu bila matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Castor Ligalama, bado *SELF* haijajitangaza vya kutosha ili kujulikana na wananchi, *SELF* imekuwa ikijitangaza kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kipindi cha redio kijulikanacho kama Kopa Ujiendeleze kinachorushwa hewani kwa kupitia Redio Tanzania, Dar es Salaa, *Radio Free Africa* na Sauti ya Tanzania Zanzibar. Kwa hiyo, mimi hapa nimewahi kusikia mara nyingi tu, kwa hiyo, mimi nakuombeni Waheshimiwa Wabunge msikilize vipindi hivi, mtapata matangazo ya hawa jamaa wanajitangaza vizuri sana. Lakini vile vile tumetoa makaratasi hapa kama alivyosema jana Mheshimiwa Paul Kimiti, kwamba tumetoa makabrasha mengi, naomba myasome.

Mimi nilisikitika juzi juzi hapa nilipopita kwenye *pigeon holes* nikatakuta mengine yametupwa, la MKUKUTA limetupwa, hata vile vielelezo vile vya *popular vision* kwa ajili ya MKUKUTA, navyo vimetupwa, sasa nikashangaa, sisi tumetumia pesa nyingi tunawagawia Waheshimiwa Wabunge msome na mpeleke nyumbani, sasa mkitupa pale, mnanivunja moyo kwa kweli, kwa sababu sasa tutajuaje? Nakuombeni msiyatupe, myachukue myasome halafu myapeleke kwenye majimbo yenu. Haya ndio maswali haya mnaniuliza haya hamtaniuliza tena maana yake nimeandika, nimeandika yote haya nimekupeni na hali ya hewa ya uchumi ya mwaka 2005, taabu kubwa kabisa msome ili muelewe, nimekupeni vipeperushi vyote hivi kwa lengo ili mfahamu, sasa mkifahamu ndio mtaeleza vizuri.

Mheshimiwa Job Ndugai, tena, Programu ya Taifa kuongeza kipato *(NIGP),* sio Programu ya Kitaifa, kwani ipo kwenye mikoa michache tu, kwa mfano, mwaka 2006/2007 *NIGP* imepanga kukamilisha miradi minne inayolenga katika kuongeza kipato katika mikoa ya Dodoma, Pwani, Dar es Salaam na Pemba. Malengo ya awali ya *NIGP* yalikuwa kutekeleza miradi nchi nzima, hata hivyo malengo haya hayajafikiwa kutokana na kutokupatikana kwa fedha za kutosha kutoka kwa wahisani na Serikali. Aidha, *NIGP* inatekeleza jumla ya miradi 26 iliyo katika sekta ya kilimo, miundombinu, biashara ndogo ndogo katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Mwanza, Dodoma, Manyara na baadhi ya mikoa ya Zanzibar, kwa hiyo, haiko katika mikoa ile mikoa minne tu imeenea sehemu kubwa ya nchi, lakini mpango wetu ni kwamba iendelee nchi nzima, hii mipango tuliyotaja minne, ni kwa sababu ndio tunaikamilisha ilikuwa haijakamilisha katika mwaka fedha uliopita, tunaikamilisha katika mwaka huu wa fedha huu wa sasa na kupanga kwa kweli ni kuchagua, kwa hiyo, hatuwezi kwenda nchi nzima kwa wakati mmoja, lazima sehemu fulani tuchague, tufike kwanza halafu tutafuatia sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu MKUKUTA na MKURABITA na mengine yanayozungumzwa na Wizara hayajawafikia wananchi wa Rukwa na jimbo la Kalambo, hili limezungumzwa na Wabunge wawili, Waheshimiwa watatu, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Castor Ligalama na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila. Sasa jibu langu ni kwamba MKUKUTA na MKURABITA unalenga watu wote kwa kweli, juhudi mbalimbali zinaendelea kutekelezwa na nyingine mpya kubuniwa ili kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya watu wetu. Programu yaani miradi zinazoendelezwa katika kutekeleza ni *TASAF, SELF, MMEM, MMES* na miradi ya kilimo ile mikubwa mikubwa ile miwili ya *ASDP, District Agricultural Development Plants (DADPs),* hii yote shabaha yake ni kuondoa umaskini, sasa *literature* tumeitoa, mimi nimeitoa mwenzangu kaitoa wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nakuombeni msome mle, mkisoma mle mtajua kila Mbunge katika eneo lake atatakiwa kufanya nini. Kama una matatizo ya kutokuelewa ama ya uhakika, tuulize sisi Mawaziri, mimi niko tayari kujibu masuala yoyote yale hapa Bungeni, hata tukiwa Dar es Salaam na hata tukiwa huko vijijini huko tutaelezana. Kwa hiyo, suala hili limeelezwa vizuri na mimi naomba tusilipuuze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Paul Kimiti, anaulizia wakati akichangia hotuba ya Waziri Mkuu aliulizia suala la sera ya wazee na idadi ya watu, sasa hii ya wazee hii, nadhani inamhusu mwenzangu Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, lakini hili la idadi ya watu naweza kutoa maelezo, kwamba kwanza sera ile tumeshaikamilisha na nilishawaambia siku ya Ijumaa wanachama wa chama kile cha idadi ya watu, nilishawaeleza kwamba sera imekamilika, tunangoja tu maamuzi tu ya Baraza la Mawaziri ili itoke na kwamba kulikuwa na hoja ya kuunda *Tanzania Council on Population and Development,* hilo nalo limo katika sehemu ya sera kwa hili nalo linafikiriwa Mheshimiwa Paul Kimiti kama Mwenyekiti wa Chama kile usipate wasiwasi tunalishughulikia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona nakaribia mwisho muda wa wangu, lakini kama nilivyosema pale mwanzo, nimejitahidi kujibu hoja hizi zilikuwa zaidi ya 100, kwa hiyo, haiwezekani katika muda huu tuliopewa tuyajibu yote. Lakini naomba niseme kwamba

kama walivyokuwa wanasema wenzangu, kwamba karatasi sijui tayari imekamilika ya majibu tutawagawia Waheshimiwa Wabunge, wote, ili kila mtu atapata jibu lake kwa maandishi na kwa uhakika. Lakini naomba sasa niwashukuru kwa mara ya mwisho kwa kunisikiliza na nakuombeni muunge mkono hoja yangu hii ili tupate pesa tukaanze kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Hoja iliyoko mbele yetu imetolewa na Waziri na imeungwa mkono, lakini ili kuiamua kwa mujibu wa Kanuni zetu inabidi tuingie katika Kamati ya Matumizi, kwa hatua hii basi nitawahoji.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

**Fungu 66 – Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... 13,220,805,500/=

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote* 66 programu ya 10, *subvote 1001* mshahara wa Waziri wa kile kifungu kidogo 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kuhoji au kupata ufafanuzi kidogo tu kwamba mwaka 2004, tumepitisha Sheria ya Mazingira, tumepitisha wenyewe ambayo inatutaka pamoja na mambo mengine sera, mikakati, pamoja na *plans* kabla hazijapitishwa, ziwe zimefanyiwa tathmini ya athari ya mazingira ya kimkakati kwa mfano *strategic environmental assessment.*

Sasa nilidhani katika mipango yetu na mikakati tunayoitoa tungeanza kwa makusudi kabisa ku-*subject plans* na mikakati yetu na kuonyesha mfano kwamba tunatekeleza sheria ile ya mwaka 2004, lakini naona katika mikakati yote ile *Min Tiger Plan* hizi *sense* zote hizi sioni dalili kana kwamba tunafanya *strategic environmental impact assessment* hata kwenye ubinafsishaji, kiutaratibu kunatakiwa tu-*subject* kwenye *strategic* ya *environmental assessment* ili tujue kama kutakuwa na matatizo ni yapi hayo yatatuliwe vipi, kama kuna *positive impact* basi tuone tutazifanya ziboreshwe vizuri zaidi kwa kufanya mambo gani?

Lakini sioni utaratibu huu wa kufanya tathmini ya mazingira kwenye mikakati kama inafanywa. Nataka nipate ufafanuzi labda mimi sijapata *documents* za namna hiyo pengine inafanywa ila mimi sijui, lakini nataka tu nithibitishiwe na Mheshimiwa Waziri kwamba, Sheria hii inalindwa na inafuatwa. Ahsante sana.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kuhusu hoja ya Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, kama ifuatavyo:-

Kwanza, namtambua Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi kama *Geographer* na mtaalam sana wa mambo ya *Environment*, nadhani kinachotakiwa kufanyika ni kwamba, nafikiri hatubishani bali tunaafiki suala la kufanyia *impact assessment* ya jambo lolote tunalotaka kulitekeleza. Lakini unafanya baada ya kupata ule mpango sasa, unataka uanze kutekelezwa, ndiyo unakwenda kuufanya, huwezi kufanya kabla hata ya ku-*draw the planning itself, it is not possible.*

Kwa hiyo, nadhani tunaelewana sisi, tunakubaliana na ushauri huo, lakini kwa mfano tutakapoanza kuchimba makaa ya mawe pale Mchuchuma, *definitely* itakuwa ni *conditional,* hata ile *Memorandum of Understand* tuliyosaini hapa mwaka 2001, kulikuwa na *provision also* ya kutoa *undertake* ya *Environmental Impact of Assessment*.

Kwa hiyo, hilo litaendelea kuzingatiwa na sasa ni zaidi, tuna Waziri hapa wa Mazingira, ambaye hawezi kuturuhusu kufanya kazi hii bila kufanya *assessment.*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nazungumzia juu *Vote* 66, Programu ya 10 kifungu 1001, kifungu kidogo cha 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kupata ufafanuzi kuhusu Sera iliyotumiwa na *PSRC* katika kuuza nyumba. Katika zoezi la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, tumeshuhudia jinsi ambavyo nyumba za mashirika hayo zilivyochukuliwa na kuwaacha wafanyakazi. Hizo nyumba zikagawanywa nyingine zikauzwa kwa wafanyabiashara na nyingine zikarudishwa Serikalini, zikauzwa kwa watumishi wa Serikali bila kuwajali wafanyakazi wa Mashirika hayo kwa kisingizio kwamba, labda wao ndiyo walishiriki katika kuyaua hayo Mashirika au kuleta *bad performance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni nani hasa aliyesababisha kuzorota kwa hayo mashirika? Kwa sababu wakati Mashirika hayo yalipoanzishwa enzi za akina Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, *STC* na kadhalika, yalifanya kazi vizuri sana. Tukaja kushuhudia baadaye jinsi yalivyokuwa yanafanya kazi vizuri, Siasa ikaingizwa kwenye Mashirika hayo tukapata *political commissars* katika Mashirika hayo, basi tukaanza migogoro ya *management,* pamoja na wafanyakazi na *political commissars* hao, kuwashawishi wafanyakazi kukataa maamuzi ya *management,* ndiyo Mashirika yakaanza kuzorota. Sasa ni nani hasa wa kulaumiwa?

Ni nani alikuwa anawateua Wenyeviti wa Bodi na Wakurugenzi wa Bodi hizi? Wafanyakazi walikuwa wanashirikishwa lakini wao walikuwa wanaletewa na ukweli ukaanza kujulikana kwamba, watu waliokuwa wanateuliwa walikuwa zaidi ni kwa utashi wa kisiasa na si kwa ajili ya utashi wa kuendesha hayo mashirika kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda nipate ufafanuzi kwamba, lawama hii anapewa nani na kwa nini hawa wafanyakazi wamenyimwa hizi nyumba? Sera gani

iliyotumika? Kwa hiyo, naomba nipewe ufafanuzi ili iweze kueleweka hawa watu walikuwa upande gani, kwa sababu Mashirika haya ni ya Serikali na Wafanyakazi wengine walitolewa wakapelekwa *on secondment* kule, kwa utashi wa Serikali yenyewe sasa ikaja ikawabagua, ikawafanya watoto yatima wakaachwa na migogoro imetokea kama mlivyoona ile ya Ukonga, watu walivyotupwa nje ya nyumba hizi. Kwa kweli kazi ya utekelezaji wa ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, mimi inanitia sana kero na ningeliomba nipate maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani maelezo yatahusu ufafanuzi kuhusu zile nyumba lakini nani wa kulaumiwa na nani walikabidhiwa mamlaka siku za nyuma, ni sehemu ya mjadala. Kwa wakati huu, haturejei katika mjadala wa vipi Mashirika ya Umma yalishindwa, ila tu tupate ufafanuzi kuhusu hili la ugawaji wa nyumba.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa ufafanuzi huo uliouweka, nilitaka nijibu lakini naona si vizuri kufanya hiyo *debate,* ni ya zamani.

Lakini labda niseme tu kwanza, Mheshimiwa John P. Lwanji, hakusema Mashirika gani lakini amezungumzia Mashirika ya jumla tu. Lakini mimi labda niseme hivi kwamba, kwanza pale tulipoanzisha *process* ya ubinafsishaji, Serikali ilikuwa inabinafsisha hata nyumba na kuna mfano wa nyumba zilizochukuliwa namna hiyo, *TBL* ni mfano mzuri sana, walichukua hata na nyumba zetu. Lakini baadaye tukagundua na tukashauriwa vizuri na tukagundua tu kwamba, hilo siyo sawasawa, tukasema ya kwamba, basi tutakapokuwa tunabinafsisha mashirika haya, tutashughulikia *core assets,* maana *core assets* ndiyo zitakazobinafsishwa ama kuuzwa.

Zile nyumba ni *non-core,* kwa mfano, Shirika la Reli *core assets* ni *track* ile, *workshops* zile, Maofisi, Mabehewa, Mainjini hizi ndiyo *core assets* zake, *Railway Station*s hizi ndiyo *core assets* zake, lakini zahanati, nyumba za watumishi, maduka, mahoteli kwa mfano, tulikuwa na hoteli hapa ya zamani ya *Tanzania Railway Corporation,* tulikuwa nayo Dodoma hapa, Tabora, Mbeya, Iringa, Kigoma na kadhalika, kwa hiyo hizi siyo *major functions z*a Shirika la Reli Tanzania, kwa hiyo hizi unaziondoa, ndivyo tulivyofanya.

Mashirika mengi kama nilivyosema hapo mwanzo, kuna mashirika mengine yaliuzia wafanyakazi tu kwa mtindo wa *MEBO,* yaani *Management and Employees Buy Out*. Kwa mfano, mmoja mzuri ambao mpaka leo nauwekea ni ule wa *Dar es Salaam RTC*, yaani *Dar es Salaam Regional Trading Company* na vilevile hata ya Mwanza. Kwa mfano, wale jamaa wa *Dar es Salaam RTC, Haji Brothers Building,* tumewakabidhi pale nyumba anayokaa *General Manager* ni ileile anakaa mpaka leo, hatukumuuzia mtu mwingine yeyote, ndiyo Serikali ya CCM imefanya mambo hayo. Kwa hiyo, *Tanzania Railways* zile nyumba za pale Uhuru Mchanganyiko, wameuziwa wafanyakazi na upande

wa pili wameuziwa watu wa *Harbours,* tena kwa bei poa ili kuwawezesha hawa wadogowadogo, ambao wanakaa nyumba hizo, waweze kuzimiliki.

Kwa hiyo, nasema labda *specific problem,* lakini *general issues* ndiyo hizo ambazo tumezifanya vizuri na mimi naomba tuzifanye vizuri na hii ndiyo Sera ya Chama chetu. Suala la kubinafsisha ni Sera ya Chama cha Mapinduzi tangu kwenye Ilani ya 1995 ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *Vote 66, Program Number 10* na *Sub Vote 1001,* kifungu kidogo 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia, pamoja na mambo mengi ambayo nilieleza, mengine nashukuru Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri, wameshayatolea maelezo, lakini kuna vipengele viwili ambavyo ningependa nipate maelezo ya ziada. Moja ambalo hawakuligusia kabisa na mimi nilichangia kwa uchungu kidogo ni suala la Posta. Nilieleza kwamba, Posta kwa Mujibu wa *Act Number 19* ya mwaka 1992, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mawasiliano, walitakiwa wakae wa-*determine* mtaji wa shirika na hawa watu hawajakaa toka miaka ya 1990 mpaka leo. Wale waliokuwepo nikatoa mfano kama vile mmoja yuko Mbinguni na mmoja yuko Duniani, hawajakaa mpaka leo.

Kwa hiyo, Shirika hili limekuwa linaendeshwa bila mtaji kutoka mwaka 1993, lilipoanzishwa mpaka sasa. Shirika hili limerithi madeni ya *East African Community*, wenzao wa *TTCL* wamesaidiwa kulipiwa madeni na mengine yamefutwa, lakini hawa hawakufutiwa, mikopo hawapati kwa sababu iko *specified*. Ule mradi wa *operation* wa Shirika hili mgumu kiasi kwambam ni yatima toka miaka ya 1990 mpaka leo.

Ni siku nyingi sana na toka limeanza kushughulikiwa suala la Posta, kwa kweli ni miaka nenda miaka rudi, Waheshimiwa hapa sitaki kuwataja, ni mashahidi na taarifa nilizonazo ni kwamba, Serikali ilifanya tathmini ya mikopo ya madeni na malipo ya pensheni ya wafanyakazi wa Posta iliyobaki kwa Serikali, ni *Cabinet* kutoa uamuzi namna ya kulikwamua shirika hili. Kama wenzao *TTCL* wamekwamuliwa, ambao ndiyo walikuwa na vyanzo vikubwa vya mapato ukilinganisha na Posta; hivi Posta kuna tatizo gani? Kwa nini hawa wanakuwa yatima na Wanyonge? Serikali ina kigugumizi gani juu ya kusaidia tatizo la Posta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka maelezo lakini sikupata lolote kwani halikugusiwa kabisa suala la Posta na mimi naomba nipate maelezo ya ufafanuzi kuna nini? Kulikoni? Lini Serikali kwa maana ya *Cabinet,* watakuwa waamuzi kuhusu suala la Posta ili Posta nao wajiendeshe kama Mashirika mengine, vinginevyo kama si umahiri na utukutu na *innovation* inayofanywa na viongozi wa Posta, hili Shirika lingekuwa limefariki kama siyo kufa. Naomba maelezo ya ziada.

Pili, nilieleze mapungufu ya Mkataba wa *ATCL*. Mheshimiwa Naibu Waziri, amejibu tu kwa ujumla kwamba, yamezingatiwa lakini nataka nikupe mfano mmoja na nilisema katika mchango wangu kwamba, ndoa ya *ATCL* na *South Africa* inakufa au imefikia mahali pale pa mwisho. Lakini Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Fedha yupo hapa, inaendelea kutoa shilingi milioni 500 kila mwezi, kuiwezesha *ATCL* kuendelea ku-*survive* mpaka leo, wakati ndoa ndiyo hivyo inafariki na baya zaidi ni kwamba, fedha hizi zinapotolewa na Hazina, zinakwenda mikononi mwa *South African Airways,* ndiyo wanaokamata na ndiyo wanaotumia na kadhalika. Sasa katika kipindi kigumu kama hiki, ambacho Hazina ndiyo inatoa fedha kwanza, lile siyo Shirila la Umma, hata hiyo Hazina kutoa pesa kupeleka kule sijui unaiitaje ni ruzuku, hisa au unaiitaje katika *terminologies* za kiuhasibu? Wanajua wenyewe hawa, unalipaje na kutoaje hela Hazina na kupeleka Shirika ambalo si Shirika la Umma?

Shilingi milioni 500 kwa muda sasa zaidi ya miezi saba au nane kila siku, Hazina wanapewa hizo hela. Sasa tutaendelea kutoa mpaka lini; hii ndoa itakufa lini na kwa nini sasa tuendelee kutoa hizi pesa, tunampa mtu ambaye tayari yuko pale? Bahati mbaya zaidi Management inaendelea ile ile, wanafanya maamuzi ya ajabu ajabu.

Hivi karibuni wameajiri Mhindi mmoja anaitwa Ajai na Mkenya mmoja wako *stationed* Nairobi, sisi hatuna ofisi Nairobi tumeshafunga kule, iliyopo kule ni *South African Airways.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata maelezo hii ndoa yetu inakufa lini na hizi hela za Hazina zinakwenda kwendaje kule na zitakwenda mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Lakini kuhusu yote mawili kwa sababu ni Posta na Shirika la Ndege, naona kama Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, ndiyo anaweza kutusaidia zaidi.

Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, tusaidie tafadhali.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mipango na Uwezeshaji, napenda kumjibu Mheshimiwa Mohamed H. Missanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hili la Posta ni kweli kwamba, Shirika la Posta liko katika hali mbaya kifedha, limerithi madeni kama alivyoeleza lakini kinachoendelea sasa hivi ni kwamba, mapendekezo ya kurekebisha Shirika hilo ili liweze kurudi kwenye hali ya neema yako *INTC*, ile Kamati ya Makatibu Wakuu ambayo inachunguza na baadaye kushauri Mawaziri ndiyo waweze kuamua. Kwa hiyo, yako *INTC* na baadaye kama ilivyo kawaida yatakwenda kwenye Baraza la Mawaziri na tumaini langu ni kuwa, muda si mrefu, Baraza litaamua na tutakuja kueleza hali ya shirika hilo kifedha, itakuwa namna gani, hii ni pamoja na Benki ya Posta vilevile kwa sababu yanahusiana. Kwa hiyo, ni jambo ambalo mimi naweza nikasema, limefikia tamati na linakaribia kuamuliwa, hilo la Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Shirika la Ndege la Tanzania, nalo wiki ya tatu ya mwezi huu, yatafanyika majadilano kati ya wataalam wa Serikali ya Tanzania na *PSRC*, kwa upande mmoja na Shirika la Ndege la Afrika ya Kusini kwa upande mwingine. Majadiliano haya yamesababishwa na kwamba, ingawa Shirika la Ndege la Afrika ya Kusini limekwisha jitoa kwenye ubia na Serikali ya Tanzania ndani ya Shirika la Ndege la Tanzania ilijitoa kuanzia tarehe 31 Machi, 2006.

Lakini papo hapo limeleta hoja, yaani madai dhidi ya Shirika la Ndege la Tanzania, ambayo ndiyo yatakuwa somo kubwa la majadiliano hayo ya wiki ya tatu ya mwezi wa nane. Ni kweli kwamba, hiyo tarehe 31 Machi, 2006, Serikali ingeweza ikajitoa mara moja na ikafanya hayo ambayo Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, anahisi ingebidi yafanywe. Uamuzi wa namna hiyo, ungeitumbukiza Serikali kwenye hasara kubwa sana kwa sababu yangetoka madai makubwa ya mabilioni ya fedha. Lakini sasa hivi, mazungumzo haya ya wiki ya tatu, yatahusu madai ya *South African Airways* dhidi ya *Air Tanzania* ya shilingi bilioni tano.

Kwa hiyo, busara ya Serikali ya Baraza la Mawaziri katika suala hili ni kwamba, tuzungumze kwanza na hawa tumalizane nao, ndiyo tuelewe jinsi ya kwenda mbele na jinsi ya kwenda mbele maana yake ni kuendelea na dhana ya kuwa na shirika jipya la ndege la Tanzania, kwa sababu hatuna nia, lakini tungekuwa na nia ya kulifunga tu, tungelifilisi na habari kwisha. Lakini tuna nia ya kutumia msingi uliopo wa *Air Tanzania* ili tuanzishe shirika lingine jipya la *Air Tanzania* na hatuwezi kutumia msingi huo kwa sababu msingi ile ni mali ya ubia huo *wa South African Airways* na Serikali ya Tanzania na ndilo somo la majadiliano hayo ya wiki ya tatu ya mwezi wa nane. Kwa hiyo, ni lazima moja liishe kwanza hili la majadiliano tujue limeishia wapi na ndiyo tujue jinsi ya kutumia msingi huo kuendelea na taratibu za kuanzisha Shirika jipya la Ndege la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Hazina wameendelea kutoa fedha kwa sababu bila fedha hizo, Shirika hili lingekuwa limekufa kifo, waswahili wanasema "kifo cha mende" na Serikali haikutaka kuona Shirika hili likikufa kifo cha mende.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, naona hajaridhika, sikiliza nyongeza kwanza kutoka kwa Waziri wa Mipango.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, kwa maelezo mazuri aliyoyatoa.

Nataka kutoa nyongeza moja ya juu ya kwa nini Serikali inataka kutoa fedha kwa Shirika la *ATCL*. Napenda kusema kwamba, Shirika la *ATCL* ni la Serikali, ni Shirika la Umma, kwa nini?

Kwa sababu asilimia 51 ya hisa ni za Serikali, kwa hiyo, bado ni la kwetu na wale wa *South African Airways* walichukua asilimia 49. Kwa hiyo, kimsingi Shirika lile ni la

Umma, ni lazima tuliendeleze pamoja na matatizo haya tuliyoyapa kama alivyosema Waziri. Sisi tuna hoja ya kwamba, Shirika lile tutaliimarisha wenyewe baadaye, kwa hiyo, hatuwezi kuliacha sasa hivi life.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru lakini Mheshimiwa Waziri, ndiyo anazidi kunichanganya anaposema lile ni Shirika la Umma na hapa anakuja na mfano ule kama hawa ambao wana asilimia 49 na asilimia 51 wanaendelea kusaidiwa na hawafanyi chochote. Lakini hawa wa Posta ambao ni asilimia 100 Shirika la Tanzania, miaka nenda rudi hawasaidiwi, hawa si ndiyo yatima niliosema?

Kwa sababu uchungu ule ule ambao Serikali inaona kui-*finance TTCL* wakati ni shirika ambalo tayari tumeshabinafsisha katika *record* yetu, wanaendelea kusaidiwa *500 million shillings*, licha ya gharama nyingine ambazo zimetokea, wanaweza kusaidiwa lakini hawa ambao ni asilimia 100, *shares* za Tanzania senti tano hawapewi na kila siku suala lake linapigwa danadana toka Serikali ya Awamu ya Tatu, nim-*offend* Waziri wangu wa Mawasiliano wa zamani, Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya pale, amehangaika nalo toka alipokuwa Waziri, licha ya *MTC* wakati huo, toka enzi ya Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya.

Hivi *MTCL* iko wapi jamani toka wakati ule *MTCL, MTCL,* si ipo, *Cabinet,* wanakaa wazee kila siku, inashindwa nini kuamuliwa, mbona haya mengine yameamuliwa kwamba, pelekeni pesa shilingi milioni 500 kila mwezi *ATCL.* Hilo limeamuriwa haraka tu bila matatizo, kuna *interest* gani? Hawa maskini ya Mungu, ambao hawana kitu hawajaamuliwa. Kwangu mimi inanipa tabu na sipati maelezo ya kutosheleza.

Kwa hiyo, ombi langu ninasema bado sijapata maelezo ya kutosheleza na ningepata *time frame,* kwa sababu toka enzi ya Awamu ya Tatu, suala hili lilikuwa *ATCL,* naomba sasa *time frame* ni lini *Cabinet,* kwa maana ya Serikali, watatoa uamuzi juu ya suala hili la Posta.

Mbili ni kwamba, juu ya *ATCL* nashukuru lakini kama ndoa haijavunjika si maana yake bado ubia upo? Kwa nini sisi Watanzania, Hazina iendelee kutoa shilingi milioni 500 peke yake, lakini wenzetu wa *South African Airways* hawachangii; si ndoa bado ipo pamoja? Bado shirika tunaendesha pamoja? Sisi Hazina tuchangie lakini wale kule hawachangii na hela hizi tunazotoa sisi wanaokwenda kuzitawala na kuzitafuna na kuzishughulikia ni *South African Airways,* ndiyo wanaopokea kama nilivyosema, mapato ya Tanzania kupitia *Ticket 083 Code* ya *South African Air ways,* yanakwenda Afrika Kusini.

Hapa hatubaki na chochote mpaka Waheshimiwa wale watumie, kama kitabaki ndiyo sisi tutapewa, kama hakibaki, basi tunaandikiwa madeni, ndiyo haya ambayo yanazungumzwa na Mheshimiwa Waziri pale na sasa tunaendelea na shilingi milioni 500 hizi. Sasa kama ndoa haijavunjika, hivi wenzetu hawana wajibu wa kuchangia katika kuiendesha hii *Airline* mpaka hapo Ndoa itakapovunjika kamili? Hayo ndiyo maelezo ambayo mimi nayataka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Lakini Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, ninavyoelewa mimi, ndoa ilikwishavunjika kama walivyoeleza Serikali tarehe 31 Machi, 2006, huyo Binti karudi kwa wazazi wake; sasa asitunzwe? Mbona iko wazi, Binti karudi kwa wazazi wake asitunzwe?

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikupingi *with due respect,* lakini hajarudi Binti kwa wazazi wake, bado *ATCL* inaendeshwa na Waafrika Kusini, bado pesa zote zinakwenda Afrika Kusini kupitia *tickets* na *tickets* zinazotumika ni *tickets* za *South African Airways, code* yetu ya Tanzania ni 197, haitumiki tena na mambo yote hayo kama unavyoona. Binti hajarudi kwa wazazi wake, bado yuko kulekule ukweni, sasa mkwe kwa nini hachangii? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nianze kwa kutoa maelezo kuhusu lile la Shirika la Posta. Mimi namwelewa *concern* yake, imenichukua muda, lakini sasa sisi watu wa Serikali ya Awamu ya Nne, tuna kaulimbiu yetu ya Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya na kwenye hotuba yangu ukurasa wa 52, *paragraph* ya 55, tumesema wazi kwamba, mashirika yaliyo katika hatua mbalimbali za urekebishaji ni pamoja na Shirika la Reli, Shirika la Bima la Taifa, Reli ya Tanzania and Zambia, yaani *TAZARA* na Shirika la Posta tunazishughulikia.

Hii *process* kama alivyosema mwenzangu, unajua mambo ya Serikali hayafanywi bila kufuata zile taratibu na taratibu nzuri sana ndiyo hiyo ya kutumia vikao mbalimbali ndani ya Serikali. Hoja hii au suala hili, liko mbele ya *Inter Ministerial Technical Committee*, wakimaliza hao ndiyo inakwenda kwa Mawaziri na mimi naweza kukuahidi kwamba, Serikali hii katika jambo hili, italishughulikia mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Kuhusu *ATCL* likifa leo unafikiri *South African Airways* watalia? Hawawezi kulia, watafurahi tu, kwa sababu watachukua zile *routes* za *ATCL* sasa na sisi tuwaunge mkono tuue *ATCL?* Sisi kama nchi, tuna *more interest of survival of ATCL by all means*. Lazima *ATCL* iweze ku-*survive,* hatutoi hela hizi kwa sababu ya kuwataka wale jamaa wale, hapana, tunataka *ATCL* iweze *survive*.

Lakini kuna Kanuni hapa za Mkataba wale wameshaondoka tangu tarehe 31 Machi, 2006 Binti yule yuko kwetu. Ndiyo! Yuko kwetu lakini sasa kama tukimwacha pale atakufa na kuwa kwetu ina maana zile gharama kwa mfano wewe binti yako karudi kwako ana watoto, watoto wale wako nyumbani kwako je watoto wale utawanyima chakula? Utasema bwana watoto hao umezalia huko? Hapana, *it can not happen that way* na haiwezekani kuwaacha wafe njaa.

**MBUNGE FULANI:** Na talaka bado haijakamilika?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Talaka bado haijakamilika ndiyo, lakini kuja kwetu ameshakuja. Kwa hiyo, sisi ni lazima tutunze watoto na tutunze na binti yetu, ili huko mbele ndiyo tujenge msingi mzuri wa kuanzisha

*Tanzania Airline*, yaani *National Air Line* na ndicho tunachokifanya. Ukikasirika na wewe, *South African Airways* watafurahi tu wale. Sasa hoja yetu ndiyo hiyo.

Unajua sisi tukifikiria mambo haya, tuna maslahi ya taifa sana. Sisi ni wazalendo pia, tunafikiria sana na *we take a lot of time,* tunabishana na kuelewana, siyo kwamba tunafanya tu kama wendawazimu, hapana ndugu zangu. Mimi nawaambia uamuzi huu umefanywa kwa makini na kwa maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote Number 66, Program 10, Sub Vote 1001, Item 250100.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia kwa maandishi, nililalamika sana kuhusu maendeleo na hasa ya uwekezaji Kusuni. Sasa kitabu hiki Mheshimiwa Waziri, ametupa hotuba yake tuisome kwa maana hiyo hata mimi hiki kitabu nitakipeleka kule Jimboni ninakotoka na Ruvuma ninakotoka. Waziri ameeleza kwamba, kitabu hiki huu ukurasa wa mwisho huu, hauna maana iliandikwa tu kwa makosa. Sasa yuko tayari kunihakikishia mimi ukurasa huu wa mwisho, ili nipeleke kule Ruvuma vizuri, auchane aweke ukurasa mwingine ambao una maana zaidi?

Kwa sababu ukurasa huu wa mwisho wa nyuma unaonesha jinsi watu hao wa Kusini wavyo-*suffer* kwa miaka 40 ya Uhuru na leo Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa tena anataka tuzidi ku-*suffer* tena kwa miaka 20 ijayo, tubaki hivyo hivyo kwa ukurasa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hotuba yake yote, inakinzana kabisa na maagizo ya Mheshimiwa Rais kwamba, sasa ni wakati wa kuelekeza nguvu katika maeneo ya Kusini na akataja maeneo ya Kusini ni yapi. Lakini nguvu ya humu ndani, akatupa na Waziri anayetoka Kusini, Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, hakukosea hata kidogo Mheshimiwa Rais. Lakini Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, anakazania tena huko huko. Sasa sisi tutaishi namna nani; tutafika lini sisi kuwa Watanzania? Maana watu wale ni Watanganyika bado, tutakuwa lini Watanzania sisi, tupate kiwanda, tupate hoteli nzuri?

Kwa mfano, mimi nina uhusiano na watu wa Malawi na huwa ninakwenda kule. Miaka mitano iliyopita nilipokwenda Kata Mbay, *Nkatta Bay* ni Bandari inayo-*correspond* na *Mbamba bay.* Kulikuwa hakuna vitu vya maana sana, nilipokwenda juzi nilikuta hoteli kubwa kabisa ya *Five Star,* nikawauliza wale viongozi, kwa nini mmefanya hivi, sisi tunajiandaa na *Mtwara Corridor.* Sasa wale wa Malawi wanajiandaa na Mtwara na *Corridor* na hoteli wameshajenga pale *Nkatta Bay,* ukifika *Mbamba Bay* ni aibu tupu kabisa. Sasa hii maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wewe mwenyewe ufike pale *Mbamba Bay,* uone hiyo *Mtwara Corridor*, mimi naona kichefuchefu, wanaposema *Mtwara Corridor, Mtwara Corridor,* naona kichefuchefu kabisa. Fika kule uone hali hii ninayoisema, haihusiani kabisa na hotuba na majigambo wanayoyafanya hapa. Ninaomba tuwe

*serious*. Nataka Mheshimiwa Waziri, aniambie haya aliyoyaandika humu ndani, yuko tayari kuyarekebisha ili na sisi kwa miaka 20 ijayo, tuonekane tunaweza kuwa na watalii wazuri. Tunaweza kuwa wawekezaji wazuri wa viwanda, maana tunazalisha sana, tunalisha nchi hii kwa chakula, tunazalisha mazao ya biashara, tunavua samaki na mapanki hayo na sisi tunayo pia kule Ziwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, arekebishe hiki kitu ili twende sawasawa. Ahsante.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa maelezo kuhusu hoja alizozieleza Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Kwanza, wakati nikitoa maelezo hapa Bungeni, nilitazama kule kwake sikumwona upande ule, sijui labda alikaa sehemu nyingine. Nimetoa maelezo marefu sana hapa kuhusu *Mtwara Development Corridor* na kwamba, hata mimi, Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, kama Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, nitatembea kutoka Dar es Salaam mpaka Mtwara, nikague barabara hiyo, halafu niende mpaka Masasi, Tunduru, Songea na mpaka *Mbamba Bay.* Nimesema hapa, kama sehemu ya kujifunza hali halisi iliyoko huko.

Lakini nilitoa maelezo kwamba, hiki kitabu huku nyuma, mnajua mimi lazima niombe radhi kwa sababu ndiyo Waziri mwenyewe, naomba radhi. Ndiyo maana nikasema haya mambo sio yenyewe katika miaka 20, haya ni ya mwanzo tu ya *planning*. Ni *planning* tu tena si *concrete planning*, ni *planning terms or planning ideas only.* Kwa hiyo, hiyo asipate matatizo. Nimweleza pale Mheshimiwa Peter J. Serukamba, kwa mfano, pale tuna miradi ya umeme unaokwenda Kigoma. Tuna Mradi wa Michikichi kwa mafuta ya kula, lakini pia kwa ajili ya kutumia kwenye magari. Humu hayamo haya, lakini fikra ziko hizi na sio fikra tu, kuna mipango tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, ametenga fedha tayari za kupeleka umeme. Songea pia safari hii umeme unapelekwa wa *grid,* zimetengwa nadhani shilingi bilioni nane au bilioni tisa, kwa ajili ya kupeleka umeme Songea na huwezi ukapeleka kiwanda kule bila kuwa na *power*. Kwa hiyo, ndiyo maana nimekwambieni na nikatoa mfano mzuri sana hapa wa Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, wakati alipokuwa *RC* wa Kilimanjaro na kuwaomba *RCs* wote na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu, ame-*organise* semina nzuri sana ya Wakuu na Mikoa na mimi kaniteua niende, ingawa nimebanwa sana nilitaka kwenda Jimboni, lakini nitakwenda pale, maana hapa ni amri, huo sio mchezo.

Kwa hiyo, moja ya jambo tutakalotilia mkazo ni kuwa na *initiative* pale pale ulipo. Kwa mfano, ukizungumza juu ya kujenga hoteli, *Mbamba Bay* au pale Liuli, unataka Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa anatoka Morogoro akajenge hoteli pale Liuli, haji. Ndiyo ukweli wenyewe huo. Unaweza kukataa lakini huo ndiyo ukweli, hawezi kujenga hoteli Liuli, hawezi kujenga hoteli *Mbamba Bay,* ni lazima watu wa pale pale wajenge hoteli hiyo. Kwa mfano, Mheshimiwa Capt. John D. Komba, umejenga

*Secondary School* nzuri Dar es Salaam. Mimi nilitarajia wewe ungejenga Shule ya Sekondari Mbinga. *It is true!* Huwezi kujenga kwa sababu Mbinga umeme ni matatizo. Kwa sababu unataka shule ile iwe na umeme, ndiyo maana tunafanya bidii umeme ufike Songea na uende Mbinga. *This is the economy reality of our country. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani tulipokuwa tunazungumza mambo ya ujamaa, akifundisha hapa Mheshimiwa Kingunge Mgombale-Mwiru na mimi nikiitwa Kingunge Mdogo, tulisema juu ya *economy reality, objective reality*, hali halisi ya mahali pale. Sasa hii ndiyo yenyewe. Kwa hiyo, sisi kama Serikali, *we are very committed.* Tena mimi ungesema Rais ninapingana naye, ninaogopa kabisa maana atanifukuza kazi. Mimi sipingani na Rais katika suala hili na mimi nimelitaja humu kwenye hotuba yangu, Mikoa ya Kusini tutaendeleza barabara, tutaendeleza Mchuchuma, tutaendeleza Liganga na mimi kama Waziri, nimetembelea mara nne Mchuchuma na Liganga. *Record* hiyo hakuna mwingine mwenye nayo; nani? Haijapata kutokea. Kwa hiyo, kusema sisi hatutaki kuendeleza Mikoa ya Kusini, *it is a misnomer and we shouldn't encourage this misnomer at all.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Capt. John D. Komba bado? Subiri kwanza, Waziri wa Miundombinu, anaongezea.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongezea jibu la Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa kwamba, nikiwa kama Mwenyekiti wa *Mtwara Corridor,* huwezi kuendeleza nchi yoyote kama haina miundombinu. Kwa hiyo, katika *Mtwara Corridor,* jambo la kwanza tunalofanya ni kuimarisha miundombinu, barabara inayotoka Mtwara kwenda *Mbamba Bay,* ndiyo kazi kubwa tunayofanya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza, tuna ahadi za wafadhili toka Mtwara mpaka Masasi, hiyo barabara tayari ina lami kilomita 54 kutoka Masasi. Tuna ahadi za Wajapan, kuanzia pale mpaka Tunduru, tuna ahadi za *BADEA* na Serikali ya Tanzania yenyewe. Barabara ya kutoka Tunduru kuelekea Songea mpaka *Mbamba Bay,* tuna ahadi za Japan na *African Development Bank*. Tarehe 8 Agosti, 2006, nilikuwa na bwana mkubwa wa *African Development Bank,* ndiyo maana mlikuwa hamnioni hapa, ametoa ahadi kwangu na ametoa ahadi kwa Mheshimiwa Rais. Marekani tunazungumza nao, Waziri wa Fedha yuko hapa, *Millennium Challenge Corporation (MCC),* barabara ile wameahidi kwamba, wataitafutia fedha. Tuna ahadi kutoka *Kuwait Fund* na tuna ahadi kutoka *BADEA.*

Kwa hiyo, tumaini langu ni kwamba, kilomita 54 Magharibi ya Masasi mpaka *Mbamba Bay*, wafadhili wote hao tukiwapanga vizuri, watakuwa wameisogeza sana barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Matumaini yangu ni kwamba, tukishapata barabara moja kutoka Mtwara mpaka *Mbamba Bay*, kwa kiwango cha lami, kitachobakia sasa ni kushughulikia vitu vingine viwili. Usafiri ndani ya Ziwa Nyasa, kama mnavyoelewa hilo, juzi juzi tu nilikuwa nimekwenda Dar es Salaam, kuharakisha kazi ya kuimarisha usafiri ndani ya Ziwa Nyasa na mipango inashughulikiwa na Shirika jipya la Bandari. Katika Viwanja vya Ndege sasa hivi kumeanza kutokea usafiri kati ya Dar es

Salaam - Mtwara - Pemba - Msumbiji. Kwa hiyo, ndege za Tanzania zinakwenda Pemba, ndege za Msumbiji zinakwenda Dar es Salaam kutokea Maputo – Pemba - Dar es Salaam. Kwa hiyo, usafiri wa ndege, umeanza kuimarika. Kwa sababu kama unajenga hoteli, watakaoenda pale wataenda kwa barabara, lakini wengi wataenda kwa ndege kama wanatokea Kaskazini au Kusini mwa Mbamba *Bay* au Kusini mwa Ziwa Nyasa.

Vilevile katika Ilani ya Uchaguzi, ipo kufanya upembuzi yakinifu wa reli itakayounganisha maeneo haya ya Mchuchuma na Bandari ya Mtwara na tayari tunaitafutia watu wa kuanza kufanya *feasibility study* ya reli hiyo.

Mwisho kabisa, tukifanya yote hayo, ndiyo sasa unaweza ukazungumza juu ya uwekezaji, kama huna miundombinu, huna barabara, huna uwanja wa ndege, huna meli, utaendaje *Mbamba Bay,* utaendaje Songea, utaendaje Tunduru, utaendaje Masasi na utaendaje Mtwara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka tu kumhakikishia Mheshimiwa John D. Komba kwamba, tena kazi hizi ninazosema, nimezifanya mimi mwenyewe kati ya mwezi Julai, 2006 na wiki iliyopita, kila siku nafikiria barabara ile, kila siku nafikiria *Mbamba Bay. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Capt. John D. Komba, nadhani unasimama kushukuru sasa.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli. Kwanza, Waheshimiwa Mawaziri hawa, ninawaheshimu sana na nina hakika wanachokisema ni cha ukweli, basi ni vizuri maana naogopa wasije wakaitwa wasanii baadaye. Sasa wawe wanasema ukweli, kwa sababu watu wa kule wamechoka na wanaposimama kusema maneno haya, unajua wanawasikiliza halafu wanafuga redio. Sasa wasije wakaitwa wasanii bure, bora wawe wakweli na waseme ukweli, halafu waje wawahukumu baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* … … … … … Sh. 435,175,700/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy Information Development* … … Sh. 649,276,500/=

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nina masuala kadhaa ya kisera. Kifungu 1003, *Policy Information Development*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masuala matatu ya kisera, ambayo napenda nipate maelezo. La kwanza, katika hotuba yangu nilishauri tufanyie mapitio sera yetu ya uwekezaji ili iandane sambamba na tunavyopitia upya mikataba mbalimbali, ambayo nchi yetu iliingia, kwa sababu mikataba yote hiyo inahusu uwekezaji. Lakini bahati mbaya, Mheshimiwa Waziri, hakuweza kueleza Sera ya Uwekezaji, sambamba na sheria iliyounda *TIC* ya mwaka 1997. Hilo la kwanza.

Pili, nilizungumzia sana na hili ni suala la kisera, umuhimu wa kuiwezesha *TIC,* kuweza kufanya kazi ya kuuza vivutio vya uwezekaji nchini kwetu vizuri na vilevile kuangalia uwezekano wa kuwapa motisha Watanzania wanaoanzisha makampuni binafsi ya kukuza uwekezaji *(Private Investment Promotion Agency)*. Lakini bahati mbaya pia sikuweza kupata majibu, napenda nipate majibu.

La mwisho kabisa, ni suala pia la kisera la *Mini Tiger Plan*. Niliongea katika hotuba yangu kwamba, kwa mujibu wa Katiba yetu Kifungu namba 63, ambayo ni majukumu ya Bunge, kifungu 63(3)(c), ambapo Bunge linapewa mamlaka ya kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mfupi, unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo. Sasa *Mini Tiger Plan* ni mpango wa miaka 20, lakini bahati mbaya, haukuletwa Bungeni, ulíletwa Bungeni kama semina, haujaletwa Bungeni kujadiliwa na kupitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata wasiwasi kwamba, kwa mtindo huo tutajikuta kwamba, Bunge linapitisha vitu kwa semina. Kwa sababu katika wiki iliyopita, nimegundua hata MKUKUTA ulikuja Bungeni sio kwa kujadiliwa na kutungiwa sheria kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri, nilishauri kwamba, angalie uwezekano sasa wa *Mini Tiger Plan* iletwe Bungeni ili kuweza kukamilisha taratibu za Kikatiba na tuweze kuitungia sheria kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo mara ya pili, maana nilitoa maelezo wakati huo Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto hakuwepo Bungeni, sasa anayauliza tena mara pili. Nilitoa maelezo marefu sana kuhusu sheria hii na nilikubali na tayari tuna mpango wa kuipitia upya sheria hii. Sheria hii ya Uwezekaji ni ya mwaka 1997, leo ni mwaka 2006, karibu miaka kumi imepita. Katika mazingira ya utandawazi, kuna vitu vingi sana vimebadilika. Kwa hiyo, mambo ya kurekebisha sheria hii, yamo ndani ya fikra ya Serikali, tunalishughulikia.

Kuhusu kutangaza vivutio pia nimesema hapa na nimesema kwa kirefu sana kuhusu Mkoa wa Kigoma kwamba, *TIC* itaendelea kutangaza, sisi Wizara tutatangaza, lakini sio Wizara yetu tu, Wizara ya Utalii, Maliasili na Mazingira wanatangaza, Wizara ya Miundombinu wanatangaza na kadhalika, kuvutia wawekezaji ndani ya nchi.

Nikasema vilevile kwamba, *charity begins at home,* pale nyumbani pia lazima mtangaze fursa mlizokuwa nazo, muandae mikakati ya ku-*explain* fursa zile na nikatoa mfano hapa wa Kilimanjaro, Mwanza na Mtwara. Hili nilishalieleza kwa kirefu kabisa na ninaomba nilirudie kwa namna hii.

Kuhusu *Tanzania Mini Tiger Plan,* nalo pia nimelitoa maelezo ingawa niliyatoa kwa muhtasari tu, kwa sababu tulisema hapa kwamba, tutatoa majibu yetu kwa kila Mheshimiwa Mbunge kwa maandishi ili aweze kuona.

Lakini kwa ufupi ni hivi, *Tanzania Mini Tiger Plan* tumeipitisha Bungeni hapa, sio kwa Semina tu, kwa kauli ya sisi Wabunge. Lakini zuri zaidi, tumepitisha Sheria ya *SEZ* mwezi Februari, 2006. Sheria ya *SEZ* imepita ndiyo inayo-*explain the implementation* ya zile *components* katika ile *Tanzania Mini Tiger Plan*. Nimeeleza kwa kirefu kabisa hapa. Kwa hiyo, unachotaka zaidi ya hapo ni nini tena? Mimi nasema hivi, maelezo haya yanatosha na shabaha yetu ni nzuri na moja ya *SEZ areas* ni Kigoma na itakuwa ile ya mashamba ya michikichi kwa ajili ya *bio fuel*, lakini haitakuwa mbaya kama tukiweka ile ya *edible oil.* Kwa hiyo, mambo haya yote yamekuwa *considered* katika maelezo yangu ya mwanzo na ninayarudia tena kwa ufupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa jibu la *Mini Tiger Plan* na kupitia upya Sera ya Uwekezaji na Sheria ya Uwekezaji. Nashukuru pia kwa kufahamishwa kwamba, Sheria ya *SEZ* ndiyo inatekeleza *Mini Tiger Plan*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili la *TIC*, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba, *charity begins at home*, lakini kwa mujibu wa sheria, *TIC* ndiyo ina jukumu la kuiuza nchi yetu na hapo ndiyo nazungumzia kuiongezea uwezo *TIC*, nina maana ya jinsi ya kupata wawekezaji kutoka nje, sina maana ya sisi ambao tunaweza kuwa wawekezaji wadogo katika Mikoa yetu. Nilizungumzia bajeti ya *TIC,* ambayo Serikali imeipa ni shilingi bilioni 1.4. tu na nikatoa mfano, Kampuni ya *TBL,* zao lao moja na *product* yao moja ya *Red Bull* wanaiuza kwa *dollar* 2,000,000, nchi inajiuza kwa chini ya *dollar* 1,200,000. Sasa nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri, anipe *commitment* kwamba, tunavyokwenda ni lazima *TIC* ijengewe uwezo wa kufanya kazi ya kuiuza nchi yetu. Hii ya kusema *charity begins at home*, tutafanya huku, lakini *TIC* kwa sababu ni chanzo cha kufanya kazi ya kuiuza nchi. Naomba Mheshimiwa Waziri, atupatie *commitment* ili mwakani tutapokuja hapa, tuone bajeti ya *TIC* imekua.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, katika hatua hii, Serikali hailazimishwi kutoa *commitment*. Hatua hii nimesisitiza mara kwa mara, ni ya kupata ufafanuzi na maelezo. Sasa Mheshimiwa Waziri, anaweza kusema juu ya maendeleo ya baadaye. Lakini kusema kuwe na *commitment,* tubaki hapa tupate *commitmen*t, itakuwa ni vigumu kwa sababu hilo ni suala la kugawa *resources* ambayo tayari tumeipitisha kwenye bajeti.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nimweleze Waziri Kivuli mwenzangu kwamba, hii *component* ya kuvutia wawekezaji, haifanywi na *TIC* peke yake. Nimesema tayari hapa kuna *Tanzania Tourist Board,* inafanya kazi hiyo. Nimetaja Wizara hapa ya Miundombinu, tena nikasema Waziri wa Miundombinu, alivyokutana na wahisani mbalimbali kwa ajili ya kuvutia wawekezaji nchini kwetu. Mheshimiwa Rais mwenyewe, kila akienda mahali anafanya kazi hiyo, Waziri Mkuu anafanya kazi hiyo na mimi kama Waziri, ninafanya kazi hiyo, tena bila kutumia bajeti ya *TIC.* Kwa sababu kuongezea uwezo maana yake nini? Hii *cake* yetu ndivyo tulivyogawana hivyo, haitoshi kwa sisi wote. Kwa hiyo, walichopata hapo ni sawasawa, ndiyo uwezo wa Taifa letu kwa hapo. Lakini kazi ya kuvutia wawekezaji inafanyika na Serikali nzima, sio *TIC* peke yake.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni ya 81(6), sasa zimesalia dakika kumi. Kwa hiyo, tutapitisha vifungu hivi vilivyopo kwa kupitisha mafungu wala sio vifungu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Macro-Economy* … … … … … Sh. 675,707,000/=
Kif. 2002 - *External Sector* … … … … … … Sh.1,628,326,500/=
Kif. 3001 - *Social Services and Human Resources Dev,* ... .... ..... ..... ..... ..... ...... .... Sh. 673,067,300/=
Kif. 3002 - *Poverty Eradication* … … … … … Sh.2,068,381,300/=
Kif. 3003 - *Economic Empowerment* … … … … Sh. 1,425,999,100/=
Kif. 5001 - *Public Investment Planning* … … … Sh. 789,282,700/=
Kif. 5002 - *Growth Strategies* … … … … … … Sh. 807,290,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 66 - Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji**

Kif. 1001 - *Administration and General* … … Sh.11,191,996,000/=
Kif. 1003 - *Policy Information Development* … Sh. 1,915,977,000/=
Kif. 2001 - *Macro- Economy* … … … … … … Sh. 124,370,000/=
Kif. 2002 - *External Sector* … … … … … … Sh. 9,330,000,000/=
Kif. 3001 - *Social Services and Human Resource Dev.* .... .... ..... .... ...... ...... ....... Sh. 809,909,100/=
Kif. 3002 - *Poverty Eradication* … … … … … Sh. 20,162,656,200/=
Kif. 5001 - *Public Investment Planning* … … Sh. 430,000,000/=
Kif. 5002 - *Growth Strategies* … … … …. Sh. 5,592,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Bunge lako Tukufu likikaa kama Kamati na kupitia bajeti ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kifungu kwa kifungu na kupitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kuwa, Bunge lako sasa likubali kuyapitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewe iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza asubuhi, tunayo shughuli ambayo itaanza saa 1.30 usiku na kwa maana hiyo, tunalazimika niombe au niwahoji ili tubadili muda ule wa jioni wa kukaa hapa Bungeni. Sasa nitamwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, tuweze kutengua kanuni inayohusika ili tukutane saa 10.00 hadi saa 12.45 jioni.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa mujibu wa kanuni namba 124, ambayo inasema: "Kwa idhini ya Spika, yoyote kati ya kanuni hizi yaweza kutenguliwa kwa madhumuni mahususi baada ya Waziri kutoa hoja kwa ajili hiyo."

Sasa naomba kutoa hoja kwamba, kanuni ya 21(3), ambayo inaeleza kwamba, Bunge hili litaisha saa 7.00 mchana na kuanza tena saa 11.00 jioni, kitenguliwe na badala yake Bunge hili likutane saa 10.00 jioni ili kutoa nafasi ya shughuli maalum, ambayo Mheshimiwa Spika, ameieleza na Bunge liahirishwe saa 12.45 jioni ili kutoa nafasi kwa shughuli hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja itolewe iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kutengua Kanuni ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha Shughuli za Bunge, kuna matangazo. Katibu wa Bunge anatangaza kwamba, katika vijisanduku vya barua mtakuta *CD* mbili, ambazo moja inaelezea wasifu wa kila Mbunge katika hali ya kufahamiana tu, ukiweka kwenye *Laptop* au kwenye *computer*, utaona wasifu wa kila Mbunge, amezaliwa lini, amesoma wapi na kadhalika na kadhalika ambayo ni *data. CD* ya pili, ina sheria zote za Tanzania na hizo *CD* zinatolewa bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, anawaomba nimelisahihisha kidogo hili tangazo, kwa sababu lilisema saa 7.00 mchana, nadhani mkutane mara baada ya huo Mkutano tutakaoenda, ambao naomba nikumbushe. Tunavyotoka hapa, tunakwenda kwenye mkutano mfupi wa kuelezana mambo muhimu, ambao umeandaliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, nawaomba Wabunge wote, tuweze kwenda tupate taarifa hizi muhimu. Ila tu nawaomba Waheshimiwa Wabunge, walio Wajumbe wa Kamati ya Uongozi na wale wa Tume ya Huduma za Bunge, Makamishna wote, tupitie katika *Speakers' Lounge* ya zamani ili tufanye mkutano mfupi sana na ndipo tuingie katika mkutano wa wote. Kuna Mheshimiwa Mbunge, amesahau ufunguo wa gari humu ndani, namwomba amwone *Sergeant- At-Arms* ataupata huo ufunguo wa gari naona kama ni Toyota.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa nasitisha Shuguli za Bunge hadi hapo saa 10.00 leo jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007 -**
**Wizara ya Fedha**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi iliyowasilishwa hapa Bungeni leo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii, kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, Mheshimiwa Anne S. Semamba Makinda, Mbunge wa Jimbo la Njombe Kusini, pamoja na Wenyeviti wa

Kamati za Bunge, kwa jinsi mlivyoendesha kwa umahiri, mjadala wa bajeti ya mwaka 2006/2007, tangu ulipoanza tarehe 13 Juni, 2006 hadi sasa. Aidha, ninashukuru kwa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati zote za Kudumu za Bunge katika kuchambua mapendekezo ya bajeti za Wizara, Idara na Mikoa. Pia Natoa shukrani za pekee kwa Kamati ya Fedha na Uchumi, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dr. Abdalah Omari Kigoda, Mbunge wa Jimbo la Handeni, kwa ushauri na mapendekezo waliyoyatoa kwa Wizara yangu. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, Serikali inathamini sana michango, maagizo na mapendekezo yenu na tutayafanyia kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yangu ya kuhitimisha mjadala wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2006/2007, nilibainisha ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Waheshimiwa Wabunge, ambao Serikali itauzingatia kuwa ni pamoja na:-

- Serikali itekeleze Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005;

- Mafanikio ya Uchumi mpana yawafikie wananchi;

- Matumizi ya Serikali yapangwe kwa vipaumbele kwa kuwa mapato hayatoshelezi mahitaji yote;

- Utulivu wa bei na thamani ya fedha yetu urejeshwe;

- Utulivu wa bei na thamani ya fedha yetu urejeshwe;

- Mifuko ya Dhamana za Mikopo iimarishwe;

- Wananchi wapewe elimu kuhusu mikopo;

- Mazingira ya kuanzisha vyombo vya mikopo ya nyumba, mikopo ya kukodi *(lease*) na mingine yawekwe;

- Mchango wa Sekta ya Fedha uongezwe;

- Riba ya mikopo ishushwe na ile ya amana ipandishwe; Sheria za kodi zisaidie kuvutia uwekezaji;

- Usimamizi wa fedha katika ngazi ya Halmashauri uimarishwe; Serikali Kuu ifuatilie matokeo ya matumizi ya fedha za Serikali, hasa katika ngazi ya Halmashauri;

- *TRA* iongeze juhudi za kukusanya mapato, yafikie angalau shilingi 200 bilioni kwa mwezi; na Kamati za Bunge zipewe muda wa kutosha kushiriki katika uchambuzi wa Bajeti;

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize kuwa, maelekezo hayo yatazingatiwa kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2006/2007. Katika hotuba ya Bajeti ya Serikali niliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 15 Juni, 2006, nilibainisha baadhi ya mafanikio katika sekta ya fedha kama ifuatavyo:-

- Bajeti za Wizara na Mikoa yote zinatayarishwa kwa kutumia Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati *(MTEF),* Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA), na Mpango wa Kimkakati (*Strategic Plan).*

- Mfumo wa kompyuta unaoitwa *Strategic Budget Allocation System (SBAS – 2)*, ndio unaotumika sasa katika kutayarisha mwongozo wa kuandaa bajeti ya Serikali. Mfumo huu unasaidia kuhakikisha kwamba, fedha za bajeti zinatengwa kulingana na matakwa ya MKUKUTA:-

- Mishahara ya Watumishi wa Serikali sasa inalipwa kwa wakati;

- Sheria mpya ya Benki Kuu ya Tanzania na Sheria mpya ya Mabenki na Taasisi za Fedha zilitungwa mwaka huu wa 2006;

- Kamati Maalum ya Mageuzi katika Mfumo wa Kodi *(Task Force on Tax Reforms*), imeendelea kuwa chombo muhimu cha kutoa ushauri kuhusu masuala ya kodi;

- Mpango wa kuboresha ukusanyaji wa kodi *(Tax Modernization Programme*) umebuniwa na unatekelezwa;

- Mkakati wa Pamoja wa Kusimamia misaada kutoka nje *(Tanzania Joint Assistance Strategy - JAS)* umekamilika; na

- Mifuko kadhaa ya kudhamini mikopo ya benki hasa kwa biashara ndogo ndogo na za kati, imeendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zimesaidia sana kuongeza ufanisi na kuboresha huduma zinazotolewa na Wizara ya Fedha na vyombo vilivyo chini yake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara iliendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali ya ndani na ya nje kwa kutekeleza yafuatayo:-

- Kurekebisha Muundo wa Mamlaka ya Mapato *(TRA)* ili kuboresha zaidi usimamizi wa vyanzo vya ndani vya mapato;

- Kurekebisha viwango vya kodi mbalimbali ili kulinda mapato ya Serikali;

- Kuziba mianya ya kukwepa kodi;

- Kuongeza ufanisi katika utawala wa ukusanyaji wa kodi hasa katika kitengo cha walipa kodi wakubwa;
- Kuimarisha uhusiano na wahisani na hivyo kuendelea kupata misaada na mikopo yenye masharti nafuu kwa wakati;

- Kuboresha mfumo wa kodi hasa katika biashara ya mafuta ya petroli;

- Kuboresha usimamizi na utendaji wa forodha kwa kuimarisha matumizi ya teknolojia ya *ASCYUDA++* katika vituo vya forodha ambavyo havitumii teknolojia hii kwa sasa; na

- Kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa mapato yasiyo ya kodi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara ya Fedha ilipanga kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi bilioni 1,961.8. Mapato ya kodi yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato yalilengwa kufikia shilingi bilioni 1,905.2 na Mapato yasiyo ya kodi shilingi milioni 56,538. Hali halisi ni kwamba, makusanyo ya kodi kutoka *TRA* kwa mwaka 2005/2006 yamefikia shilingi bilioni 1,971.4, ambazo ni juu ya makisio kwa asilimia tatu. Aidha, makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara ya Fedha kwa mwaka 2005/2006, yamefikia shilingi milioni 61,625.9, sawa na asilimia 109 ya makisio. Kwa mujibu wa taarifa za makusanyo, *TRA* ilivunja rekodi ya makusanyo kwa kukusanya shilingi bilioni 225.6 mwezi wa Juni, 2006. Kiwango hiki cha makusanyo ya mapato kwa mwezi, hakijawahi kufikiwa tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania mwaka 1995. Hii inadhihirisha kwamba, wito wa Waheshimiwa Wabunge wa kuitaka *TRA* iongeze juhudi za kukusanya mapato ili yafikie shilingi bilioni 200 kwa mwezi, imetimizwa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya ni makubwa sana, hasa ikizingatiwa kwamba, nchi ilipatwa na matatizo ya ukame, uhaba wa umeme, upungufu wa chakula na bei kubwa ya mafuta ya petroli. Mafanikio haya yanatokana na juhudi kubwa za Mamlaka ya Mapato katika kutekeleza Mpango wake wa Uboreshaji wa Ukusanyaji Mapato. Naipongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania, kwa mafanikio haya. Aidha, nawapongeza walipa kodi wote, ambao wanatimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa mujibu wa sheria na kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu ilipanga kupata jumla ya bilioni 1,631.3 misaada ya bajeti na mikopo ya masharti nafuu, kutoka kwa nchi wahisani na mashirika ya fedha mbalimbali ya Kimataifa. Hadi mwisho wa mwezi Juni, 2006, shilingi milioni 1,622,232 zilipatikana sawa na asilimia 99.4 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Benki Kuu ya Tanzania, iliendelea kuboresha mazingira ya kuwezesha benki za biashara kutoa mikopo. Aidha, amana za benki ziliongezeka kwa asilimia 35 katika mwaka ulioishia Aprili, 2006, hadi kufikia shilingi bilioni 3,473.9.

Aidha, mikopo ya benki kwa sekta binafsi, iliongezeka kwa asilimia 36.8. Katika kipindi hiki kilichotawaliwa na ukame, upungufu wa umeme na bei kubwa za mafuta ya petroli, mahitaji ya fedha za kigeni yaliongezeka sana kukidhi uagizaji wa petroli na chakula. Hata hivyo, ongezeko la misaada na mikopo yenye masharti nafuu, uwekezaji kutoka nje, pamoja na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, vilisaidia kuzuia akiba ya fedha za nje isiporomoke.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shughuli za mikopo midogo midogo *(Microfinance),* Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki Kuu, iliendelea kuboresha mazingira yatakayowezesha kukua kwa sekta hii. Wizara imeandaa miongozo ya uendeshaji itakayotumiwa na wawekezaji katika mabenki, *SACCOS* na *NGOs*, ili kuongeza uelewa na uwezo wa wadau katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2006/2007, Serikali itaendeleza sera nzuri za mapato, matumizi na ujazi wa fedha, ili kuhakikisha kwamba, mfumuko wa bei unakuwa wa chini, yaani asilimia nne na usiobadilika mara kwa mara; kuhakikisha kwamba, kiwango cha ujazo wa fedha ni sahihi na hautazidi asilimia 24 kwa mwaka; ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi usiopungua asilimia 37 kwa mwaka; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi isiyopungua sita.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa mikopo, Wizara kwa kushirikiana na Benki Kuu, inatekeleza Mkakati wa Kurekebisha Sekta ya Fedha, ujulikanao kama *Second Generation Financial Sector Reform,* ambao madhumuni yake ni pamoja na:-

(a) Kuimarisha uwezo wa Benki Kuu wa kusimamia shughuli za mabenki na vyombo vya fedha nchini;

(b) Kuimarisha Masoko ya fedha na mitaji;

(c) Kurekebisha Sekta ya Pensheni, ikiwa ni pamoja na kutunga sheria ya udhibiti wa shughuli za mifuko ya hifadhi ya jamii na pensheni na kuunda chombo kimoja cha kusimamia mifuko hiyo;

(d) Kuimarisha shughuli za Bima, hususan kwa kujenga uwezo wa Idara ya Usimamizi wa Bima *(ISD)* kusimamia shughuli hizo;

(e) Kuimarisha shughuli za mikopo midogo midogo mijini na vijijini, hususan kwa kuboresha usimamizi wa *SACCOS* na kuimarisha asasi zinazotoa mikopo midogo midogo;

(f) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu ya uzalishaji;

(g) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya nyumba; na

(h) Aidha, Serikali itaandaa Sera na Taratibu za kisheria zitakazo simamia utoaji wa mikopo ya uzalishaji ambayo ikiwa ni pamoja na mikopo ya rehani, kukodisha majengo, matrekta, mitambo na vitendea kazi *(lease financing).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ulioishia Desemba, 2005, Benki ya Rasilimali *(TIB),* ilipata mapato ya shilingi bilioni 7.9 ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 4.3 mwaka 2004, ongezeko la asilimia 84. Kiasi cha mikopo iliyotolewa na *TIB* katika mwaka 2005, ilikuwa shilingi bilioni 23.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 16.5 mwaka 2004.

Aidha, amana za wateja ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 33.7 mwisho wa Desemba, 2004 hadi shilingi bilioni 45.7 mwisho wa Desemba, 2005. Ufanisi huu uliwezesha *TIB* kupata faida ya shilingi bilioni 2.9 ikilinganishwa na shilingi milioni 858 tu mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wakati nikiwasilisha Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali, Serikali imeanza kuongeza mtaji wa benki hii ili iweze kuwa Benki ya Maendeleo. Tayari Serikali imekwisha ongeza mtaji wa benki hii kutoka shilingi bilioni 7.4 hadi shilingi bilioni 24.9. Serikali itaendelea kuongeza mtaji huo kidogo kidogo hadi kufikia shilingi bilioni 50.

Mheshimiwa Spika, *NMB* ilibinafsishwa mwezi Septemba, 2005 ambapo Serikali iliuza asilimia 49 ya hisa zake kwa Muungano wa kampuni nne zikiongozwa na *RABO Bank* ya Uholanzi. Kampuni hizo ni Kampuni ya Uwekezaji Tanzania *(National*

*Investment Company – NICO),* Kampuni ya Uwekezaji ya Chama cha Wenye Viwanda, Biashara na Kilimo na *Exim Bank.* Benki ya *RABO* ni moja ya benki kubwa duniani na ina uzoefu mkubwa katika fani ya Ushirika, ina mtandao wa benki ndogo ndogo zipatazo 328 zenye matawi 1,378 na vituo *(agencies)* 356 duniani kote.

Mheshimiwa Spika, mtaji wa *NMB* umeongezeka kwa asilimia 58.6 kutoka shilingi bilioni 35.5 mwaka 2004 hadi shilingi bilioni 61 mwaka 2005. Amana za wateja nazo ziliongezeka kwa asilimia 26 kutoka shilingi bilioni 492.1 hadi shilingi bilioni 620, wakati mikopo kwa wateja yenye thamani ya shilingi bilioni 88 ilitolewa katika kipindi cha mwaka 2005. Aidha, idadi ya matawi nayo imeongezeka kutoka 95 mwaka 1997 hadi matawi 115 kufikia Juni 30, 2006. Ufanisi huu uliingizia Benki hii faida ya shilingi bilioni 25.4 baada ya kodi na kuiwezesha *NMB* kwa mara ya kwanza, kulipa Serikali Gawio la shilingi bilioni 2.5.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwisho wa mwaka 2006, amana za wateja *NMB* zinatarajiwa kukua kwa asilimia 5.5 na kufikia shilingi bilioni 654 na mikopo kuongezeka hadi shilingi bilioni 125. Mtaji wa Benki hii unatarajiwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 78.7 wakati rasilimali ya *NMB* inatarajiwa kuongezeka na kufikia shilingi bilioni 748.4 katika kipindi hicho. Kwa kuzingatia ufanisi huu, Serikali inaandaa utaratibu muafaka wa kuwauzia Wananchi asilimia 21 kati ya 51 ya hisa zake katika benki hii kwa utaratibu wa *Public Offer.* Ni matarajio ya Wizara yangu kuwa, hisa hizo zitauzwa ifikapo mwezi Aprili, 2007.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Posta imeendelea kufanya kazi zake kwa ufanisi na tija. Katika mwaka 2005, Benki hii iliweza kukusanya amana za wateja zenye thamani ya shilingi bilioni 58.2, ikilinganishwa na shilingi bilioni 51.4 mwaka uliopita. Aidha, vitega uchumi viliongezeka kutoka shilingi bilioni 43.2 mwaka 2004 hadi shilingi bilioni 52.9 mwaka 2005 na mikopo nayo iliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 14.9 kutoka shilingi bilioni 12.2 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika,, *Twiga Bancorp Limited,* iliyokuwa inajulikana kama *National Bureau de Change* hadi Novemba, 2004, ni mojawapo ya taasisi za fedha za umma inayokua kwa kasi kubwa baada ya marekebisho ya jina na muundo wake. Katika mwaka 2005, benki hii ilipata faida ya shilingi bilioni 1.24 baada ya kodi, ikilinganishwa na shilingi milioni 364.3 tu zilizopatikana mwaka 2004. Aidha, amana za wateja zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 13.87 mwaka 2004 hadi shilingi bilioni 22.98 mwaka 2005. Benki hii imetoa mikopo ya shilingi bilioni 8.8 mwaka 2005 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.07 mwaka 2004, ongezeko la asilimia 24.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2006/2007, *Twiga Bancorp* itaendelea kuimarisha huduma zake hasa katika maeneo ya hati za malipo ya biashara ya nje *(letters of credit),* kutuma na kupokea fedha kwa njia ya maandishi *(telegraphic transfers)* na *Money Gram*. Aidha, Benki hii itajiunga na Mpango wa Kimataifa wa mabenki wa kutuma na kupokea fedha ujulikanao kama *SWIFT* na kufunga Mashine za Kisasa za kuchukua fedha wakati wowote *(Automatic Teller Machines – ATMs).* Juhudi hizi na

nyingine, zinatarajiwa kukuza amana za wateja hadi shilingi bilioni 23.36 ifikapo Desemba, 2006 na benki imepanga kutoa mikopo ya shilingi bilioni 12.553 mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2006, Idara ya Usimamizi wa shughuli za Bima ilikuwa imesajili makampuni 15 ya Bima, 32 ya Wakala wa Bima na Wakadiriaji Hasara 34. Usajili huu ni ongezeko la asilimia 9.7 ikilinganishwa na mwaka uliopita. Pato la bima limeongezeka kwa asilimia 17.7 kutoka shilingi bilioni 81.8 mwaka 2004, hadi kufikia shilingi bilioni 96.3 mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa ni kwamba, majengo, magari na mali nyingine za Serikali, hazikatiwi bima dhidi ya majanga mbalimbali. Wizara yangu inafanya utafiti ili kubaini faida na hasara zinazoweza kutokea endapo Serikali itaamua kukatia bima mali zake. Aidha, tumeanza utafiti wa kubaini uwezekano wa kuanzisha Bima ya Mazao *(Crop Insurance*) na Bima ya Mifugo *(Livestock Insurance)* kwa wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Shirika la Bima la Taifa *(NIC),* likisaidiwa na Serikali, linaendelea kupunguza mzigo mkubwa wa madai ya bima ya muda mrefu ya wateja wake. Katika mwaka 2005/2006, *NIC* iliweza kulipa madai ya shilingi bilioni 11.317 kati ya madai ya jumla ya shilingi bilioni 25.850.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kubinafsisha *NIC* chini ya Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC),* linaendelea vizuri. Mkakati ulioidhinishwa ni ama kutenganisha na kuuza tofauti biashara ya Bima za Maisha *(Life)* na Bima zisizo za Maisha *(Non Life)* au kuziuza zote kwa pamoja, kutegemea matakwa ya wazabuni watakaoshinda. Zoezi hili bado linaendelea na linategemewa kwamba, litakamilika katika muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2005/2006, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana *(CMSA)* imeendelea kusimamia maendeleo ya Soko la Mitaji na Dhamana hususan kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha kukua kwa Soko la Hisa la Dar es salaam na kuanzishwa kwa *Umoja Fund.* Aidha, Mamlaka inakamilisha utafiti wenye lengo la kuanzisha soko lingine la uwekezaji na mitaji *(alternative investment market)*, ili kupanua wigo wa uwekezaji na mitaji kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Soko la Hisa bado ni changa na halijaeleweka vyema, katika mwaka 2006/2007, Mamlaka itaendelea kutoa elimu kwa umma kuelezea umuhimu wa Soko. Aidha, ili kuwezesha Manispaa za Miji yetu kupata fedha kutoka kwenye soko za kuendesha miradi ya maendeleo, Mamlaka inashauriana na Wadau mbalimbali, kuhusu matayarisho ya kuziwezesha Manispaa kuuza kwenye soko Hatifungani *(Municipal Bonds).* Aidha, soko la Hisa la Dar es Salaam, linaboreshwa kwa kuwekewa vitendea kazi vya kisasa ili liwe soko la kisasa na linalovutia wawekezaji. Vilevile, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, inakamilisha utaratibu wa kutoa leseni, uwekezaji wa pamoja *(Unit Trusts)* na kusajili hatifungani zaidi katika soko. Serikali hivi karibuni imeuza hisa zake asilimia 30 katika kampuni ya *Tanzania Portland Cement* ya *Wazo Hill (TPCC),* kwa wananchi kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Hisa hizo zimekuwa na mvuto mkubwa kiasi kwamba, maombi ya kununua yalivuka idadi ya hisa zilizokuwa sokoni.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na *CMSA,* imekwisha andaa mapendekezo ya sheria mpya ya Kupiga Marufuku Michezo ya Upatu *(Pyramid Schemes),* ambayo imewaingizia hasara watu wengi hasa akina Mama. Sheria nyingine inayoandaliwa ni ile ya kuanzisha utaratibu wa *Central Depository System,* kwa ajilli ya kuweka kumbukumbu za hisa *(custodian of share certificates)* na kurahisisha uhamishaji wa umiliki wa hisa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Matarajio ya Wizara ni kuwasilisha miswada ya sheria hizo Bungeni katika mwaka huu wa fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Ukusanyaji na Udhamini wa Madeni *(LART)*, ulianzishwa kwa Sheria ya Bunge Sura Namba 134. Awali, Mfuko huo ulipaswa umalize shughuli zake mwaka 2001. Kutokana na kuongezeka kwa madeni, Serikali iliomba Bunge na likakubali kuongeza muda wa *LART* hadi Juni, 2004. Hata hivyo, kutokana na shughuli za *LART* kutokumalizika kama ilivyotarajiwa, Serikali iliomba kwa mara ya mwisho, nyongeza nyingine ya miaka miwili hadi tarehe 30 Juni, 2006 ili kukamilisha shughuli zilizokuwa zimesalia. Tathmini imeonesha kwamba, shughuli za *LART* zilizosalia, zinaweza kukamilishwa na asasi nyingine yenye uzoefu kama *LART* na ambayo haijamaliza muda wake. Hivyo, ilipofika tarehe 30 Juni, 2006, Sheria ya *LART* ilimaliza muda wake na hivyo *LART* pamoja na Baraza la *LART* hazipo tena. Shughuli zote za *LART* zilizosalia, zimehamishiwa *Consolidated Holding Corporation (CHC)* kuanzia tarehe 1 Julai, 2006.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha *(Gaming Board of Tanzania),* ndio msimamizi wa biashara ya michezo ya kubahatisha hapa nchini. Katika mwaka 2005/2006, Bodi iliweza kusajili *Casino* nane, sita zikiwa Dar es Salaam na nyingine Mwanza na Arusha na ilitoa leseni 99 za *slot machines* katika miji mbalimbali ya Tanzania.

Aidha, Bodi ilitoa leseni mbili za michezo ya Bahati Nasibu ya Taifa ya Lotto na *SMS* (ujumbe kwa njia ya simu), kwa Kampuni ya *Gaming Management Limited,* ambayo haijaonesha mafanikio ya kuridhisha. Katika mwaka 2005/2006, Bodi iliweza kuanza kujitegemea kwa kuwa na mapato yake yenyewe na hivyo kutotegemea ruzuku ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Wizara yangu itawasilisha marekebisho kadhaa kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha 2006, yanayozingatia mabadiliko ya sekta hii ikiwa ni pamoja na kuelekeza *Casino* zote, kutumia mfumo mmoja wa Kompyuta katika kuendesha biashara yao ili kurahisisha udhibiti na ukusanyaji wa mapato. Mfumo huu utawezesha Bodi kukusanya mapato yanayokadiriwa kufikia shilingi bilioni 1.6 kutokana na *Casino* pekee, ikilinganishwa na shilingi milioni 800 tu zilizokusanywa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kuwa mwanachama wa Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika wa Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu *(The Eastern and Southern Africa Anti-Money Laundering Group – ESAAMLG).* Hivi karibuni, Umoja huu ambao Makao Makuu ya Sekretariati yake ni Dar es Salaam, Tanzania, ulipata Katibu Mtendaji Mtanzania, aliyepatikana kwa njia ya ushindani miongoni mwa nchi 14 wanachama. Aidha, kama Wizara ilivyoahidi katika hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha uliopita wa 2005/2006, Serikali imewasilisha Bungeni kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya kwanza, Muswada unaokusudia kutunga sheria madhubuti ya udhibiti wa biashara ya Fedha Haramu na vitendo vinavyoambatana na fedha hizo, yaani *The Anti-Money Laundering Act,* 2006.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara yangu iliendelea kutekeleza hatua mbalimbali za kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, malengo na matarajio ya mwaka 2006/2007, ni kuendelea kuboresha utekelezaji na kuhakikisha Bajeti ya Serikali inasimamiwa kwa ufanisi zaidi.

Aidha, mafunzo kuhusu utayarishaji na usimamizi wa Bajeti kwa Wizara, Idara, Mikoa na Serikali za Mitaa, yatatolewa kwa maafisa wahusika. Wizara itaendelea kuimarisha Mfumo wa Ugawaji Rasilimali *(resource allocation*), ufuatiliaji na udhibiti wa bajeti ambao ni pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakiki matumizi ya fedha kulingana na malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara iliendelea kusimamia kikamilifu, mwenendo wa madeni ya Serikali ya ndani na ya nje, kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada na Mkakati wa Kusimamia Deni la Taifa. Hali ya Deni la Taifa ni nzuri baada ya kufutiwa kiasi kikubwa cha madeni na wadai wetu mbalimbali. Kwa sasa Deni la nje sio mzigo mkubwa tena kwa Serikali, kwa kuwa linalipika bila kuathiri malengo ya kiuchumi na fedha za Serikali. Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, juhudi za kusimamia Deni la Taifa zitaendelezwa kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kukopa kutoka kwenye vyanzo vyenye masharti nafuu kwa ajili ya miradi muhimu;

(b) Serikali haitatoa Dhamana kwa mikopo ya nje;

(c) Kuhimiza kukamilisha majadiliano na Nchi na mashirika wadai ambazo bado hazijatufutia madeni; na

(d) Kuimarisha uwezo wa wataalam wetu wa usimamizi wa madeni kwa njia za mafunzo na matumizi ya teknolojia mpya ya usimamizi wa madeni na uchambuzi wa miradi.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, katika mwaka wa 2005/2006, Tume ya Pamoja ya Fedha *(JFC),* iliajiri Mshauri Mwelekezi *(Consultant*), kubainisha mapato yanayotokana na vyanzo vya Muungano na kupendekeza vigezo vya kudumu vya kugawana mapato na kuchangia gharama za shughuli za Muungano. Rasimu ya mwisho ya taarifa ya mshauri imekwishawasilishwa kwenye Tume na inafanyiwa kazi.

Aidha, Tume ilikamilisha taarifa za Uchambuzi wa takwimu za madeni baina ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na ilichanganua gharama za Muungano kwa kipindi cha 1993/94 hadi 2003/2004. *JFC* pia ilifanya mapitio ya Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha Sura Namba 140 na imeshiriki katika Kamati ya Marekebisho ya Mfumo wa Kodi *(Task Force on Tax Reform)*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2006/2007, Tume ya Pamoja ya Fedha imepanga kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kukamilisha na kuwasilisha Serikalini mapendekezo ya vigezo vya kutumika katika kuchangia gharama na kugawana mapato yanayotokana na vyanzo vya Muungano;

(b) Kuwasilisha Serikalini, taarifa inayobainisha Wizara/Idara na asasi za Muungano na mchanganuo wa gharama za Muungano katika kipindi cha 1993/94 hadi 2003/2004 na taarifa ya uchambuzi wa takwimu za madeni baina ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(c) Kujaza nafasi za kazi zilizo wazi kwa mujibu wa Muundo wa Tume ya Pamoja ya Fedha; na

(d) Kuendelea kuelimisha wananchi na wadau wa masuala ya Muungano na majukumu ya Tume ya Pamoja ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuboresha mtandao wa malipo kwa kutumia kompyuta *(IFMS)* ili kuimarisha zaidi usimamizi wa fedha za Serikali. Ili kuhakikisha kwamba, nidhamu na ufanisi katika usimamizi wa fedha za umma vinaimarika, Wizara yangu itaendeleza Mafunzo ya Usimamizi wa Fedha na matumizi ya mtandao katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Aidha, nafasi zilizo wazi kwenye kada ya Ukaguzi wa Ndani ambayo tayari muundo wake umekamilishwa, zimeanza kujazwa sambamba na kutathmini uwezo wa watumishi kulingana na muundo.

Wizara yangu inasimamia zoezi la kudhibiti na kuboresha mapato yatokanayo na Viza zinazotolewa kwa wageni wanaoingia nchini. Zoezi hili linaendelea vizuri, kwani mpaka sasa mfumo wa kutoa *Viza* kwa njia ya kompyuta, umewekwa katika vituo vya Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam, Zanzibar, Balozi zetu za London, Paris, Washington, Roma na Ubalozi wetu mdogo uliopo Uholanzi. Pia Balozi zetu za Tokyo,

Brussels, Cairo, Moscow, Abu Dhabi na Riyadh, zimeshapokea vifaa vya kompyuta na mafunzo yametolewa kwa watumiaji wa mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007, mfumo huo utafungwa katika balozi zetu na ofisi za viza za Muscat, Berlin, Ottawa, New York, Stockholm, Otterup, Nice, Hamburg, Frankfurt na Milan. Vituo vingine ni viwanja vya Ndege vya Kilimanjaro na Mwanza, vituo vya uhamiaji vya mipakani vya Holili, Tarakea, Namanga, Horohoro, Mtukula, Rusumo, Kabanga, Tunduma, Kasumulu, Chilambo, Kasesya, Manyovu, Sirari, *Kigoma Port* na *Zanzibar Port*. Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuhakikisha kwamba, Viza zilizotolewa ziko katika viwango vya kimataifa na kwamba mapato ya Serikali yatokanayo na Viza yanadhibitiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, inaendelea na mkakati wa kujenga uwezo wa wataalamu wa ununuzi nchini kwa kuendesha mafunzo ya muda mfupi kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake. Wataalam 1,250 kutoka Serikali Kuu, Idara zinazojitegemea na Mashirika ya Umma, wameshaelimishwa. Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, mafunzo yataelekezwa kwa watendaji wa Halmashauri za Wilaya, ambao uwezo wao kuhusu masuala ya ununuzi, umekuwa unalalamikiwa na wadau mbalimbali nchini. Aidha, Wizara inaandaa mpango wa kuanzisha Kada ya Maofisa Ununuzi Serikalini ili kuchukua nafasi ya Kada ya sasa ya Maafisa Ugavi. Aidha, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma itajiimarisha kiuwezo ili iweze kusimamia kikamilifu, shughuli za Ununuzi katika Wizara mbalimbali, Mikoa, Halmashauri za Wilaya na Miji na Idara za Serikali zinazojitegemea.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Rufani za Kodi ilianzishwa chini ya Sheria ya Rufaa za Kodi Sura Namba 408. Majukumu ya Bodi hii ni kusikiliza na kutolea maamuzi, malalamiko kati ya walipa kodi na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Katika mwaka wa 2005/2006, Bodi ilisikiliza na kutolea maamuzi rufaa 55 kati ya rufaa 64 zilizofunguliwa.

Aidha, Bodi ilitoa elimu kwa wadau mbalimbali, juu ya utaratibu wa kufungua malalamiko katika Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Mara, Tabora, Singida na Kagera.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006/2007, Bodi ya Rufani za Kodi itaendelea na majukumu yake ya kusikiliza migogoro yote ya kodi na kuitolea maamuzi mapema. Sambamba na majukumu hayo, Bodi itaendelea na zoezi la kutoa elimu kwa wadau katika mikoa na wilaya ambazo elimu hiyo haijatolewa.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Rufani za Kodi nalo lilianzishwa kwa Sheria ya Rufaa za Kodi Sura Namba 408, ili kusikiliza rufaa zinazohusu maamuzi ya Bodi ya Rufani za kodi. Katika mwaka wa 2005/2006, Baraza lilipokea rufaa 33, ambapo rufaa 28 zilisikilizwa na kutolewa maamuzi. Rufaa zilizosalia zinaendelea kusikilizwa na kutolewa maamuzi ipasavyo. Aidha, Baraza liliendelea kuendesha mafunzo kwa wadau

mbalimbali wa kodi, kuhusu taratibu za kukata rufani kwenye Baraza ili kuongeza ufanisi wa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Baraza litajizatiti kusikiliza na kutoa maamuzi ya migogoro ya kodi kwa haraka zaidi ili kuondoa kero kwa wadau, pamoja na kuendelea kuwaelimisha kuhusu sheria, taratibu na kanuni za rufani za kodi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Wizara yangu ilikamilisha tathmini ya mali ya Serikali katika Wizara kumi na moja; ilihakiki Bohari 445 za Serikali; iliuza kwa mnada Magari 266, Mitambo 161, Pikipiki 52, *scrap lots* 52 na vifaa chakavu katika Mikoa kumi na tatu. Aidha, Serikali imefidiwa kiasi cha shilingi milioni 26.29 kutoka kwa maafisa waliosababisha hasara ya upotevu wa mali. Kwa upande mwingine, Serikali ililipa kifuta machozi na fidia ya jumla ya shilingi bilioni 3.06 kwa wadai 36. Aidha, taarifa 64 za upotevu wa mali zenye thamani ya shilingi milioni 330.45 zilifutwa kwa Azimio la Bunge Na. 9/2005 na tarifa za upotevu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2006/2007, Wizara yangu itaendelea na uthamini wa mali za Serikali katika Wizara saba na Idara zinazojitegemea tano. Uthamini huo utaiwezesha Serikali kuwa na Orodha Kuu *(Master Inventory)* na daftari la mali za Serikali *(Assets Register),* ikionesha thamani na muda mali iliponunuliwa na kuwezesha msawazisho *(Standardization)*, kwa mali za Serikali nchini kote kama ilivyoainishwa kwenye Sheria na Kanuni za Fedha za Umma za 2001.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Hesabu *(NBAA),* ndiyo mamlaka ya kisheria ya kusimamia taaluma ya uhasibu na ukaguzi hapa nchini. Kuanzia Julai, 2005, kuandika na kukagua hesabu za Mashirika na Makampuni kunafuata miongozo ya kimataifa. Miongozo hiyo ni pamoja na *International Financial Reporting Standards (IFRSs), International Standards on Auditing (ISAs)* na *International Public Sector Accounting Standards (IPSAs),* ili kwenda sambamba na viwango vya kimataifa vya taaluma hii.

Mheshimiwa Spika, *NBAA* kwa kushirikiana na wadau wake, imeendelea kutoa mafunzo na kusimamia uboreshaji wa elimu ya uhasibu kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo viwango vinavyotambulika na kukubaliwa kimataifa. *NBAA* pia, inatathmini Sheria mbalimbali zinazohusu uhasibu na ukaguzi wa hesabu za fedha hapa nchini ili kuhakikisha usimamizi na udhibiti wa viwango katika taaluma hii. Katika mwaka 2006/2007, *NBAA* imelenga kuhariri Mitaala ya mitihani, kuandaa *study manuals* na vitabu ili kuhakikisha inaendana na matakwa ya soko na mabadiliko ya kimataifa. Aidha, *NBAA* itaendelea kuhakikisha ubora wa kazi ya ukaguzi *(Audit Quality Review)* na inapanga kuanzisha Kituo cha Utaalam wa Wahasibu *(Accountancy Professional Centre)* hapa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Fedha za Umma Sura Namba 348 ya mwaka 2001, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali *(National Audit Office – NAO)* ni Idara inayojitegemea. Hata hivyo, kutokana na utaratibu uliopo, bajeti ya Idara hii huwasilishwa katika Bunge na Waziri wa Fedha. Kwa mwaka 2005/2006, Ofisi hii iliweza kutekeleza yafuatayo:-

(a) Ilikagua hesabu za Wizara na Idara 47, hesabu 33 za Wakala wa Serikali, hesabu 21 za Mikoa, hesabu 117 za Halmashauri na Ofisi kumi za Ubalozi wa Tanzania nje ya nchi;

(b) Ilitoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu, pamoja na semina kwa watumishi wa *NAO* ndani na nje ya nchi. Lengo ni kuwawezesha kufanya *Performance Auditing* kwa kutumia kompyuta na kuwaongezea viwango vya taaluma, ufanisi na utoaji wa huduma bora; na

(c) Ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2004/2005 imetolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2006/2007, ni kuhakikisha ukaguzi wa hesabu 53 za mafungu ya Wizara na Idara za Serikali, hesabu 33 za Wakala wa Serikali, hesabu 21 za Mikoa ya Tanzania Bara, hesabu 120 za Halmashauri za Miji na Wilaya na hesabu 20 za Balozi zetu nje ya nchi, pamoja na kusimamia ukaguzi wa Mashirika ya Umma. Aidha, *NAO* itaendelea na ukarabati wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu, pamoja na kujenga ofisi mpya za mikoa ya Mara, Mwanza na Lindi. Vilevile, itaendelea kutoa Mafunzo kwa viwango tofauti kwa watumishi wake.

Mheshimiwa Spika,, katika mwaka 2005/2006, Wizara ya Fedha imetoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu, nje na ndani ya nchi kwa watumishi wapatao 289 wa kada mbalimbali. Mkazo ulikuwa katika mafunzo yatakayowakwamua katika Miundo yao ya Utumishi. Katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi. Nafasi 400 za masomo katika fani za Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani, Uchambuzi wa Mifumo ya Kompyuta, Ugavi na Ununuzi, zimetengwa kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, vyuo vya Uhasibu na Fedha; *Tanzania Institute of Accountancy - TIA, Institute of Finance Management - IFM* na *Institute of Accountancy Arusha - IAA,* vimetoa wahitimu katika fani mbalimbali wapatao 3,793. Kati yao 960, ni Wahasibu, Wakaguzi wa Ndani, Wagavi na Wachambuzi wa Mifumo ya Kompyuta. Kwa ujumla, Wizara ilitoa udhamini kwa wanafunzi 2,697 ambao kati yao 2,300 walikuwa watarajali na 397 walikuwa watumishi. Aidha, Wizara imepanga kudhamini wanafunzi 3,050 katika mwaka wa 2006/2007, ambao kati yao 2,650 ni watarajali na 400 ni watumishi wa kada ya Uhasibu, Kompyuta na Ugavi katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha usalama wa kutosha, Serikali iliamua mishahara ya watumishi wake wote, ilipwe kupitia Benki ili kuondokana na tatizo la uporaji wa mishahara. Wizara, Idara na Halmashauri nyingi kwa sasa zinalipa watumishi wao kupitia benki. Jitihada zinafanyika ili ifikapo Oktoba, 2006 mishahara ya watumishi wote wa Serikali, iwe inapitia benki. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha mishahara inalipwa kwa wakati kila mwezi, kwa kupunguza muda wa kuandaa *payroll* ili ziwe zinatoka kila juma la kwanza la mwezi. Aidha, Wizara itaangalia uwezekano wa kusogeza karibu zaidi huduma ya malipo ya mishahara ili kupunguza usumbufu wanaopata watumishi walioko mbali na Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, tatizo la malimbikizo ya mishahara na posho mbalimbali kwa watumishi wa Serikali, limeendelea kuwepo ingawa limepungua sana baada ya kuwalipa walimu wa shule za msingi. Hadi mwisho wa Juni, 2006, kiasi cha shilingi bilioni 15.28 zilikuwa zimelipwa kwa watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, kama malimbikizo ya mishahara na posho baada ya kuhakikiwa. Kati ya hizo, malipo ya malimbikizo ya walimu yalifikia shilingi bilioni 7.48 na watumishi wengine shilingi bilioni 7.80.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo hilo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imekusudia kufanya yafuatayo mwaka huu wa 2006/2007:-

(a) Kwa kuwa hivi sasa Wizara, Idara, Mikoa na Halmashauri ni mamlaka kamili za kuajiri, kupandisha vyeo na kufanya marekebisho ya mishahara ya Watumishi, Mamlaka hizi zitaelimishwa kuhusu *Integrated Human Resource* na *Payroll System,* ili kuwawezesha kuingiza ajira mpya pamoja na marekebisho ya mishahara ya watumishi wao kwa njia ya mtandao.

(b) Kila Asasi itaunganishwa kwenye mtandao na marekebisho yataonekana moja kwa moja katika mitambo *(server)* ya Idara ya Kompyuta ya Hazina. Aidha, fomu ya kuombea marekebisho ya mishahara itaboreshwa ili kujumuisha marekebisho ya mishahara na posho kwa pamoja. Vile vile, jukumu la kuhakikisha kuwa watumishi wanaofariki, kuacha au kufukuzwa kazi, wanaondolewa kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara *(payroll),* litakuwa ni la Afisa Mhasibu. Wizara ya Fedha itabaki na jukumu la kufuatilia kuona kuwa malipo ya mishahara katika *payroll* yanafanyika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi bilioni 71.7 kililipwa mwaka wa fedha wa 2005/2006, ikiwa ni malipo ya pensheni na mafao mengine ya wastaafu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha wa 2006/2007, Wizara yangu imepanga kuchukua hatua kadhaa kupunguza adha kwa waastafu. Hatua moja tunayofikiria kuchukua ni kuhamisha wastaafu wa kada kadhaa, wanaolipwa na Hazina

wakahudumiwe na mifuko ya pensheni ikiwemo *PPF, NSSF, PSPF, GEPF,* ili waweze kufaidika na huduma za kisasa zinazotolewa na mifuko hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005/2006, lengo la Wizara yangu lilikuwa kuwarejesha katika Daftari, wastaafu 8,351 waliokuwa wamelipwa malipo yao ya uzeeni kwa mkupuo. Hata hivyo, ni wastaafu 7,022 ndio waliorejeshwa. Jumla ya wastaafu 17,805 wamerejeshwa kwenye Daftari la Wastaafu tangu zoezi hili lilipoanza miaka mitatu iliyopita. Lengo ni kuwarejesha wastaafu wanaokadiriwa kufika 26,536 hapo zoezi litakapokamilika. Kundi lingine lililorejeshwa ni wastaafu 279 wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* chini ya *General Fund Service (GFS)* iliyovunjika. Waastaafu hawa walikuwa wanalipwa pensheni yao ya kila mwezi na Ofisi ya *Public Trustees* Arusha, ambayo sasa imefungwa.

Mheshimiwa Spika, zoezi la ukokotoaji wa mafao ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, iliyovunjika mwaka 1977, lililoanza mwezi Julai, 2005, bado linaendelea. Kiasi cha shilingi 110.0 bilioni kilipelekwa benki kwa ajili ya kuwalipa wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki wapatao 35,036. Wastaafu 8,195 kati ya 35,036 waliokusudiwa kulipwa, hawajajitokeza kuchukua fedha zao. Juhudi za kuwapata wastaafu hao wajitokeze kulipwa mafao yao zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2005/2006, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali *(PSPF)*, uliendelea kutekeleza majukumu ya kusajili, kuhifadhi kumbukumbu sahihi za wanachama wake, kukusanya michango na kuiwekeza. Mfuko pia uliendelea kutekeleza jukumu la kulipa mafao kwa wateja wake waliostaafu. Tatizo la kumbukumbu za watumishi wa Serikali wanapostaafu, liliendelea kuwepo japokuwa limepungua sana. Katika jitihada za kuondokana kabisa na tatizo hilo, Mfuko umeendelea kukusanya kumbukumbu hizo wakati wa zoezi la usajili na wakati wa utoaji wa semina mbalimbali kwa wadau nchini kote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Mfuko ulikusanya jumla ya shilingi bilioni 122.49, michango ya waajiri na waajiriwa Serikalini, ambao ni wateja wa *PSPF.* Katika mwaka wa 2006/2007, Mfuko unatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 134.30 kutoka kwenye vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni, 2006, Mfuko ulikusanya shillingi 15,762.83 milioni sawa na asilimia 89.4 ya malengo ya mwaka mzima. Matarajio hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2006 ni kukusanya kiasi cha shilingi 18,454.52 milioni ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 4.9 ya lengo la mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma, Mfuko huu umekamilisha zoezi la kuingiza kumbukumbu za wanachama katika kompyuta na umeanza kutoa taarifa za michango kwa wanachama wake. Wanachama wote watakuwa wanatumiwa taarifa za michango mwezi Desemba kila mwaka. Hali kadhalika, taratibu za kuwahamishia wastaafu wote walio katika masharti ya mikataba katika mfuko, zitakamilika na kuanza kutumika katika mwaka wa fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Mfuko unalenga kuongeza mapato yanayotokana na vitega uchumi kwa asilimia 30, kuendelea kutoa elimu ili waajiri wanaotumia utaratibu wa mikataba wajenge tabia ya kuwachangia watumishi Akiba ya Uzeeni na kuhakikisha wanachama wanapata taarifa kuhusu michango yao kila mwezi Desemba. Mfuko unatarajia kukusanya jumla ya shilingi 23,391.40 milioni, kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma *(PPF)*, umeendelea kukua na kuboresha huduma yake kwa wanachama. Katika kipindi cha Januari – Desemba, 2005, mfuko ulikusanya shilingi bilioni 52.8 za michango ya wanachama, ikiwa ni ongezeko la asilimia 23 ikilinganishwa na shilingi bilioni 42.97 mwaka 2004. Mapato yaliyotokana na uwekezaji yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 14.18 hadi shilingi bilioni 25.9 katika kipindi hicho. Kwa upande wa mafao, Mfuko ulilipa jumla ya shilingi bilioni 17.1 mwaka 2005, ikilinganishwa na shilingi bilioni 14.7 mwaka 2004. Malengo ya Mfuko katika mwaka 2006/2007, ni pamoja na:-

(a) Kuongeza wanachama hasa kutoka sekta binafsi;

(b) Kutekeleza awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba 300 za bei nafuu huko Kiseke Jijini Mwanza. Awamu ya kwanza yenye nyumba 280. Hii ni sehemu ya mpango

wa nyumba 1,140 ambazo zitajengwa eneo hilo kwa ajili ya kuuzwa kwa wananchi kwa bei nafuu; na

(c) Kuboresha huduma kwa wanachama wa Mfuko ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo yenye riba nafuu, hasa kupitia *SACCOS* za wanachama.

Mheshimiwa Spika, katika mapambano dhidi ya ubadhirifu na rushwa, Wizara itaendelea kuboresha mifumo na taratibu za kazi ili kuziba mianya ya rushwa katika ukusanyaji wa mapato na katika matumizi ya Serikali. Wizara pia itaendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wote wa Wizara, Makao Makuu, pamoja na ofisi za mikoani Tanzania Bara kuhusu jinsi ya kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuyapa kipaumbele masuala ya jinsia katika nyanja mbalimbali. Wizara inatoa fursa sawa katika ajira, haki, mafunzo, kupandishwa vyeo na katika uongozi. Naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru Naibu Mawaziri wa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, Mbunge wa Jimbo la Makunduchi na Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Mbunge wa Jimbo la Kilosa, kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika kipindi hiki kifupi cha miezi sita na katika maandalizi ya bajeti hii. Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika yake chini ya Katibu Mkuu, Bwana Gray S. Mgonja na Naibu Makatibu Wakuu, Bwana Ramadhani M. Khijjah na Bibi Joyce K. G. Mapunjo. Nawaomba ushirikiano walionipa hadi leo uendelee ili tuweze kutekeleza kwa ukamilifu na kwa tija ya juu majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu ambayo nimekwisha yaeleza na kufikia malengo yaliyokusudiwa katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu inaomba Bunge lako liidhinishe matumizi yafuatayo: -

(a) Fungu 50 - Wizara ya Fedha: Matumizi ya Kawaida shilingi 157,150,900,000/=; kati ya hizo Matumizi ya Kawaida ya Idara na Taasisi chini ya Wizara shilingi 136,557,700,000/=; Matumizi Maalum shilingi 20,593,200,000/=. Miradi ya Maendeleo shilingi 33,764,800,000/=. Kati ya hizo; Fedha za ndani shilingi 5,023.0 milioni na fedha za nje shilingi 28,741,800,000/=.

(b) Fungu 22 - Deni la Taifa: Shilingi bilioni 282,235,300,000/=.

(c) Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali: Matumizi ya Kawaida shilingi 88,805,400,000/=; Miradi ya Maendeleo shilingi 6,153,800,000/=; Fedha za ndani shilingi milioni 454.0 na fedha za nje shilingi 5, 699,800,000/=.

(d) Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi: Matumizi ya Kawaida shilingi 9,027,500,000/=; Miradi ya Maendeleo shilingi 2,541,000,000/=. Fedha za ndani shilingi milioni 279.0 na fedha za nje shilingi 2,262,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 81 (1) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, tarehe 1 Juni, 2006, Kamati yangu ilikutana na Waziri wa Fedha, ambapo Kamati ilipata fursa ya kupitia, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2005/2006 na Taarifa ya Shabaha na Malengo ya Wizara hiyo, kama ilivyo kwenye Makadirio ya Matumizi ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Kamati inachukua fursa hii, kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakhia H. Meghji, Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib na Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Makatibu Wakuu wa Wizara, pamoja na Wakurugenzi wote wa Wizara kwa ushirikiano wao, walioutoa kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ni kiungo muhimili kutokana na majukumu yake ya kusimamia na kuendeleza uchumi imara, kwa kubuni na kusimami utekelezaji wa sera, ukusanyaji mapato na matumizi ya Serikali, pamoja na kusimamia utaratibu, udhibiti wa mfumo wa taarifa za kihasibu Serikalini za mapato na matumizi. Aidha, Wizara ina jukumu pia la kusimamia vitega uchumi vya Serikali katika Makampuni na Mashirika ya Umma na kusimamia na kuhakiki mali za Serikali na udhibiti wa deni la Taifa. Kimsingi kazi kubwa ya Wizara ni kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria za mapato na matumizi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, Wizara imepata mafanikio katika ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya Serikali. Aidha, nchi yetu imendelea kuwa na mahusiano mazuri na wahisani, pamoja na kusimamia vizuri matumizi ya umma na hivyo kufanikisha ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Kamati ilifahamishwa kwamba, Wizara ilitekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

(a) Kusimamia na kuendeleza uchumi wa miaka mitatu endelevu, yaani Mpango wa Matumizi ya Muda wa Kati *(MTEF)*.

(b) Kuboresha mapato kwa kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali ya ndani na nje, kupitia kwa Kamati Maalum ya Mageuzi ya Mfumo wa Kodi *(Task Force of Tax Reform)*, ambayo iliendelea kutoa ushauri kuhusu masuala ya kodi, Kuratibu misaada ya kiufundi kupitia *TRA,* kutayarisha Mkakati wa pamoja na kusimamia misaada ya mikopo ya masharti nafuu kutoka nje ya nchi *(Joint Assistance Strategy)*, kuimarisha

uhusiano na Wahisani hivyo, kuendelea kupata misaada na mikopo kwa wakati na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

(c) Kujenga uwezo *(Capacity Building)* na kubuni mbinu za kusimamia vizuri bajeti ya Serikali, kupitia utoaji wa mafunzo kwa wafanyakazi, pamoja na kuajiri watumishi wapya; kujenga uwezo na ujuzi katika fani ya ununuzi wa mali za umma pamoja na utekelezaji wa sheria za manunuzi.

(d) Kusimamia matumizi na kutoa mafunzo ya uhasibu kwa watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Kuimarisha kada ya ukaguzi wa ndani wa hesabu na kuimarisha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi. Kuanzisha mtandao hadi kwenye ofisi za Makatibu Tawala na Mikoa na Balozi zetu ili kuimarisha udhibiti wa mapato na matumizi na kushughulikia ajira za wahasibu na wakaguzi kwa ajili ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Mapato ya ndani na nje, Kamati kwa ujumla imeridhika na utendaji kazi wa Wizara kwa kipindi kilichopita. Aidha, imeridhika na hali ya mapato ambayo yameonesha kuongezeka. Hali hii inatia moyo, tukizingatia tumeweza kukabiliana hususan na tatizo la uhaba wa chakula, uliotokana na ukame, uhaba wa umeme na bei kubwa ya mafuta duniani. Kamati yangu inaipongeza Wizara na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Taasisi zake zote.

Kuhusu fedha za nje ambazo ni misaada na mikopo nafuu ya bajeti kutoka kwa wahisani mbalimbali kati ya kiasi kilichokadiriwa cha shilingi 100,656,244/= milioni, hadi kufikia Machi, 2006, kiasi cha shilingi milioni 100,332,959/= kilipatikana, ambazo ni sawa na asilimia 80.4. Kamati yangu inazipongeza nchi wahisani, kwa misaada yao. Hata hivyo, Serikali inatakiwa ifanye juhudi za makusudi ili kupunguza pengo la bajeti yetu ambayo ni tegemezi kwa asilimia 39.0. Mapato ya Serikali bado hayawiani na matumizi, hali inayosababisha kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ili kuziba pengo la bajeti.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuongeza juhudi ya kukusanya mapato yetu ya ndani. Hali hii itasaidia kudhibiti ongezeko la fedha inayotokana na mikopo na misaada kutoka kwa wahisani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazingatizo mengi yaliyotolewa na Kamati yangu kwa Wizara, yafuatayo yaendelee kupewa umuhimu upasao:-

(a) Kamati yangu inamsisitizia Waziri kuzingatia maoni ya ushauri iliyoyatoa mwezi wa Juni, 2006 wakati wa kujadili na kuchambua bajeti na Mipango ya Taifa.

(b) Suala la usimamizi wa matumizi ya Serikali ni muhimu katika kufanikisha maendeleo ya nchi. Kamati inaipongeza Wizara katika

kuihusisha Kamati kushiriki katika utaratibu wa *Mid Year Budget Review*. Hata hivyo, Kamati inazidi kusisitiza kuwa ili kuwe na uelewa mpana wa Kamati katika mchakato wa kuandaa bajeti ya Serikali, ni vyema Kamati ihusishwe katika hatua zote za mwanzo baada ya wataalam kuzifanyia kazi.

(c) Taarifa mbalimbali zinaonesha kuwepo kwa fedha za amana nyingi katika Mabenki hapa nchini. Aidha, Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Fedha, hususan Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, zinaendelea kutunisha mifuko ambayo hutumika katika kuwekeza katika majengo na amana za Serikali. Hata hivyo, ni vyema sasa jamii ya Watanzania walio wengi, waweze kutumia fedha hizi kutoka kwenye Mabenki na Taasisi za Fedha, kwa kupatiwa mikopo midogo midogo kwa masharti nafuu ili kuwekeza katika shughuli za biashara, uzalishaji mali kwenye viwanda na maendeleo, hususan kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi. Hii itawezesha kutekeleza MKUKUTA, pamoja na kutekeleza Mkakati wa Uwezeshaji kwa vitendo na elimu ya kukopa na kulipa iendelezwe na ihamasishwe baina ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa fedha Serikalini, kwa maana ya matokeo ya matumizi ya fedha za Serikali. Bado Kamati yangu inaishauri Serikali kuwekea mkazo eneo hili ili kupata thamani ya fedha inayotumika katika utekelezaji wa miradi na kuboresha hali za wananchi kupitia rasilimali za Serikali. Wizara ya Fedha itafanikiwa pale tu ambapo Mfumo wa Uhasibu na Ukaguzi, utakapoimarishwa na kutosheleza mahitaji ya taarifa muhimu zitokanazo na matumizi ya rasilimali hizo. Hivi sasa udhibiti umeegemea zaidi katika eneo la fedha *(Cash Basis).*

Hili bado halijatosheleza, Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla, wanahitaji kuelewa na kupata taarifa zaidi katika eneo la rasilimali na mali za Serikali. Bunge linahitaji kujua thamani ya mali za Serikali, ambazo ni za muda mfupi, kama vile mafuta ya magari, mitambo, vifaa vya kuandikia maofisini, vifaa na madawa hospitalini, mashuleni na kadhalika. Vyote hivi vinajumuisha gharama kwa rasilimali za Serikali. Zipo mali za Serikali kama vile majumba, magari, mashamba ya nafaka na mifugo, mashine na mitambo, barabara na kadhalika, zote hizi ni mali za Serikali. Wizara inaelewa thamani ya mali hizi ambazo ni *fixed assets*.

Mheshimiwa Spika, yapo Mashirika ya Umma na taasisi zake, ambazo zinamiliki mali nyingi, kwa mfano, *TANESCO*, *TTCL*, BIMA, Benki Kuu na kadhalika. Je, Serikali kupitia Wizara Fedha, inaweza kuelezea faida na hasara ipatikanayo baada ya uwekezaji huu wa Serikali? Kwa maana nyingine, kumbukumbu na mahesabu ya mali hizi, yanaweza kutolewa na Serikali. Je, Serikali inazo kumbukumbu za mahesabu ya *honorarium* na mirabaha inayopatikana kutoka kwenye misitu yetu, mazao ya utalii, madini, mbuga za wanyama na kadhalika? Hili ni changamoto kwa Wizara ya Fedha kwa vile linagusa moja kwa moja eneo la rasilimali za Taifa na utajiri wa Taifa. Kumbukumbu hizi ni muhimu sasa zianze kufanyiwa kazi, kwa vile hivi sasa

hazioneshwi sawa sawa kwenye *Balance Sheet* ya Serikali, kwa maana ya mizania ya Serikali.

Mifumo ya uwendeshaji na uwekezaji wa mitaji ni vigezo mahususi zinavyoonesha gharama inayoingia Serikalini kwa matarajio ya kutathmini faida au hasara kwa upande wa Serikali. Aidha, ni kigezo muhimu cha kuonesha kwa usahihi, uwiano kati ya akiba na uwekezaji Serikalini na uwiano wa uwekezaji, vikilinganishwa na Pato la Taifa. Inawezekana takwimu tunazozitoa zikawa chini ya viwango vya hali halisi, ikilinganishwa na viwango vya rasilimali na uwezekezaji kwa upande wa Serikali. Umefika wakati sasa, kwa vitabu vya Serikali kuonesha taarifa zote hizi ili kutoa picha halisi ya udhibiti wa mali na rasilimali zinazogharamia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi zinazoendelea tayari zimeshaanza kuchukua hatua ya kupambana na changamoto hii. Udhibiti unaanza kutekelezwa kwenye maeneo kwa mfano ya *IT Audit*, *Forensic Audit*, *Environment Audit* na *Cash Audit* na kadhalika. Mfumo wa uhasibu na udhibiti, hauna budi kupewa kipaumbele na Wizara ya Fedha ili uimarishwe tupate matokeo mazuri na ya thamani ya matumizi ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu kama ilivyoshauri awali, tunaikumbusha Wizara ya Fedha kuimarisha kitengo cha ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Serikali zilizotengwa kwenye bajeti, hususan Serikali Kuu na Serikali za Mitaa *(Expenditure Tracking Unit)*. Fedha hizi zinazokwenda kwenye Halmashauri zetu za Wilaya ni nyingi, hali hii itasaidia Serikali kuona matokeo ya matumizi ya fedha yanavyofanyika na thamani ya matumizi hayo.

Kamati yangu ilipata nafasi ya kutembelea Mradi wa Ujenzi wa Benki Kuu Dar es Salaam na Zanzibar, Kamati iliridhia hatua nzuri ambayo miradi ilifikia. Hata hivyo, Kamati inasisitiza, Serikali iwasilishe maelezo ya kina ya gharama za mradi huo kwa ujumla wake. Liko tatizo linalojitokeza mara kwa mara, wakati wa kujadili bajeti za Wizara mbalimbali, hasa katika eneo la utoaji wa fedha nyingi katika miradi Fulani, ikilinganishwa na mingine katika sekta husika. Tatizo hili si zuri na halileti tija au picha nzuri, licha ya kuwa miradi yote ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama kinachotawala.

Tatizo hili ni ushahidi tosha wa kujiuliza ni upi wakati muafaka wa kuchambua, kutathimi na kupitia bajeti za Wizara mbalimbali. Kinachojitokeza, utaratibu tuliojiwekea unatufanya tuichambue bajeti ndani ya Bunge, wakati huo si muda wake muafaka. Ipo haja sasa ya kuanzisha utaratibu wa kuchambua mipango na bajeti ya mwaka ujao kwa kina hivi sasa au mwaka huu, badala ya utaratibu huu wakati bajeti sasa inapoendelea, yaani *Current Budget*. Ipo haja sasa ya kuwa na wataalam watakaosaidia kutafsiri misingi ya *METF* na taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hatimaye taswira ya mipango na bajeti ya mwaka wa fedha ujao, iwe inaeleweka na Wabunge mwaka huu au hivi sasa kabla ya kipindi husika kufika.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu bado inasisitiza kuwa, hatuna muda wa kutosha kujadili bajeti ya sasa na ndiyo maana utaratibu wa kujadili kwa kina bajeti ijayo iliyooneshwa kwenye *METF,* inatakiwa ianze sasa. Utaratibu huu utapunguza tatizo

lililotajwa hapo mwanzo. Kimsingi katika kipindi hiki cha Bunge la Bajeti, ilipaswa sisi Wabunge tujikite zaidi katika kutafakari na kuiuliza Serikali, itawajibika vipi katika kuendesha mipango na bajeti iliyokwisha chambuliwa kutokana na mikakati iliyowekwa? Serikali itatekeleza vipi bajeti iliyopo, kulingana na miongozo na sera ilizoweka.

Kwa maana hii, kazi ya Bunge itakuwa ni kuangalia bajeti ya kila Wizara, kwa mfumo wa uwajibikaji na si kuanza kupanga tena bajeti ndani ya Bunge. Uchambuzi wa kina wa *METF* ni muhimu sana na hii inabakia kuwa ni changamoto kwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha. Kwa lugha ya Kigeni, mantiki ya ushauri huu ni ule wa suala la *timing*, wakati gani Wabunge tunafanya nini na wakati gani tunahoji nini juu ya mipango na bajeti zetu.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2006/2007, ili Wizara iweze kutekeza majukumu yake inaomba fedha kama ifuatavyo:-

Fungu 50, Matumizi ya Kawaida shilingi, 157, 150,900,000/=, Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni shilingi 33,764,800,000/=.

Fungu la 22, Deni la Taifa shilingi 282,235,300,000/=, Mhasibu Mkuu wa Serikali shilingi 88,805,400,000/=, Matumizi ya Miradi ya Maendeleo shilingi 6,153,800,000/=, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Matumizi ya Kawaida shilingi 9,027,500,000/= na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo shilingi 2,541,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe maombi haya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii tena, kumshukuru Waziri wa Fedha, Naibu Mawaziri na wataalam wote, kutoka Idara na Asasi zilizo chini ya Wizara Fedha, jinsi walivyoisaidia Kamati kufanya kazi zake kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii, niwapongeze Wajumbe wa Kamati yangu, kwa michango na maoni yao, pamoja na kufanya kazi kwa tija na ufanisi. Naomba niwatambue Wajumbe hao kwa majina yao, mbele ya Bunge lako Tukufu kama ifutavyo:-

Mheshimiwa, Dr. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti na Mheshimiwa Adam K. Malima, Makamu Mwenyekiti. Wajumbe ni Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Dr. Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Omari M. Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

Mheshimiwa Spika, hatimaye nikushikuru wewe mwenyewe binafsi, kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu, ambayo wakati wote wamefanikisha kazi za Kamati. Ni dhahiri kuwa, Mkutano huu wa Bajeti ni wa kwanza kwa Bunge letu ambapo sote tumeridhika na uendeshaji wake, ambao umezingatia *standard and speed*. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka na Makatibu wa Kamati, Ndugu Anselm Mrema na Ndugu Helen Mbeba, kwa kuwezesha na kuipa Kamati yetu, nyezo muhimu katika kufanikisha kazi zake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutamka kuwa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema na Utukufu, kwa kutujalia kukaribia kumaliza shughuli zetu za Bunge hili la Bajeti katika hali ya usalama, maelewano na katika kutujenga katika umoja ambao ndio ngao kuu ya kushinda katika vita vyetu vikuu vya kujenga Demokrasia ya kweli, ambayo ndio nyezo muhimu katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba upokee shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Bajeti, Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2006/2007, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukupongeza kwa umahiri wako wa kendesha shughuli zetu za Bunge kwa ufanisi wa hali ya juu. Sisi tuliomo humu ndani ya Bunge lako na Watanzania waliokuwa wakifuatilia shughuli za Bunge, watakubaliana na mimi kwamba, wewe ni muungwana, kwani sifa kuu ya muungwana ni yule atembeae kwenye maneno yake, nawe umetembea kwenye maneno yako, *Speed and Standard*. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, filosofia mpya, huchukua muda kuelewaka hasa kwa watu ambao fikra zao hazipokei haraka mabadiliko. Hivyo, katika kutekeleza azma yako njema, ni dhahiri utakumbana na vikwazo vingi. Naomba uwe mvumilivu na viwe chachu kwako katika kuongeza *Speed and Standard*. Kazi ya kujenga ni ngumu, lakini kubomoa huwa haihitaji Wizara na mabomu yao hata kibiriti kinatosha.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imeridhika na utendaji wako, hukupata hata wakati mmoja kudai kuona hotuba zetuhivyo, tunazidi kukuhakikishia kukupa kila ushirikiano katika kulifanya Bunge letu, liwajibike ipasavyo kwa wananchi wa Tanzania. Kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni, ambazo zote zinahitaji ama kuandikwa upya Katiba au mabadiliko makubwa Sheria na Kanuni, kazi ambayo umekwishaianza, kinachohitajika ni kwa wale wenye nia ya kweli ya kutaka kuimarisha utendaji wa Bunge letu kukupa ushirikiano kama tulivyokuahidi sisi Kambi ya Upinzani. Lakini, wote humu

tuna nia hiyo hasa tukitilia maanani maneno ya Rais wetu kuwa, sote mdau wetu ni mmoja, ni Mtanzania wa Kawaida. Hivyo, naamini kabisa kuwa katika kikao kijacho, tutakuwa na kanuni ambazo kwa kiasi Fulani, kinakidhi malengo tuliyokusudia ya kulifanya Bunge liwe mhimili wenye kusimamia kwa dhati Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani, kwa ushirikiano wao walionipa katika kutimiza majukumu yangu ya Kiongozi wa Upinzani, aidha, nimshukuru kipekee, Mheshimiwa Dr.Wilbrod P. Slaa, kwa kutoa kila ya aina ya ushirikiano katika kuiongoza kambi yetu. Mawaziri Vivuli na wasaidizi wao, wamefanya kazi kubwa nzito, mimi kama kiongozi wao, nimeridhika na uwakilishi wa hoja zao Bungeni. Naamini, Watanzania wengi, watajuta ni kwa nini hawakutuleta wengi hapa Bungeni, lakini msijute kwani ukupigao ndio ukufunzao. Tuchagueni kwa wingi kwenye uchaguzi wa Serikali za mitaa na hatimaye Uchaguzi Mkuu ujao.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa si kutenda haki, kama sikutoa shukrani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Waziri Mkuu, pamoja na Mawaziri wote, kwa ushirikiano mkubwa tulioupata kama Kambi na mimi binafsi katika kutimiza majukumu yetu.

Tunaomba kumhakikishia yeye na Watanzania wote kuwa, Kambi ya Upinzani na vyama vyetu, kwanza kila wakati tutatanguliza maslahi ya Taifa kuliko itikadi zetu, pili hatutoacha kupongeza kwa mazuri Serikali inayoyafanya, lakini pia hatutaacha kufichua na kuyasema mabaya yanayofanywa na Serikali maana huo ni sehemu ya wajibu wetu. Katika kikao hiki, Kambi na Wabunge kwa ujumla, tumedai ufafanuzi na kuomba vielelezo katika maeneo mengi, yapo uliyatolea maelekezo na yapo ambayo Serikali imeahidi kutupatia maelezo na vielelezo. Ni matumaini yetu, Serikali itatupatia taarifa kamili kwa kila tulichoomba hapa kama ni sehemu ya Serikali kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, wakati Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, wakijibu hoja mbalimbali za Wabunge, suala la mpasuko wa kisiasa Zanzibar, lilijitokeza na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, alilitolea kauli. Kauli ambayo imethibitishwa zaidi na vitendo anavyovifanya Spika wa Baraza la Wawakilishi vya kuuthibitishia umma wa Watanzania na Ulimwengu kwa ujumla kwamba, mpasuko uko ndani ya Mihimili ya Serikali, Baraza likiwa mmoja wapo. Naomba kuweka katika kumbukumbu kuwa, Watanzania na hasa Wazanzibari, hawataki tena kauli nyingine, wanataka kuona hatua za wazi wazi katika kulishughulikia suala hili, maana viongozi wanaoendelea kuwatuliza wananchi kwamba, wasubiri utekelezaji wa kauli ya Rais na Amiri Jeshi Mkuu, aliyoitoa hapa Bungeni, sasa hawaaminiki tena, wanaonekana kama ni mapandikizi.

Mheshimiwa Spika, naomba kukumbusha aliyoyasema Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kuhusu matokeo ya mwaka 2001 hadi kuundwa Tume ya Brig. Jen. Mstaafu, Balozi Hashim Mbita, yaliotokea 2001, yaliitia doa nchi yetu, si vyema yakajirudia.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kumpongeza Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Naibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib na Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, pamoja na watendaji wote wa Wizara na asasi zake, chini ya Katibu Mkuu wao Bwana Mgonja, kwa kazi nzuri wanayoifanya, katika kushughulikia masuala ya kifedha na hasa mapato na matumizi ya Serikali, pamoja na kuratibu vitega uchumi vya Serikali katika makampuni na mashirika ya ndani na nje ya nchi. Majukumu haya yameelezwa kwa upana na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Bajeti, pamoja na Bunge lako Tukufu, kupewa mamlaka na Katiba ya kuisimamia Serikali katika kutekeleza majukumu yake, Wabunge hawapati fursa ya kushiriki katika mchakato mzima wa mipango ya muda mfupi na mrefu, pamoja na maandalizi ya bajeti ya nchi. Matokeo ya haya ni kwa Wabunge kuongea ndani ya Bunge kwa sauti kali na hatimaye kuridhia hata kama hakupata majibu muafaka kwa aliloshauri.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Wabunge wanahoji vipaumbele vya ujenzi wa miradi ya maendeleo kwamba, hakuna uwiano, kutokana na utaratibu wetu, Mbunge hawezi kubadili vipaumbele hata ikidhihirika kuwa kulikuwa na haja ya kufanya hivyo, aidha, upo wasi wasi wa hata bajeti tunayopitisha hapa sio matumizi halisi yanavyokwenda.

Mfano, ulio hai ni hivi karibuni tulipopitisha Bajeti ya Waziri Mkuu na kuarifiwa kuwa kila mkoa utapewa shilingi milioni mia tano. Hivi karibuni tumesikia Rais ameongeza na kuwa shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa. Nia hii, Kambi ya Upinzani inaipongeza na ninaomba Waheshimiwa watuelewe hivyo, lakini tunachosema hapa ni utaratibu wa Kikatiba na Sheria. Ongezeko la 10.5 bilioni lazima limeongeza matumizi ya Serikali, lakini pia inaonesha kuna mapato ya Serikali, ambayo Bunge lako haliyajui na hivyo Serikali ina mamlaka ya kuyatumia bila ya idhini ya Bunge. Ni nani aliyeidhinisha fedha hizo za ziada au kuna mapato gani ya Serikali ambayo hayahitaji idhini ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele hapa, ni kutekeleza sheria ya kuwalipia wanafunzi wote waliofaulu kuingia vyuo vikuu au ni kutumia fedha ambazo hata mpango wa matumizi yake haujaridhiwa na Bunge? Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri alieleze Bunge lako Tukufu:-

Ni mfumo gani wa kibajeti, unaoruhusu kuongezewa fedha bila ya idhini ya Bunge, kutokana na kutokuwepo programu ya matumizi ya mfuko huu, haukuidhinishwa na Bunge bali umepitia kwenye *briefing* tu ya Wabunge hivyo, haukuwahi kufanyiwa kazi. Fedha zinazoanzisha mfuko huu, zinatokana na mapato ya Muungano; je, utaratibu wa Wilaya za Zanzibar utakuwaje?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara ya Mambo ya Nje, ilitumia si chini ya shilingi bilioni nne zaidi ya bajeti, iliyoidhinishwa na Bunge kinyume na taratiibu za Sheria ya Fedha. Bajeti ya mwaka huu, tumeshuhudia Serikali ikifuta *VAT* kwenye mafuta bila ya kuonesha wazi wazi pengo litazibwa kwa njia gani, matokeo yake

bei ya mafuta iko pale pale, ukiacha mafuta ya taa ambayo hayasababishi sana ongezeko la gharama za uzalishaji.

Kambi ya Upinzani, katika kutekeleza matakwa ya Katiba ya Majukumu ya Bunge inaitaka Serikali kuwa na mfumo wa mipango ya bajeti kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Shirikishi katika kuweka vipaumbele na hata kuweka viwango vya matumizi;

(b) Kuwa wazi zaidi kwa kila *Vote, Sub Vote* na vifungu vidogo ili kupata usahihi wa fedha iliyotengwa. Kwa mfano, ni vyema kujua, ukiacha safari za dharura, Rais anategemewa kusafiri mara ngapi katika mwaka na gharama zake ni kiasi gani;

(c) Kamati za kisekta za Bunge, zijengewe uwezo wa kufanya ukaguzi wa thamani halisi *(Value for Money Audit),* ili kuweza kuoanisha matumizi na thamani halisi;

(d) Kamati ziweze kwenda kwa undani zaidi katika kujua vyanzo vya mapato na kama kweli walipa kodi wanalipa kodi wanayostahili kulipa kwa mujibu wa sheria; na

(e) Kushiriki katika kuishauri Serikali katika kupanua wigo wa kodi na kuziba mianya ya ukwepaji kodi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuupongeza uongozi wa *TRA,* kwa kazi nzuri ya kukusanya Mapato ya Nchi, kwa ufanisi wa wastani kwa kulinganisha na majirani zetu. Tulikotoka na tulipo, ipo tafauti kubwa, hongereni.

Mheshimiwa Spika, matatizo yanayoikumba *TRA* ni pamoja na misamaha ya kodi, ambayo kwa kiasi kikubwa, inapunguza wigo wa kodi. Pamoja katika hotuba ya Waziri ameelezea juhudi zinazokusudiwa kuchukuliwa katika eneo hili, lakini Kambi ya Upinzani inaona hii ni ahadi ya kila siku, bila ya kuwa na utekelezaji thabiti.

Mheshimiwa Spika kwa mfano, Serikali iliingia Mkataba na *Alex Stewart,* wa kufanya *assay* ya dhahabu kwa malipo ya asilimia 1.9 kati ya asilimia tatu ya mrabaha kutokana na dhahabu inayosafirishwa na Serikali kubakiwa na asilimia 1.1 tu.

Mwaka 2004 mauzo yalikuwa Dola 680.2 milioni na 2005 Dola 711.3 milioni, jumla kwa miaka hii miwili ni Dola bilioni 1,391.5. Kwa mgao, kampuni hiyo imelipwa shilingi milioni 34 na Serikali imepata shilingi milioni 20 tu, malipo haya hayana kodi yeyote.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa kampuni hii imekwishalipwa *USD* 35 milioni na Mkataba umeongezwa muda hadi 2007, ambapo atakuwa amelipwa *USD* 65 milioni, je, Serikali iko makini katika kuziba mianya ya kodi? Lakini wasi wasi zaidi ni je, hizi fedha za mrabaha zinalingana na kiasi alichokwisha kulipwa?

Tunaomba mahesabu ya uhakika kama kima kilicholipwa, kweli kimetokana na makusanyo ya kodi na mrabaha wa tokea alipowekeana mkataba na Serikali.

Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge lako Tukufu, ni nani mwenye mamlaka ya kuipunguzia Serikali mapato, maana kitendo cha kuongeza muda bila ya idhini ya Bunge ni kitendo cha kuipunguzia Serikali mapato.

Aidha, wakati Waziri wa Fedha na Waziri wa Nishati na Madini, wakijibu hoja hapa Bungeni, waliahidi kutoa taarifa rasmi juu ya matokeo ya uchunguzi uliofanywa na kampuni hii, ili na sisi Wabunge turidhike na matumizi hayo makubwa ya fedha za wavuja jasho, yaliyofanywa bila idhini ya Bunge. Kwa kuwa Waziri nilimwarifu mapema kwenye Kamati juu ya hoja hii, naamini kuwa atakapofanya majumuisho, atatupa taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Mamlaka kwa kuongeza orodha ya walipa kodi wakubwa, lakini bado kuna haja ya kuangalia kuwa, je, kodi halisi inalipwa?

Tunashauri wakadiriaji wa kodi wa kitengo hiki, wawe wanapangwa kwa kushtukizwa kwani upo mwanya wa kuzoeana na walipa kodi hawa na kusababisha kupungua kwa mapato.

Mheshimiwa Spika, usumbufu katika utoaji wa mizigo, pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Mamlaka za kupunguza usumbufu katika utoaji wa mizigo katika bandari zetu hasa Dar es Salaam, bado ucheleweshaji wa kutoa mizigo haujapungua. Ipo dhana kuwa, makampuni ya kuhakiki mizigo *TISCAN* na nyenginezo, zinafanya hivyo ili kupata mapato zaidi kwa kuchelewesha mizigo.

Tunashauri suala hili liwekewe mkakati ili ufumbuzi wa kudumu upatikane. Aidha, Waziri aliahidi kulishughulikia tatizo la mizigo inayotoka Zanzibar, je, ufumbuzi umepatikana?

Mheshimiwa Spika, Msajili wa Hazina ndiye, mdhibiti mkuu wa Raslimali za Serikali, zilizoko kwenye miliki ya Serikali Kuu, Mtaa au Mashirika ya Umma, Ubia wa ndani na nje ya Nchi.

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, inaonesha kuwa Serikali ina dhamana zenye thamani ya shilingi 2,443,005,970,893/= katika makampuni na mashirika ya ndani *(National Local Organization).* Aidha, Serikali ina dhamana za kiasi cha shilingi 397,485,135,451/= katika makampuni, mashirika na asasi za kigeni. Je, mapato yake yamejitokeza katika mapato ya Serikali au ndio kama yale mapato ya *TANSORT* iliyoko London?

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi wa Serikali, kuhoji juu ya kuingizwa kwenye vitabu, rasilimali za Serikali, lakini bado rasilimali nyingi za Serikali

hazijaingizwa kwenye vitabu hivyo, tunamtaka Waziri alieleze Bunge lako Tukufu, ni Wizara, Mashirika mangapi mali zake zimekwisha hakikiwa na kuingizwa kwenye vitabu vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimetanguliza masuala haya kutokana na utaratibu wa Serikali, kuuza mali za Serikali bila ya kulishirikisha Bunge na pale inapolishirikisha huwa haisikilizi ushauri wake. Kwa mfano, *Air Tanzania, TTCL* na kadhalika, kama Wabunge wangelisikilizwa, hali ingekuwa tofauti, ambapo baada ya kuwatajirisha watu, sasa tumeachiwa uoza wetu na mzigo wa gharama zote anabebeshwa Mtanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, baada ya Sheria Na.21 ya mwaka 2004, Mamlaka ilijitahidi kuweka utaratibu wa ununuzi kwa mujibu wa sheria mpya. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Bodi katika kuratibu shughuli za manunuzi, bado Sheria ya Manunuzi haifuatwi, sio kwa kutokuijua, bali kwa makusudi. Kwa mfano, kutokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Wizara, Idara na Asasi 25 kati ya 60 zilizokaguliwa, hazikufuata masharti ya ununuzi katika kipindi cha mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, sababu kuu ni kutokuwa na mipango madhubuti juu ya manunuzi ya dharura ambayo hununuliwa bila zabuni; kutokukutana mara kwa mara na Bodi za zabuni; udhaifu katika kuweka rekodi za manunuzi, hivyo kusababisha manunuzi ya mara mbili na pengine suala la rushwa pengine limo ndani yake.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 65 ya matumizi ya Serikali yako kwenye manunuzi ambayo yanafanywa kwa njia ya zabuni. Utaratibu unaotumika kwa sasa wa kumpata mzabuni ni ule ambao una mahusiano ya moja kwa moja na mzabuni, jambo ambalo linasababisha kuwepo kwa mianya ya rushwa na udanganyifu katika kutoa zabuni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikikosa mapato kutokana na yenyewe kutokuheshimu Sheria ya Manunuzi *(Procurement Act)*, hivyo kuingilia Taasisi ya Zabuni bila ya kufuata utaratibu. Ipo mifano mingi. Zabuni ya vitambulisho vya uraia, zabuni ya mchele kutoka Japan, zabuni ya kuweka mtandao Serikali za Mitaa, Kampuni iliyoshinda ni Micronix, lakini ilienguliwa na nyingine nyingi. Baadhi ya waathirika huamua kwenda Mahakamani, hatimaye Serikali wakati mwingine hulazimika kulipa fidia na gharama za Mahakama.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, inaonyesha kiasi cha Shilingi milioni 210 alicholipwa mzabuni kwa ajili ya ununuzi wa magari na pikipiki, lakini mpaka sasa mzabuni huyo hakuwahi kuleta magari na pikipiki wala hakurejesha fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba zetu za miaka ya nyuma tulishauri Serikali kupitia Bodi ya Zabuni kuanzisha utaratibu wa zabuni kwa njia ya Mtandao *(Electronic Procurement)*, utaratibu ambao unatumika sana katika nchi za wenzetu na ni utaratibu ulio na uwazi katika uendeshaji, unatoa mwanya kwa mzalishaji wa kweli *(manufacturer)* kuuza bidhaa zake. Teknolojia hii inapunguza sana uwezekano wa

Serikali kufanya biashara na matapeli kama wale waliochukua fedha za walipakodi, lakini wakashindwa kuwasilisha bidhaa.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako hili kwa kupitia Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali, ilishauri Serikali itumie utaratibu wa *Electronic Procurement,* ambao utapunguza urasimu, utapunguza rushwa, utatoa ushindani wa wazi, hivyo kuongeza ufanisi, utaipunguzia gharama ya manunuzi Serikali sio chini ya asilimia 15 ya manunuzi, hivyo kuiongezea uwezo Serikali wa kutoa huduma zaidi na kupunguza Bajeti tegemezi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kutumia njia hii, Serikali ingeliweza kupunguza kwa kiwango kikubwa matumizi yasiyoipatia faida Serikali *(Nugatory Expenditure),* kwenye zabuni, kwani inahusisha vikao visivyoisha vya kupitisha zabuni ambavyo kama tulivyoona katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuwa, vikao vingi vya Bodi ya Zabuni havikai, hivyo kusababisha uvunjwaji wa Sheria ya Manunuzi.

Mheshimiwa Spika, tunapendekeza kwa mara nyingine tena utaratibu huu wa *E-Procurement* uanze kutumika, hasa tukitilia maanani kuwa, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka anaufahamu vizuri na Serikali sasa imeanza kuingia katika *E –Government.*

Mheshimiwa Spika, naomba kuupongeza Uongozi wa Benki Kuu kwa kufanya utafiti wa kina juu ya Taarifa ya Uwekezaji kutoka Nje ya Tanzania *(Tanzania Investment Report On Foreign Private Investment 2004).* Sababu moja kubwa *BOT* kufanya utafiti huu ni kutokana na utaratibu unaotumiwa na nchi nyingi katika kuratibu na kufuatilia madeni ya nchi husika. Kwa niaba ya Serikali, Benki Kuu huitumia *Commonwealth Secretariat Debt Recording and Management System (CS-DRMS)* kuweka rekodi ya madeni yetu.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hiyo, *Chapter Four - Private Sector External Debt (PSED)* inaelezea kuwa kuna haja ya kuwa makini katika kufuatilia madeni yaliyokopwa na Makampuni binafsi kwa ajili ya uwekezaji hapa Tanzania ambayo yana asilimia 44 ya jumla ya uwekezaji kutoka nje ya nchi ambapo kutokana na ripoti hiyo, hadi mwaka 2001 ni jumla Dola za Kimarekani bilioni 1,285.7 ambapo Sekta ya Madini peke yake imekopa Dola za Kimarekani milioni.559.5.

Mheshimiwa Spika, katika ripoti hiyo pia inaeleza nchi ambazo mikopo hiyo imekopwa (Jedwali 4.7). Baada ya kulipitia, nimepata maswali ambayo nahitaji ufafanuzi:-

(a) Kutokana uchunguzi huu, thamani iliyogundulika ni Dola za Kimarekani 1,285.7 wakati takwimu s ahihi zilizoko kwenye kumbukumbu ni Dola za Kimarekani 592.9 tofauti ya Dola 504.1. Tafsiri yake ni nini? Mheshimiwa Waziri tunaomba atueleze.

(b) Jedwali 4.7 linaonyesha nchi zilizokopesha, mstari wa kwanza imeandikwa *East African Community* kiasi cha Dola

za Kimarekani milioni nane, lakini wakati huo huo chini yake kuna Kenya inaonekana milioni nane. Je, Kenya haimo katika *East African Community?*

(c) Je, kutokana na swali la kwanza, haiwezekani kuwa makampuni haya kuendelea kulipa malipo hewa na hasa ukiangalia takwimu za mauzo ya nje ya dhahabu na kiwango cha deni kinavyopungua, uwezekano huo haupo?

(d) Kwa nini, katika kitabu cha hali ya uchumi, deni la Taifa haionyeshi deni hili la Makampuni yanayowekeza Tanzania?

(e) Kama wadeni hawa hawakulipa na wameweka dhamana raslimali walizowekeza Tanzania, ikitokea hali hiyo inakuwaje?

Benki Kuu imewekeza katika sehemu mbalimbali ili kujipatia mapato ikiwemo katika Sekta ya Madini. Wakati Waziri akiwasilisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara yake mbele ya Kamati ya Fedha na Uchumi, nilimuarifu rasmi kwamba, Kambi ya Upinzani itataka kupata taarifa sahihi juu ya uwekezaji wa *BOT* katika *Mwananchi Gold Mines Ltd: -*

(a) Hisa za kila mwekezaji;
(b) Chanzo cha mitaji cha kila mwekezaji;
(c) Kama ni mikopo, tujue ilikotoka na masharti yake;
(d) Uzalishaji uliokwishafanyika na kama upo mgao wa mapato au hasara.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kuna *Buhemba Gold Mine* inayomilikiwa na *MEREMETA Ltd.* Mawaziri wakati wakijibu hoja hapa Bungeni, wametuambia kuwa Kampuni hii imefilisika na sasa iko katika hatua za mwisho za ufilisi. Kutokana na taarifa iliyochapishwa katika kitabu *"The Promise"* kilichozinduliwa hapa Bungeni, ukurasa wa 307 inaonyesha Kampuni hiyo bado inaendelea na uzalishaji na ina uwezo wa kuendelea kuzalisha kwa kipindi cha miaka minane ikitoa wastani wa *Tray oz. 80,000* ambayo *oz.1 = gram 31.103.*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa: -

(a) Usahihi wa kauli hizi za Mawaziri na usahihi wa taarifa iliyomo kitabu *"The Promise."*

(b) Benki Kuu iliwekeza kiasi gani katika mradi huu?

(c) Hazina kama Msajili Mkuu wa mali za Serikali, imepata hasara kiasi gani kutokana na kufilisika kwa kampuni hiyo kama taarifa za Mawaziri ni sahihi, au kama taarifa ya Prof. Malyamkono ni sahihi: Je, Serikali imepata gawio au hasara kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza *BOT* kwa kujenga majengo mapya ya Benki Kuu, kwa gharama yao karibu Dola za Kimarekani milioni 200. Ipo taarifa kuwa Majengo hayo yalifunguliwa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Je, ni kweli?

Mheshimiwa Spika, tumeuliza swali hilo kwani, wakati Kamati ya Fedha na Uchumi ilipotembelea imekuta majengo hayo bado yanaendelea kujengwa hadi leo hii? Je, ni nini kilichoharakisha kufunguliwa kama kweli yamekwishafunguliwa?

Mheshimiwa Spika, kutokana na wasiwasi wa Kambi ya Upinzani, naamini na Wabunge wengine, juu ya namna mradi huo ulivyotumia fedha nyingi za nchi bila ya hata Bunge lako kuarifiwa. Tunaomba Bunge lako liridhie ushauri wetu wa kuunda Kamati Maalum ya Bunge kuchunguza uwekezaji huu wa majengo ya Benki Kuu ya Tanzania, ili sisi wawakilishi wa walipakodi tujiridhishe na matumizi ya mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu za Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ya mwaka 2005 inaonesha kuwa, pato la Bima liliongezeka kutoka Shilingi bilioni 32 mwaka 1995 na kufikia Shilingi bilioni 83 mwaka 2004. Kutokana na mafanikio hayo na takwimu kutoka *Insurance Supervisory Department - Dar es Salaam* ya mwezi Agosti, 2004, inaonesha kuwa, kati ya Makampuni yote yanayojihusisha na biashara ya Bima hapa nchini, *NIC* ndiyo ilikuwa inaongoza kwa kuwa na *market share* kubwa ya asilimia 26, kitu kinachoashiria kuwa Shirika hilo linafanya biashara nzuri katika Sekta hii. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania kati ya mafanikio hayo, kiasi gani ni mchango wa Shirika la Bima la Taifa?

Mheshimiwa Spika, aidha, katika hotuba ya Waziri, inaonesha kuwa vitega uchumi katika Sekta ya Bima vimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 87 hadi Shilingi bilioni 124 katika kipindi hicho hicho. Kambi ya Upinzani inaomba kupata maelezo kati ya thamani ya vitega uchumi hivyo, *NIC* ina vitega uchumi vyenye thamani kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hiyo hiyo, Waziri alisema kuwa, Serikali imelikopesha Shirika hilo jumla ya Shilingi bilioni nne kwa ajili ya kulisaidia Shirika hilo ili kulipa wadai wake. Kupitia Vyombo vya Habari hivi karibuni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo amesikika akisema kuwa, Shirika hilo bado liko hai kiuchumi na lina uwezo wa kujiendesha kibiashara na halijawahi kupokea fedha za kujiendesha kutoka Serikalini. Tunaichukulia taarifa hii ya habari ni sahihi, kwani Serikali mpaka leo haijakanusha.

Mheshimiwa Spika, kujiendesha maana yake ni kuwa na uwezo wa kulipa wadai na kuwalipa wafanyakazi wake mishahara kwa mujibu wa sheria. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo ukweli hapa uko wapi. Au inajengwa hoja ya kuhalalisha kuligawa bure kwa kisingizio kuwa halina uwezo wa kujiendesha?

Mheshimiwa Spika, suala la watumishi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, limekuwa kama donda ndugu. Katika hotuba ya Waziri kwa mwaka 2005

aliliambia Bunge kuwa bado Wizara ilikuwa inafanya zoezi la kukokotoa mahesabu ya wazee hao ili malipo yao kulingana na stahili zao yafanyike.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa zilizopo, mpaka sasa ni kwamba, Wastaafu ambao hawajalipwa hata senti moja ni 326; Wasimamizi wa mirathi ambao hawajalipwa ni 189; Waliopata mafao sifuri ila fedha ya usafiri tu ni 918; ambao wamelipwa kwa mapunjo mbalimbali ni 1,519 na waliopigiwa hesabu za mafao kwa Shilingi ya Tanzania ya mwaka 1977 badala ya 2005/2006 ni takriban 277.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa wastaafu, ulimalizika kwa maamuzi ya pamoja nje ya Mahakama baada ya wastaafu kufungua madai yao Mahakamani *(Civil Case No. 95 ya 2003).* Tunapenda kuuliza hapa, ni kitu gani kimeshindikana kutekeleza maamuzi haya ya Mahakama hasa kifungu cha 11 kinachozungumzia *Real Value* na kifungu cha 12 kinachozungumzia suala la *Compound Interest?*

Mheshimiwa Spika, tunamshauri Waziri, alimalize suala hili kwa kuzingatia maamuzi ya Mahakama na ili hili liwe rahisi kulitekeleza. Ni vyema Waziri akakutana na Mawakili wa Wastaafu na Kiongozi mmoja katika kila kundi ili kumaliza madai yao.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha *(Joint Finance Commission - JFC)* ni Asasi ya Muungano iliyoundwa kwa mujibu wa ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha Na.14 ya mwaka 1996.

Mheshimiwa Spika, suala hili kila Bunge la Bajeti, huibuka kutokana na kuchelewa kwa kipindi cha miaka isiyopungua 40. Kutokutekelezwa ibara hii ya Katiba pamoja na Sheria ya iliyoanzisha Tume, kumechangia kwa kiwango kikubwa kuzorota kwa utekelezaji wa shughuli za Muungano hadi kusababisha kuwa na manung'uniko kila upande wa Jamuhuri.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge hili, ni lini kazi ya Tume hii itaanza kufanya kazi kwa maana ya kuwa na *formula* ya mchango wa mapato na matumizi ya Muungano kwa kila upande wa Jamhuri. Tumechoka kupewa ahadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi ulitupatia fursa ya kupata Semina juu ya UKIMWI na athari zake. Tunakushukuru sana. Jambo ambalo sote Wabunge tulishuhudia juzi ni namna vijana wetu wanavyozidi kuathirika kwa UKIMWI na kujiingiza katika masuala ya kujamiiana mapema, kunakochangiwa kwa kiasi kikubwa na magazeti yanayoonyesha waziwazi sehemu za siri za wanawake, filamu na mitandao ya ngono. Kwa kuwa zipo sheria zinazoweza kukabiliana na hali hii, tunaiomba Serikali itoe amri ya kupiga marufuku, uuzwaji wa hadharani na siri wa picha za ngono, ama kwenye vijarida, magazeti au hata kaseti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tena upokee shukrani zetu za dhati kwa namna ulivyoliongoza Bunge hili la Bajeti kwa mara ya kwanza tokea uchaguliwe kuwa Spika.

Aidha, wasaidizi wako wakiongozwa na Naibu Spika, Wenyeviti na Watendaji wa Ofisi ya Katibu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani za pekee ziwaendee, vijana wetu *(page boys)* wanaotuhudumia humu Bungeni, sijui kwa siku wanatembea kilomita ngapi, lakini hawachoki wala hawakimwi. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, ninao wachangiaji tisa hadi sasa na kwa hesabu zangu, nadhani ndio wanatosha, kwa maana ya leo. Kesho wataongea wawili, halafu nitawaita Manaibu Waziri na Mheshimiwa Waziri Mtoa hoja atamalizia.

Nitasoma majina ili mfahamu. Wa kwanza ni Mheshimiwa Gaudence Kayombo, ambaye amechangia mara moja tu tangu tumeanza Mkutano huu. Kwa hiyo, ana haki ya kwanza kabisa na ndiye atakayeanza. Wanafuata waliochangia mara mbili ambao ni Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula na Mheshimiwa Yono Kevela.

Waliochangia mara tatu ni Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Lucas Selelii. Waliochangia mara nne ni Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi na Profesa Raphael Mwalyosi. Sikupata takwimu, Mheshimiwa Dr. Chegeni amechangia mara ngapi, lakini yuko kwenye orodha. Kwa hiyo, basi tutaanza na Mheshimiwa Gaudence Kayombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Paschal Degera.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kutangaza tu uwepo wa wanafunzi 20 kutoka *Meriwa English Medium Primary School, Dodoma* na Walimu wao wanne, naomba msimame. Ahsanteni, karibuni sana Walimu na watoto, hapa ndiyo Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wa Ilala, Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga yeye ni wa Jimbo la Ukonga, lakini Wilaya ni ya Ilala na Mheshimiwa Azzan Zungu wanao wageni ambao ni Wajumbe wa Baraza la Vijana wa CCM Wilaya ya Ilala ambao ni Deus Daffi, Athumani Magembe, Athumani Mohammed, Halima Salum, Happy Kayombo na Mohamed Besta. Wale pale upande wa kushoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed anao wageni wake, nao ni Viongozi wa Wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wageni hao ni Bwana Alfred Kinyondo, yule pale amekaa Speaker's Gallery na Bwana Jones Musokwa, hao hapo. Ahsante sana.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bajeti hii siku ya leo. Lakini pia naomba nimpongeze Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mama Zakia Meghji, Manaibu wake pamoja na wataalam wote katika Wizara ya Fedha kwa umahiri wao. Umahiri wao

unadhihirika zaidi pale ambapo wameamua kuchukua mengi ya mapendekezo ya Kamati ya Fedha ambayo mimi pia nimebahatika kuwa Mjumbe wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umahiri huo katika hali ya kawaida, pengine nisingelazimika kuchangia, lakini naomba nichangie kwa sababu kuna mambo mawili/matatu ambayo naona ni ya msingi na yanawahusu sana wapigakura wa Jimbo la Mbinga Mashariki.

Kwanza ni suala la mishahara ambalo limezungumziwa humu katika ukurasa wa 30 na Waziri anaahidi kushughulikia wale wafanyakazi ambao wanakaa mbali na Makao Makuu ya Wilaya ambako ndiko mishahara inafikishwa katika Benki na Benki nyingi zinaishia hapo katika Makao Makuu ya Wilaya. Hii programu ya kupitisha mishahara ya wafanyakazi wote Benki ina miaka kama miwili au mitatu hivi na ilianzishwa katika Serikali ya Awamu ya Tatu, Serikali ambayo ilikuwa inafahamika kwamba kulikuwa na Askari wa Miamvuli.

Kwa hiyo, kulikuwa na Mawaziri wazuri, wafanyakazi wazuri na Watendaji wazuri ambao wakati ule walipokuwa wanaanzisha hiyo *project* bila shaka walijua kabisa mtandao wa Benki unaishia wapi na kwa hiyo, ilikuwa ni rahisi tu bila kupiga hesabu kali kuona kwamba kuna wafanyakazi ambao bado hawatapata huduma hiyo kiurahisi. Kwa sababu suala hili tumelizungumzia mara nyingi toka tumeanza Bunge hili la *speed and standards*, nilitarajia Wizara angalau badala tu ya kusema Wizara itaangalia uwezekano wa kusogeza karibu, ingekuja na *statement* ambayo ni *more quantifiable* na *workable* ili kuona kwamba wafanyakazi wote wanapata ule mshahara ambao umetangazwa na Serikali ambao mfanyakazi ameambiwa na mwajiri wake kwamba ataupata.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wafanyakazi wenzetu wengine na hasa wa kule Jimbo la Mbinga Mashariki hawapati mishahara wanayostahili kupata. Mtu anaambiwa atapata Sh.80,000/= au Sh.100,000/= au Sh.60,000/= lakini hapati mshahara huo kwa sababu analazimika kwanza kutoka katika kituo cha kazi na kuufuata mshahara huo Mbinga Mjini katika Benki ya *NMB*. Kwa hiyo, anatumia nauli. Katika *any point* katika Jimbo langu huwezi kutumia chini ya Sh.5,000/=.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unahesabu Sh.5,000/= imeondoka. Lakini pia hawezi kurudi, ni lazima atalala. Atalala kwenye nyumba ya wageni Sh.5,000/= itaondoka, lakini pia atakula. Kwa hiyo, pengine Sh.30,000/= anazitumia katika biashara hiyo tu.

Mheshimiwa Spika, hili lingeweza kuonekana wazi kabisa wakati tunaanzisha utaratibu wa kuwalipa watumishi wote katika Benki kwa sababu hata kabla ya hapo utaratibu wao haukuwa mzuri, walikuwa wanapata shida hii. Sasa sielewi kwa nini jambo hili halikuangaliwa mpaka leo tuambiwe kwamba tutaangalia. Nafikiri *that's not good enough,* tulitakiwa tupate mikakati mizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninafahamu, lakini Mheshimiwa Waziri anaweza kunisahihisha katika hili, kwamba zoezi la kulipia mishahara ya watumishi kupitia Benki limeisaidia Serikali kwa sababu inawalipa wale wafanyakazi ambao kweli wameajiriwa na wale wafanyakazi hewa wengi wameondolewa kwa mtindo huu. Kwa hiyo, kuna *savings*. Kwa nini Serikali isifikirie kuwapa zaidi kwa maana ya nauli na malazi hawa wafanyakazi ambao wanalazimika kufuata mishahara yao katika hizi Benki ambazo tumeambiwa wakachukue? Ni *irresponsibility* ambayo Serikali ni lazima ikubali.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi ku-*take* tu *for granted* kwa sababu wao ni wafanyakazi, tukawafanyia tunavyotaka na hasa tukizingatia kwamba Serikali hii ya Awamu ya Nne inayosema "Maisha bora kwa kila Mtanzania" na inayosisitiza sana juu ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, utawala bora ni pamoja na kuhakikisha kwamba mfanyakazi anapata mshahara mahali alipo *very conveniently* kama ambavyo sisi wengine tunapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu mishahara hiyo ni kwamba, kwa wale ambao wanapitisha mishahara yao Benki, *NMB* inajitahidi kufanya kazi yake vizuri, lakini imezidiwa, inahitaji msaada zaidi. Hapo ndiyo ningeomba Wizara pia ijaribu kuangalia kwa sababu huduma za *NMB* zinaathirika kwa sababu ya kuwalipa wafanyakazi wote katika tarehe zinazofanana. Kwa hiyo, wateja wengine wana-*suffer*.

Mheshimiwa Spika, kwanza wale ambao wanakuja kuchukua mshahara wanatakiwa kupanga foleni na kuchukua muda mwingi sana. Lakini pia wale wateja wengine wa kawaida na wenyewe wanapata shida. Kwa hiyo, nafikiri pia Serikali ingeweza kuwasaidia hawa jamaa wa *NMB* pamoja na kwamba wanawalipa hela, lakini nafikiri ni wajibu wetu kuangalia kwamba hawa wafanyakazi wanaipata hela hii vizuri zaidi kwani wengine wanaweza wakaibiwa katika ule msururu wa foleni pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la *Payment System* katika nchi yetu. Wizara hii inafanya juhudi kubwa ya kukuza uchumi wetu. Uchumi ni pamoja na kuangalia zile *instruments* za fedha zinatumika zaidi kuliko *cash* yenyewe. Wakati tumepata msamaha wa magari yetu, tulitakiwa kulipia *VAT.* Kwa hiyo, unatakiwa uchukue milioni kadhaa mfukoni kuzipeleka *TRA* na wafanyabiashara wengine na wenyewe walilazimika kufanya hivyo.

Kwa hiyo, unashtukia unatembea na manoti mengi ya kupeleka *TRA* na unaweza kukuta kwa sababu moja au nyingine uende halafu urudi nazo nyumbani, uje nazo tena kesho ukihangaika kuzipeleka *TRA*. Kwa hiyo, nafikiri pengine Wizara ingefanya juhudi za makusudi kupitia vyombo vyake kuhakikisha kwamba *instruments* za fedha ambazo zipo kama *cheque system*, sasa zinaanza kutiliwa mkazo ili kadri maendeleo yetu yanavyokuja juu tunaanza kutumia *instruments* za fedha kuliko fedha yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuongelea juu ya *Pension Funds.* Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 37 amezungumzia juu ya ujenzi wa nyumba za *PPF* kule Mwanza. *PPF* ni Chombo cha Kitaifa na mimi pia nilikuwa mchangiaji wa huko *PPF*.

Wakati ambapo Mheshimiwa Rais ameishatuongoza tuangalie Mikoa ile ambayo haijaendelea na inafahamika kwa majina, pengine ingekuwa ni wakati huu mzuri kuhakikisha kwamba hivi Vyombo vya *Pensions* sasa pia vinaanza kuwekeza katika Mikoa hii ili kuinua uchumi wa Mikoa hiyo kwa makusudi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa napenda kutoa mfano. Wakati *NBC* alipokuwepo Marehemu Nsekela kama Mkurugenzi Mtendaji, alikuwa ana kitu kinaitwa *The frontline banking.* Maana yake ni kuwa, Benki inaanza kwenda halafu maendeleo yanakuja baadaye. Wote ni mashahidi kwamba ukienda katika Wilaya, majengo mazuri mengi ni yale ambayo yalikuwa ya Benki ya *NBC*. Hivyo ndiyo tunavyopaswa kufanya katika hivi Vyombo vya Pensheni kuhakikisha kwamba vinasaidia maendeleo katika Mikoa hii ambayo imetajwa kwamba iko nyuma kuliko Mikoa mingine ikiwemo na Ruvuma na likiwemo Jimbo langu la Mbinga Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunao uwezo, viwanja vipo na nilishamwambia Mkurugenzi Mtendaji wa *PPF* kwamba viwanja vipo kuliko huko Mjini ambako wanakwenda wanapata shida ya viwanja na wananunua kwa bei ghali sana. Lakini pia gharama za ujenzi katika sehemu hizi ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, wakulima wa kule wanao uwezo wa kununua nyumba hizo kama wakizijenga, lakini pia hata wafanyakazi wanaotoka Mikoa hiyo wanao uwezo huo. Nafikiri hii ni *social responsibility,* siyo lazima tuangalie tu Mwanza, Dar es Salaam na Arusha, lakini pia tunaweza tukaangalia sehemu hizi ili kuleta uwiano kwa sababu wachangiaji wa Mifuko hii hawatoki sehemu hizo peke yake, kwa nini keki hii iende sehemu moja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala mengi ya Kitaifa nimechangia wakati nachangia katika Kamati ya Fedha na Uchumi. Niliona ni afadhali nichangie kuhusu Jimbo langu la Mbinga Mashariki katika masuala haya matatu na ninafikiri Mheshimiwa Waziri ataangalia kuona kwamba wapigakura wa Jimbo la Mbinga Mashariki hawagharamiki katika kufuata mishahara yao kwa sababu ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba mtu anapata mshahara ule ambao amehakikishiwa atapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba hii muhimu ya Waziri wa Fedha.

Awali ya yote, napenda nimpongeze sana Waziri kwa hotuba yake nzuri sana ambayo imeeleza mambo kinaganaga. Aidha, napenda kuwapongeza Waziri mwenyewe, Manaibu Waziri wake wawili, Katibu Mkuu na Watendaji wengine kwa kazi nzuri ambayo wanafanya kwa manufaa ya Taifa letu. *(Makofi)*

Pia, nisije nikawasahau watu wa *TRA* ambao ndio wanatufanya leo tusimame hapa na kuzungumza juu ya Bajeti hii. Kwa hiyo, napenda nimpongeze sana Mtendaji wao Mkuu pia na Watendaji wengine kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Kwa kweli kiwango cha makusanyo ya mapato ya Serikali kinaongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa hiyo, napenda niwapongeze sana na kuwashukuru kwa kazi nzuri ambayo wamefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hizo pongezi, nami naomba nichangie maeneo machache tu ya hotuba ya Waziri. Sitakwenda moja kwa moja kwenye hotuba ambayo ameitoa, nitachangia juu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Kazi ambayo imepewa Wizara hii ni kukusanya mapato ya Serikali na kugawa mapato haya kwa Wizara mbalimbali, Idara, Taasisi na pia hata Halmashauri zetu. Ndiyo kazi ambayo imepewa. Sasa katika kutekeleza kazi hii, naona kuna dosari chache ambazo ningependa nizizungumze hapa ili Waziri na wataalam wake waweze kuziondoa.

Jambo la kwanza ni suala la kuchelewesha kutoa fedha kwa Taasisi mbalimbali zikiwemo Wizara, Idara, Taasisi ambazo zinajitegemea na Halmashauri zetu. Napenda niseme tu kwamba, kwa upande wa matumizi ya kawaida, Wizara inajitahidi sana kutuma pesa kwa wakati, lakini tatizo lipo kwenye fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tukiwa tunachambua utekelezaji wa Wizara mbalimbali, imebainika kwamba Wizara nyingi wanapewa pesa robo mwaka ya mwisho ya kipindi cha mwaka wa fedha ama mwaka wa Serikali na hasa fedha nyingi zinatoka mwezi wa tano.

Mheshimiwa Spika, ninavyoelewa mimi, Wizara hii inawajibika kutoa fedha kila robo mwaka kwa ajili ya miradi mbalimbali ambayo imepitishwa na Bunge lako Tukufu, ili miradi hiyo iweze kutekelezwa hatua kwa hatua na ifikapo mwezi Juni, miradi hiyo iwe imekamilika. Lakini tofauti na hayo ni kwamba, Wizara hii inahodhi fedha. Siamini kwamba hizi fedha zinakusanywa *quarter* ya mwisho zote, inahodhi fedha mpaka robo ya mwisho kabisa ya nne ndiyo fedha nyingi zinatokea katika Wizara zote na hasa mimi katika Halmashauri yangu mara nyingi naona fedha zinaletwa dakika za mwisho. *(Makofi)*

Lakini sasa tunachoangalia, pia Serikali Kuu inalaumu sana utendaji wa Halmashauri zetu na hasa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo inagharamiwa na ruzuku ya Serikali Kuu. Utakuta Serikali Kuu inalalamika kwamba Halmashauri zimeshindwa kutekeleza miradi yao kwa sababu labda hawana *capacity* ya kutekeleza lakini sio kweli. Ukweli ni kwamba, fedha zinakuja dakika za mwisho au mwisho wa mwaka na hivyo fedha zinalimbikizwa katika robo ya mwisho ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba sana, ili tuwe na utendaji mzuri wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, fedha zitumwe kwa wakati ili Halmashauri, Wizara, Idara na Taasisi ziweze kuweka mpango mzuri wa kutekeleza miradi kwa taratibu zinazotakiwa. Kwa hiyo, naomba sana Wizara itoe fedha za maendeleo kila robo mwaka ili tuweze kuweka mipango mizuri ya kutekeleza miradi yetu ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba nigusie suala la utoaji au kutokutoa fedha kabisa. Imedhihirika kwamba, baadhi ya fedha ambazo zinapitishwa na Bunge lako Tukufu, huwa hazitolewi kabisa. Tatizo lipo kubwa. Nisingependa nitoe kwa ujumla, lakini nataka nichukue mfano mmoja tu nielezee kwa Wilaya/Halmashauri yangu ya Kondoa.

Katika Wilaya ya Kondoa, tuna mradi mkubwa wa maji unaitwa Mradi wa Ntomoko. Mradi huu uliasisiwa na Baba wa Taifa miaka ya 1970. Kiutaratibu ni kwamba, mradi huu huwa unatengewa fedha kila mwaka takribani Shilingi milioni 20 hadi 30 ili kuweza kuhudumia ule mtaro uweze kufanya kazi na kuweza kutoa huduma ya maji kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru Mawaziri wa Maji waliopita akiwemo Waziri Mkuu wa sasa, Mheshimiwa Edward Lowassa. Yeye alihakikisha kwamba kila mwaka mtaro huu unapatiwa fedha za ukarabati kwa sababu mradi huu ni muhimu na unahudumia watu wengi. *(Makofi)*

Napenda kusema kwamba, mradi huu unahudumia vijiji 18 na kwa kweli unahudumia wananchi zaidi ya 50,000. Kwa hiyo, kila mwaka tunawajibika kupewa fedha za kuweza kutoa huduma hiyo. Nasikitika sana kwamba, mwaka wa fedha 2005/2006 hatukupata hata senti tano. Matokeo yake ni nini? Mimi nimefuatilia sana Wizara ya Maji, wamenihakikishia kwamba Wizara ya Fedha mwaka huo wa Fedha 2005 haikutoa hata senti tano kwenda Wizara ya Maji. Kutokana na hilo na wenyewe wameshindwa kutupa fedha. Lakini athari/matokeo yake ni nini? Matokeo yake ni kwamba ule mradi sasa hivi umevurugika kabisa. Katika vijiji 18 ambavyo vinahudumiwa na mradi huo, kijiji kimoja tu ndiyo kinapata maji sasa hivi. Kwa hiyo, vijiji 17 havina maji kabisa.

Mheshimiwa Spika, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Waziri wa Fedha umuhimu wa mradi huo. Ni kwamba, mradi huo unahudumia watu 50,000 kama nilivyosema na hakuna vyanzo vingine vya maji, hakuna chemchem, tumeshindwa kuchimba visima virefu, kwa hiyo, wote wanategemea mtaro huo.

Sasa kama Wizara haitoi fedha kwa mradi muhimu kama huo, mimi sielewi tunafanyaje. Lakini ukweli wenyewe ni kwamba, hivi sasa watu wanahangaika kweli kweli. Wengine wanakwenda mpaka Mjini Kondoa kwenye chemchem kuchota maji kwa maana ya kwamba wanapanda mabasi kufuata maji Mjini kilomita kama 30 ama 40 hivi. Wengine wanatembea kwa mguu mpaka Kata za jirani kwenda kuchota maji.

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa tunaomba kura, tulisema kwamba tutaboresha huduma ya maji kwa nchi nzima. Tumekuwa na chanzo hicho, lakini mimi siwezi kusema ni uzembe, labda kutokuwa na uzoefu. Naona watu walifikiri kwamba mtaro wa Ntomoko ni mtaro tu ambao unapitisha maji. Unahitaji ukarabati wa kila mwaka.

Nimewasiliana na Wizara ya Maji, wamenihakikishia kwamba hawajapewa fedha za mtaro wa Ntomoko Shilingi milioni 30 za mwaka 2005. Nimewasiliana na

Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, wamenihakikishia mpaka sasa hawajapata fedha. Sasa mimi nashindwa kurudi Jimboni kwangu, watu 50,000 wakija nyumbani kwangu kutafuta maji sijui nitawapa jibu gani.

Mheshimiwa Spika, sitaki kurefusha historia iwe ndefu, lakini nilitaka kuelezea umuhimu wa mtaro huo. Sasa naomba basi, Mheshimiwa Waziri, naomba popote ambapo kuna fedha naomba atupatie Shilingi milioni 30, tukarabati ili angalau watu waweze kupata huduma hiyo ya maji kwa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kuhusu mradi huu, napenda niishukuru sana Serikali. Hivi sasa mradi huu umewekwa katika ule mradi wa Benki ya Dunia wa Maji na Mazingira Vijijini. Mwaka huu tumetengewa Shilingi milioni 100 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, nafikiri ili mradi uweze kukarabatiwa kwa kiwango kikubwa. Lakini wakati tunangoja ukarabati huo, tunaomba tupewe Shilingi milioni 30 angalau wananchi waweze kuendeleza kupata huduma ya maji wakati tunasubiri ukarabati mkubwa.

Kwa hiyo, kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Kondoa Kusini na hasa hasa wale walengwa wa mradi huu, napenda nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kitendo ambacho wamechukua, ni mradi muhimu ndio maana wametenga fedha na kuanzisha mradi maalum wa kuweza kukarabati mradi wa Ntomoko. *(Makofi)*

Kwa hiyo, napenda niwashukuru, lakini naomba haraka iwezekanavyo tupatiwe fedha kwa sababu vinginevyo wananchi hawa watataabika sana kwa sababu fedha za mwaka 2005 hatukupata. Kwa hiyo, tunaomba zile za mwaka jana kwa sababu ilikuwa ni haki yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hiyo kero ya Jimbo langu, sasa naomba niongezee jambo moja. Kuna wastaafu wengi sana wanalalamika sana kuhusu malipo yao ama stahili zao za *pension* na hasa wale wa kiwango cha chini *(Minimum pension)* wako hata leo wanazunguka hapa kujaribu kutafuta namna gani wasaidiwe ili wapate haki zao. Lakini sijui, kwa sababu Mawaziri wapo hapa na Katibu Mkuu, Watendaji wako hapa, kwa nini hawawasaidii?

Mheshimiwa Spika, Wapo hapa wana makaratasi yao na maelezo yao, mimi nitawawakilisha niwape yale malalamiko kwa niaba ya wenzao hasa hawa waliokuja hapa kulalamika, ni wale wa Mkoa wa Dodoma kwa niaba ya wenzao wa Tanzania nzima. Naomba kwa wakati muafaka, nimpe Waziri karatasi za malalamiko ya hawa wastaafu aziangalie na kama wana haki ya kulipwa, basi achukue hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache naomba tena nikushukuru na naomba nitamke kwamba naunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha, lakini naomba hizo fedha Shilingi milioni 30 za mtaro wa Ntomoko tupewe mapema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii. Awali ya yote, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji katika Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii na hatimaye tunaijadili katika Kikao cha leo.

Aidha, napenda kutoa shukrani pia kwa Mheshimiwa Waziri Zakia Meghji, pamoja na Gavana Msaidizi Mr. Leli kwa sababu tuliwasiliana nao hasa katika tatizo la ukosefu wa Benki Wilayani Bukombe na hatimaye sasa kwa taarifa zilizo rasmi *NMB* wamekwenda Bukomba na wanatafuta nyumba na kiwanja ili waweze kufungua Benki pale. Kwa hiyo, niendelee kuomba pia kwamba, waendelee kuwasiliana na Benki nyingi hata na *CRDB* kwa sababu tumesikia hata fedha tunazokwenda kukopesha wananchi wetu zinapitia aidha katika *NMB* au *CRDB* na wao pia wasogee katika Jimbo la Bukombe, ili turahisishe shida ya upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

Baada ya hapo, pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa tamko lake alilolitoa tarehe 2 Agosti, 2006 hapa Bungeni la kuhusiana na wastaafu hasa wanaodai mirathi yao. Nakumbuka alisema kwamba Wabunge twende kule tukaorodheshe wale wanaodai mirathi na hatimaye tuilete Serikalini. Mimi naamini kwamba ni uamuzi mzuri na sisi hii kazi tutaifanya, tuombe Serikali iwe tayari kupokea majina hayo na kuyafanyia kazi kama alivyosema Mheshimiwa Degera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nami nichangie yale niliyokusudia kuyasema katika siku ya leo na hasa yanayolenga katika Jimbo la Bukombe na maeneo mengine, pengine kama matatizo yale yatakuwa yanafanana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kuongelea juu ya tatizo la *OC,* mtiririko wa *Other Charges* kutoka Hazina kwenda kwenye Halmashauri zetu. Pamekuwepo na tatizo ambalo mimi nimelibaini hasa katika Kikao cha Kamati ya Fedha Wilayani kwangu nilipohudhuria Julai mwaka huu, nikaona kwamba fedha hizi haziendi kama vile Bajeti ilivyoidhinishwa. Kwa mfano katika Wilaya ya Bukombe mwaka huu, *OC* tulikuwa tumeidhinishiwa Shilingi bilioni 1,647,457,200/= lakini fedha tulizopewa ni Shilingi bilioni 1.2 tukabaki tunadai Shilingi milioni milioni 439,583,800.

Kwa hiyo, tulipokuwa ndani ya Kikao, nikamwuliza Mkurugenzi, hii Bajeti iliidhinishwa, hizi fedha ambazo hazijafika hatma yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, labda kupitia Mjadala huu wa Wizara ya Fedha, wanaweza wakatusaidia kwamba, fedha hizi mimi ninachoamini ni kwamba, tumepisha fedha mbalimbali katika Wizara mbalimbali, lakini hata katika Halmashauri zetu tunapitisha. Matokeo, fedha yote haiji kama tulivyopitisha. Tulipofanya Bajeti au *proposal* tulikusudia kwamba kazi yetu tutafanya kulingana na fedha hii. Inaposhindwa kuja fedha yote, hatupati pengine majibu, hatma majibu yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, naona pengine labda tufahamishwe au niambiwe kwa Bukombe, Sh. 439,583,800/= zilizobaki katika *OC* zinazolenga katika Idara ya Kilimo, Elimu, Afya, Barabara na Maji: Je, hizo fedha tutazipata au kwa sababu muda wa Bajeti

umepita, hizo fedha hazipatikani tena? Hilo nilitaka niulize na nilitaka nilichangie katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia Wilayani Bukombe tunalo tatizo. Nakumbuka kuna barua ambayo iliandikwa tarehe 21 Juni, 2004 yenye Kumb.Na.F20/1/2/115 ikiomba mapunjo, inasema: "Maombi ya kulipwa mapunjo ya fedha za mishahara mwezi Aprili na Mei." Barua nyingine iliandikwa kwa Katibu Mkuu Hazina na barua nyingine iliyoandikwa tarehe 2 Julai, 2004 yenye Kumb. Na. F20/11/2/1118 ikienda kwa Katibu Mkuu ikisema: "Fedha za mishahara ya mwezi Juni ya watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe kuletwa pungufu kwa Tshs. 23,111,633/=."

Mheshimiwa Spika, hizi barua ziliandikwa kwenda Hazina. Hazina wakati wanapeleka fedha za mishahara hii ya Walimu pamoja na watumishi mbalimbali, zilikwenda pungufu na ndio maana hizi barua ziliandikwa kwa nyakati tofauti kwa sababu mwezi Aprili, Mei na Juni, fedha zilikwenda pungufu kwa jumla ya Sh.37,467,994.65. Hazina hawajatoa jibu. Lakini pia kwa hali hii watumishi wetu unakuta wakati mwingine tunawaingiza hata katika matatizo yasiyostahili kwa sababu kama fedha haijafika, unategemea hawa watumishi si tunawaingiza katika *temptation* za kufanya mambo maovu?

Mheshimiwa Spika, naomba basi kunapokuwa pengine na matatizo, pawepo na mawasiliano mazuri kati ya Hazina na Halmashauri zetu ili tuweze kujua. Lakini pia niweze kuambiwa hatma ya hizi hela ni nini, hii mishahara tunayodai ambayo ilikuwa ni pungufu na barua zilishakwenda hazina toka mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, pia nichangie kuhusiana na watumishi wanaopata ulemavu wakiwa kazini. Katika Wilaya ya Bukombe, wako watumishi ambao waliajiriwa ndani ya Serikali yetu lakini pengine wakapata ulemavu wakiwa kazini. Mfano, ninaye mzee mmoja anaitwa Mzee John Nuhu, aliajiriwa mwaka 1971, lakini mwaka 2003 akapata upofu, akapofuka yule mzee. Sasa ni wa kushika mkono akitaka kwenda kuoga anashikwa mkono na mke wake, kwenda Kanisani hivyo hivyo. Hafanyi lolote sasa.

Tarehe 17 Februari, 2005 ilibidi astaafishwe kwa sababu sana hakuna chochote anachokifanya katika Serikali yetu. Tarehe 18 Februari alipata mafao yake ya Shilingi milioni 1,400,000/=. Sasa nilipokuwa najaribu kuongea naye nikiwa nawaza, huyu Mzee ambaye sasa amekuwa kilema hawezi akafanya biashara, hawezi akafanya shughuli yoyote, fedha alizopata ni Shilingi milioni 1.4 ni mwanzo na mwisho. Sasa sijui hatma ya watu hawa ni nini! Inawezekana nasema Bukombe, lakini pengine maeneo mengine wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wazo langu na ushauri wangu, nilikuwa naomba Serikali ikiwezekana iangalie utaratibu wa watu hawa wanaopata ulemavu katika utumishi. Pengine wawe wanapata kitu fulani kwa mwezi ambacho kitamfanya aweze kuendelea kuishi na hatimaye kurefusha maisha yake. Vinginevyo, mtu huyu atakula hii Sh.1,400,000/= ndani ya miezi mitatu au miwili kwa sababu yuko kijijini na hatimaye anakufa. Naomba tuliangalie hili na hatimaye tuweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii, kuna kipengele ambacho mapendekezo yalitolewa na Kamati na mimi ninayaafiki kabisa. Walisema kwamba, Kamati za Bunge zipate muda wa kutosha kuchambua Bajeti. Mimi mtazamo wangu ulikuwa tofauti kweli na kwa sababu ni mara ya kwanza kuingia Bungeni, nilianza kupata shida mara ya kwanza nilipoambiwa tunakwenda kupitia Bajeti Dar es Saalam, mimi nikafikiri kwamba tukifika pale ninao uwezo wa kusema *point* ambayo niliitaja iingie pengine katika Bajeti ile na pengine hata swali langu nililojibiwa, mimi nilijua pengine tutakwenda tukaliongee kule kwenye Bajeti watoe kipaumbele kadri jinsi Mbunge anavyoona nini kinahitajika kifanyike.

Lakini kumbe Bajeti zinakuwa zimeshapitishwa. Kwa hiyo, inakuwa kama *formality* tunayofanya. Mimi niiombe tupitie kwenye *draft* ili tuweze na sisi ku-*comment* nini kinatakiwa kifanyike kabla ya kupitisha kwenye vitabu hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, lakini pia nipewe majibu ya hatima ya fedha zetu ambazo zimekuja pungufu katika *OC* na hatima ya mishahara tuliyokuwa tunadai kwenye barua nilizozitaja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Fedha. Vile vile, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Fedha na Manaibu Mawaziri kwa jinsi wanavyochapa kazi na jinsi hotuba ilivyokuwa imeeleweka na imekamilika.

Lakini pamoja na hayo, nishukuru vile vile Wabunge wenzangu ambao wamechangia hii hotuba kwa ufanisi mkubwa kwa sababu, sasa hivi nina hofu kwamba inawezekana nikawa nazungumza kitu ambacho pengine wenzangu tayari wameshakizungumza. Lakini sasa inatakiwa tuzungumze kwa sababu tupate nafasi. Lakini vitu ambavyo vinanikera mimi viko upande wa haya malipo ya wastaafu. Haya malipo ya wastaafu kwa kweli wanapata shida sana hasa wale wa *(East Africa Community),* iliyokuwa Afrika Mashariki, hawa watu bado wanateseka sana.

Nina mfano hai kutoka Jimboni kwangu, kuna mtu ametoka sehemu ya Igodivaha, yule mzee amezeeka sana, anafuatilia Dar es Salaam anapoteza hela zake nyingi tu, Mzee Nyanginywa. Amekwenda pale Wizara ya Fedha anazungushwa. Sasa mifano kama hii iko mingi, watu wengi wanateseka sana, wamelipwa hela kidogo sana, wanaambiwa kuna hela nyingine zipo, lakini wanakwenda kule wanazungushwa. Sasa nilikuwa nafikiria, kwa kweli kumuenzi Mheshimiwa Rais. Ni vizuri sana hawa wafanyakazi waliostaafu wasizungushwe, wapate hela kwa sababu kumbukumbu zipo. Kama zimepotea, ule ni uzembe wa Wizara. Kwa hiyo, inatakiwa wale walipwe mapema.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho nataka nichangie ni upande wa *SACCOS*. Kule kwetu Njombe Magharibi, tunapata shida sana kuhusu huduma za kibenki. Bahati nzuri leo nilikuwa nimemwandikia ki-*note* Mkurugenzi Mkuu wa *CRDB* kwamba, angalau atafikirie pale Ilembula aweke tawi au watu wa *NMB* nao watuletee huduma za

Benki. Tunapata shida sana, ni mbali sana. Tunakwenda Makambako ambako ni nje ya Jimbo, tunakwenda Njombe. Sasa ile sisi inatuumiza sana. Sisi tupo mpakani mwa Mbeya, sasa watu wanapofika Makambako au Njombe wanafikiri wamefika Njombe Magharibi. Sisi tupo mpakani, watu wangu wanapata shida sana katika huduma za kifedha. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri vyombo vya fedha wajaribu kutuangalia kwa jicho la huruma na sisi tuwe kama raia wengine tupate huduma za kibenki.

Mheshimiwa Spika, lingine ni hili suala la *SACCOS*. Zipo *SACCOS* zimeanzishwa sasa hivi, tunashukuru Waziri anayehusika wa Ushirika na Masoko na Msaidizi wake, kwa kweli amesaidia sana kwa sababu kulikuwa kuna ukiritimba kuanzisha *SACCOS*. Afisa Ushirika wa Njombe hatufai kabisa, anatukwamisha, hatuwezi tukataja jina kwa sababu huko atakuwa anasikia. Kwa kweli, karibu miaka mitatu tunahangaika *Ubena SACCOS* haisajili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunashukuru sana nguvu za Waziri na msaidizi wake kwamba, nilipolalamika wamesikia wamemweleza Mrajisi wa Vyama vya Ushirika *Ubena SACCOS* imesajiliwa, kwa sasa tuna vyama vikubwa Njombe Magharibi ambavyo ni vizuri, kuna *Ng'anda SACCOS* na *Ubena SACCOS.* Lakini vitu hivi vinatakiwa viwezeshwe kwa kuletewa fedha pale watu wapate hela, wakopeshwe, akina mama na vijana wakopeshwe.

Mheshimiwa Spika, watu wa kule ni wakulima, wana bidii, wanalima sana. Kuna kipindi fulani nilikuwa napiga kelele kuhusu suala la vinyungu, nimezungumza suala la vinyungu, watu wengine wanaweza kushindwa kunielewa, ni kile kilimo cha umwagiliaji. Watu wa kule wanajituma sana, wana nguvu na tukasema kwa kweli kusema kwamba mzuie vinyungu maana yake mtatufanye tufe. Kwa hiyo, wananchi wamenituma kwa kweli tuangalie tufuate zile taratibu tusizuie moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kingine ambacho nataka nichangie ni kuhusu suala la fedha tunazotengewa. Njombe Magharibi fedha tunazotengewa ni kidogo sana. Kwa mfano, Mradi wa Maji, Wizara ya Maji, Mradi wa Wanging'ombe tumetengewa Shilingi milioni 45. Lakini ukifanya uchambuzi yakinifu, ni karibu zaidi ya Shilingi milioni 500 kwa sababu mradi mkubwa ulikuwa wa *UNICEF*.

Sasa una miaka mingi umeshazeeka, una zaidi ya miaka 20. Sasa unatutengea Shilingi milioni 45, milioni 45 kwa kweli ni kidogo sana. Sasa tulikuwa tunashauri wenzetu wa Wizara ya Fedha, tunaelewa kweli keki ni ni kidogo, lakini mtufikirie, hela ziende pale, kama mradi ukifanikiwa ukakarabatiwa vizuri kwa kiasi cha Shilingi milioni 500 utasaidia vijiji vingi sana hasa Tarafa ya Wanging'ombe, kuna tatizo kubwa pale Lyamluki, kuna tatizo kubwa sana pale kijiji cha Lyadebwe, Vijiji vya Saja na Utiga hali ni mbaya. Watu wanakunywa maji machafu kabisa ambayo wanyama wanakunywa na wao wanakunywa. Sasa nilikuwa naomba nitumie nafasi hii kwa kweli mtutengee fedha ambazo ni nzuri kidogo, watu wangu waweze kupata unafuu wa kupata maji safi.

Mheshimiwa Spika, lingine, nishukuru pamoja na kwamba leo ninachangia, lakini nimefarijika. Waheshimiwa Madiwani, wamekuja karibu nane au tisa kwa ajili ya

kuzungumza nami kwamba nichangie hiki na hiki. Kwa hiyo, wamekuja Madiwani Wangama, kuna Madiwani wamekuja kutoka Ilembula, Wanging'ombe na Imarinyi. Ningetaja Kata zote, lakini kwa kweli nimefarijika sana, wamekuja kutoa kilio kwamba, jamani wenzenu huku mambo siyo mazuri na leo bahati nzuri mmeona ninyi wenyewe.

Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba sana, sisi watu wa Njombe Magharibi kwa kweli tunasahaulika sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, kuna kipindi nilikuwa napiga kelele kwamba huwa hawatembelei, kuna Mawaziri wameshafika. Nawashukuru sana. Kwa hiyo, nategemea hata ninachozungumza mtanisaidia. Kwa mfano kuangalia vitu vya msingi ambavyo mnaweza mkatusaidia hasa suala la Benki ambalo ni tatizo. Kwa mfano, Jimbo halina hata Benki moja. Sasa tulitegemea kwamba kama Benki zinakuwa sehemu za Makambako au sehemu za Njombe Mjini kule Njombe Magharibi, hamlete huduma za Benki kwa *NMB*.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunaomba sana, wangekuja pale wawekeze pale, wangetengeza fedha nzuri au *CRDB,* wangeleta pale Ilembula au Igosi au Isaja, mambo yangekuwa mazuri. Tuna mifugo mingi kama ng'ombe, tuna kilimo kizuri. Kuna viazi, hizi *chips,* zinatoka Igosi, watu wa Dar es Salaam mnapata *chips* nzuri, zinatoka Igosi. Kwa hiyo, tulikuwa tunafikiria kwamba ni vizuri waje wawekeze sehemu ambazo zina matatizo ya huduma kama hizi za kifedha.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, karibu mengi wameni-*pre-empt* wenzangu, lakini nishukuru vile vile *FINCA* wamejitahidi sana kufika pale Ilembula. Akina mama wanapata mikopo, lakini tungewashauri waeneze zile huduma, watu wa *FINCA* waeneze sehemu nyingine ambazo hazijapata huduma katika Jimbo letu. Kwa mfano waende mpaka Usuka, Kipengere, na sehemu nyingine, lakini wasi-*concentrate* sehemu moja tu.

Mheshimiwa Spika, Benki nyingine zije pale zilete ushindani. Ingetusaidia sana kuwainua vijana na wanawake katika hali zao za kimaisha kwa sababu hali zao bado siyo nzuri sana.

La mwisho, nichukue nafasi hii kupongeza *TRA*. Kweli *TRA* watu wengi wanalaumu kwamba huduma zao wananyanyasa. Lakini *TRA* wanafanya kazi nzuri sana. Wanakusanya kodi kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, wanavuka malengo. Kwa hiyo, tunashukuru.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Makamishna na Wizara nzima jinsi walivyosimamia ukusanyaji wa mapato. Kwa sababu muda bado ninao, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Njombe Magharibi, kwa kunileta hapa Bungeni na mimi Yono Stanly Kevela ndiyo naongea hapa. *(Kicheko)*

Mimi mwezi wa nane ninawaahidi nitawatembelea bila tatizo. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kevela. Umesahau kuunga au kutokuunga mkono hoja. Basi ili mradi Njombe Magharibi wamesikia, inatosha.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, nimeunga mkono hoja. *(Kicheko)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kuchangia kuhusu hoja ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, inawezekana tukaonekana kama tunarejea yale ambayo wenzangu wamezungumza lakini ninazungumza yale ambayo yanalihusu au yatalihusu sana Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijafanya hivyo, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Fedha, pamoja na Manaibu wake kwa kuandaa Bajeti hii ambayo imewasilishwa leo hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Nawapongeza sana pamoja na Watendaji wao wote.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze kuchangia moja hasa linalohusu huduma za kibenki. Tunajua jiografia ya nchi yetu ni pana sana. Kwa bahatimbaya tu ya maendeleo, tulipofikia sasa hivi bado huduma za mabenki, maeneo makubwa zimefika katika ngazi za Wilaya, basi, hayajakwenda zaidi. Lakini ukifika Makao Makuu ya baadhi ya Wilaya kama walivyosema wenzangu, kwenda vijijini ni mbali na wakati mwingine unaweza kwenda zaidi ya kilomita 200.

Nazungumzia huduma za watumishi hawa ambao kwa kweli wanafanya kazi vijijini huko. Unapofika mwisho wa mwezi, hawa watu tunawaonea huruma. Hawa watu wanasafiri katika mazingira magumu na wakati mwingine tunajua mishahara ya watumishi ni midogo sana. Sasa wanapokwenda umbali huo, mtu atalazimika kulipa nauli ya Sh. 10,000/= kwenda, alipe nauli ya kulala, alipe nauli ya kurudi tena, ni kama anarudi bila mshahara tena.

Sasa mimi nilikuwa naomba, tulishawahi kulizungumza hili suala hapa na huko nyuma nadhani tarehe 15 Juni, 2006 Waziri alipowasilisha Bajeti ya Seriakali, nadhani ilishachangiwa. Kwa hiyo, mimi naomba tufikirie namna nzuri ya kuwahudumia Walimu au watumishi wote kwa ujumla vijijini katika mazingira waliyopo hasa linapokuja suala la kuwalipa mishahara.

Mheshimiwa Spika, kama tunaweza tukaanzisha huduma za kibenki, *Mobile Bank* huko nyuma kulikuwa na utaratibu, likazungumzwa likaonekakana kwamba, wakati mwingine ni hatari pia kusafirisha pesa. Lakini mimi nadhani tuwahurumie hawa wafanyakazi ambao wanakaa vijijini na ni mbali sana wanapofuata mishahara, unaposema mtu mshahara wake ni kiasi hiki, lakini anachopata kwa kweli ni kidogo sana kama wataendelea katika utaratibu huu. Mimi naiomba Serikali ilitazame hili suala kwa

namna nyingine iliyo bora zaidi ili kuwasaidia watumishi hawa ambao wanakaa kwa kweli maeneo ya mbali sana na huduma za kibenki zinazopatikana huko mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hilo, naomba pia nizungumzie masuala sasa ya pensheni kwa wastaafu. Suala la penseheni kwa wastaafu na suala la mirathi kwa wafanyakazi waliofariki, mimi nadhani hili hatutaacha kulizungumza mpaka pale tutakapoona pengine watu wanapata haki zao katika muda muafaka bila matatizo yoyote. Mimi nimetumwa na baadhi ya watumishi wangu na wale wanaofuatilia Marehemu wao kule Wizarani Dar es Salaam.

Lakini nilikuwa nasikia kama hadithi kwamba ukienda Wizara ya Fedha pale kudai fedha, kuna adha na usumbufu mkubwa sana. Nilikuwa siamini sana. Lakini nilipofika pale, wanakuambia faili halionekani. Kilichonishangaza zaidi ni kwamba, pale sikuona kompyuta hata moja ambayo watu pengine unaweza kusema kwamba kuna kumbukumbu zinatunzwa. Wakati mwingine mtu unapokwenda kufuatilia, basi kumbukumbu ziweze kutafutwa kwa urahisi. Hakuna!

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara na Waziri pamoja na Wasaidizi wake, waangalie utaratibu nzuri wa kuiweka ile Ofisi ambayo wanashughulika na masuala ya pensheni, wawe na *data bank,* zile kumbukumbu zitatunzwa vizuri zaidi. Kwa maana hiyo, mtu anapokwenda pale anaweza kupata taarifa na kumbukumbu zote muhimu bila matatizo yoyote hata ukajua kwamba faili liko, malipo haya yamefikia wapi.

Mheshimiwa Spika, nina mfano, kuna mtumishi mmoja alikuwa Jeshi la Wananchi. Alifariki mwaka 1999 na mirathi yake ikafunguliwa mwaka 2001. Huyu alikuwa ni Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Alikwenda pale Upanga Makao Makuu ya Jeshi wakafungua mirathi wale ndugu zake. Lakini kumbukumbu zikaenda Wizara ya Fedha. Waliniletea kumbukumbu mimi nikafuatilia Wizara ya Fedha, Wizara ya Fedha wakaniambia kwamba hawana kumbukumbu hizo. Lakini pale Upanga kumbukumbu zinaonyesha faili zimeshakwenda Wizara ya Fedha. Sasa hakuna namna wanayoweza ku-*trace,* kwa sababu wanasema faili halionekani. Lakini kama kungekuwa na kompyuta, pengine ingekuwa rahisi zaidi ku-*trace* na kujua kwamba kweli faili lilifika na kwa maana hiyo mtu kuweza kuhudumiwa kwa urahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iliangalie vizuri sana hili suala ili kuepusha usumbufu kwa ajili ya wananchi wetu. Lakini pia kuna suala la wastaafu kupotea nyaraka zao muhimu. Kuna watumishi wengi ambao wameajiriwa miaka mingi iliyopita na wengi tunajua mazingira tunayoishi sio mazuri sana ya kutunza nyaraka.

Lakini pia nyaraka zinaweza zikapotea kwa njia mbalimbali. Mtu anaweza akaibiwa, nyumba ikaungua, kwa maana hiyo, nyaraka zikapotea. Sasa unapostaafu, sharti ni kwamba mtu ulete barua yako ya kuajiriwa, barua yako ya kuthibitishwa kazini na kumbukumbu nyingine muhimu ambazo sasa wakati huo huwezi ukazipata. Mtu umeshaajiriwa pengine miaka 20 na zimeshapotea.

Mheshimiwa Spika, sasa hilo sharti mimi naona lisingekuwepo kama kungekuwa na *data bank* kama Wizara ya Fedha ingekuwa na kumbukumbu muhimu kwa watumishi wote au basi Taasisi hizi ambazo wafanyakazi wangekuwa na kumbukumbu hizi, basi

kusingekuwa na kuwasumbua wastaafu. Kwa kweli inaleta shida kidogo kwa mtu ambaye amelitumikia Taifa hili kwa zaidi ya miaka 20 au 30, inapokuja wakati wa kustaafu anahangaishwa sana.

Mheshimiwa Spik,a ninaomba Wizara ijielekeze katika kurekebisha hali hii ili watu waone kwamba utumishi wao kwa Taifa hili haukuwa wa bure na kwamba utumishi wao umetambuliwa na Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu suala la kushuka kwa thamani ya fedha. Mimi siyo mchumi. Hapa tuna Wachumi, na bahati nzuri Waziri wa Fedha mwenyewe ni Mchumi na wataalam wake ni Wachumi. Sasa naomba mimi wanielimishe, thamani ya Shilingi ya Tanzania inashuka kila kukicha. Sasa mimi sielewi sababu ni nini hasa ambayo inafanya thamani yetu ishuke kila wakati.

Mimi nilipoajiriwa kwa mara ya kwanza mwaka 1991, nadhani thamani ya fedha ya Tanzania ilikuwa haijazidi Sh. 400/= kwa dola moja. Leo *rate exchange* yetu tunayoizungumza kwa Shilingi ya Tanzania ni karibu Sh.1,300/=, lakini Shilingi ya Kenya imekuwa *very stable.* Karibu Sh. 70/=, Sh.72/= za Kenya na Uganda ambayo wakati fulani thamani yake ilikuwa chini sana. Karibu sasa Tanzania tunaikuta Shilingi ya Uganda. Hili mimi huwa linanipa shida kidogo.

Ninaomba pengine Waziri atueleze kwamba, kwa nini Shilingi yetu inashuka thamani kila kukicha? Hatujawahi kusikia hata siku moja kwamba, leo angalau imeanza kushuka. Wakati wote inapanda, *against the dollar.*

Mheshimiwa Spika, sasa tuelezwe, kwa sisi tusio wachumi, wengine hili kutu-*convice* inakuwa shida kidogo. Basi tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up,* atueleze kwamba kwa nini hali hii inajitokeza na kwa nini Shilingi yetu inashindwa kuwa *stable* kwa muda mrefu namna hiyo? Lakini pia lazima niseme kwamba hili lilitugusa sana kwa sisi Wabunge.

Mheshimiwa Spika, tuliagiza magari kupitia Kampuni ya *TOYOTA,* tukalipa pesa mara ya kwanza. Baadaye *TOY0TA* wanatuandikia barua wanasema kwamba lazima mwongeze kiasi fulani cha fedha kwa sababu *by the time* mnalipa fedha zenu tayari Shilingi ilikuwa imeshashuka thamani. Sasa hili linasumbua. Lakini tuna hakika kama fedha yetu ingekuwa *stable,* yote haya yasingeweza kujitokeza. Kwa hiyo, tunaomba pengine hili Serikali ili-*address,* Serikali itueleze, kwa nini hali inajitokeza hivyo?

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala lingine linalohusiana na *TRA* kwa ujumla. Kwanza na mimi naomba niungane na wenzangu kuipongeza sana *TRA* kwa kufanya kazi vizuri sana. Naomba niipongeze sana. Suala la kukusanya zaidi ya Shilingi bilioni 200 kwa mwezi, ni dalili kwamba uwezo kumbe upo *TRA*. Kinachotakiwa mimi nadhani ni kuongeza jitihada ili tuweze kukusanya zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na pongezi hizo, mimi nilikuwa nizungumze mambo machache ambayo yawezekana ni *weakness* kwa upande wa *TRA*. Ukiagiza gari

na mimi hili liliwahi kunitokea, unaagiza gari linakwenda kwa ajili ya ku-*escort,* wanapelekewa watu wa Kitengo cha *TISCA* wana-*assess,* wanaweza wakakwambia kodi yako ni kiasi fulani pengine. Au niseme tu *figure* kwamba, wanaweza kukwambia Sh.2,500,000/=. Ikirudi ndani ya *TRA*, kuna *Internal Assessor* ndani ya *TRA*. Huyu anaweza kukwambia, aah!! Walivyo-*assess* sio sahihi. Mimi nilivyo-*assess* hapa utalipa pengine Shilingi milioni tatu.

Mheshimiwa Spika, hili linashangaza sana. Hivi hakuna *formula* ya ku-*calculate kodi?* Mimi nadhani hili linatuchanganya, *TISCA* wamewekwa na Serikali, wanalipwa pesa nyingi. Kwa hiyo, kama hawana uwezo tuwatumie wataalam wetu. *TISCA* basi waondoke, tusitupe hela ya Serikali bila sababu ya msingi. Kwa hiyo, kama *formula* zipo, basi zitumie f*ormula*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kengele ya kwanza imegonga, naomba nizungumzie suala la mwisho.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni kwamba, tarehe 15 Juni, 2006 tulipopitisha Bajeti ya Serikali, Serikali iliondoa *VAT* kwenye mafuta ya taa pamoja na petroli, lakini pia mafuta ya ndege. Kwa hiyo, tulijua kwamba hiyo haina kodi. Bei ya mafuta ni kubwa sana na imeanza ku-*shoot* pengine kuliko pale Bajeti inatangazwa zilipokuwa imekwenda juu zaidi. Leo bei ya mafuta Dodoma ni Sh. 1,100/= mafuta ya taa na petroli ni Sh. 1,400/=.

Mheshimiwa Spika, nashangaa hii *VAT* tuliyoiondoa imetusaidieaje? Sielewi imetusaidiaje. Labda Mheshimiwa Waziri atueleze imetusaidia namna gani. Lakini pia wafanyabiashara wakubwa wa mafuta wasio waaminifu wanaagiza mafuta ya ndege haya na wanauza kwenye Vituo vya Mafuta, kama mafuta ya taa badala yake. Kwa maana hiyo, wanatumia mwanya wa kutokuwa na kodi kwenye mafuta ya ndege kuyapeleka kwenye Vituo vya Mafuta ya Taa. Kwa maana hiyo, wanapata faida kubwa sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi naomba Serikali kama ilikuwa hailijui hili, basi ilifuatilie na kuweka mikakati ya kuhakikisha kwamba mafuta ya ndege yanatumika kwa madhumuni tu ya ndege na kama ni ngumu kutofautisha mafuta ya ndege na mafuta ya taa, basi mafuta ya ndege au mafuta ya taa yawekewe rangi ili kuweza kutofautisha zaidi na kwa maana hiyo, yasiweze kupindishwa na kwenda kwenye vituo watu wakayauza kama mafuta ya taa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, mimi naomba tu niseme kwamba huo ndio ulikuwa mchango wangu na naomba sasa niseme kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ningependa kupongeza Uongozi wa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Zakia Meghji. Mheshimiwa Naibu Waziri - Abdisalaam Khatib pamoja na Mheshimiwa Mustafa Mkulo pamoja na Katibu Mkuu ndugu Grey Mgonja. Kwa kweli

ninawapongeza kwa hoja nzito ambayo wameileta hapa. Kwa kweli imenifanya niunge mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile niupongeze uongozi wa Spika, wamekuwa hapa tangu tarehe 13 Juni, 2006 hadi leo wapo hapa. Wamefanya kazi nzuri ya kupokea hoja mbalimbali. *(Makofi)*

Vile vile, nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Baada ya kusema hayo, nichukue nafasi hii kutoa au kuuliza maswali mbalimbali kutokana na hoja ambayo imeletwa hapa Mezani.

Kwanza huduma ya wastaafu ambayo ipo katika ukurasa wa 33; nachukua nafasi hii kuushukuru uongozi huu wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kuwahudumia wastaafu, hasa Wakuu wa Wilaya Tanzania nzima. Kwa kweli wote ambao wamestaafu wamepata malipo yao yote. Kwa niaba yao,naushuru uongozi huu mzima wa Fedha. Ahsante sana. *(Makofi)*

La pili, ni suala la kufutwa kwa madeni ya ndani na ya nje ambayo ipo katika ukurasa wa 20. Tunaushukuru uongozi huu kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kufuta au kufutwa kwa madeni ya nje na ya ndani. Siku moja nilisema kwamba kukopa ni heshima na kwamba mtu hathaminiwi kwanza kabla hajakopa. Tanzania tumekopa na tumerudisha madeni, tumefutiwa madeni. Hii kwa kweli ni heshima kubwa kwetu na sasa hivi Tanzania tunaweza tukakopa popote kwa sababu heshima yetu imejulikana. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ambalo nilitaka kulizungumzia hapa ni suala la mishahra kupokelea Benki. Hiyo ipo katika ukurasa wa 30 mpaka 31. Katika Wilaya nyingine Tanzania hazina mabenki kama walivyotangulia kuzungumza wenzangu kwamba Mikoa mingine Wilaya zake bado mpaka sasa hazina mabenki. Moja ya Wilaya naweza nikazitaja ni Wilaya ya Ruangwa. Wilaya ya Ruangwa ina Benki kilometa 30 kutoka pale Ruangwa, inakwenda Nachingwea kupokelea mishahara yake.

Wananchi wa Wilaya ya Ruangwa walisema hali hii kwa kweli tunaweza kupata matatizo. Sasa labda tufungue Benki yetu wenyewe, wananchi wa Ruangwa wajitahidi. Walijitahidi kuchangisha fedha ili mradi na wao wanafungua Benki yao, lakini kutokana na ukame na matatizo ya njaa, Benki hii ilishindwa kufunguliwa. Ilifika mpaka Shilingi milioni 50.3, pesa ambazo wananchi wenyewe wameanza kuchangishana ili mradi wanaanzisha Benki yao kuwanusuru wafanyakazi na watu wengine ili waweze kuanzisha Benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Benki hiyo haijaanzishwa kutokana na fedha kutotimia kwa sababu zinatakiwa Shilingi milioni 200. Shilingi milioni 200 sisi tumeshindwa. Tumechangisha hadi Shilingi milioni 50.3. Sasa tungeomba Wizara itusaidie kwa kadri itakavyoweza, basi angalau tuweze kufungua Benki yetu Wilaya ya Ruangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la *SACCOS* ukurasa 10 wa hoja hii. Suala la *SACCOS/SACCAS* na vitu kama hivyo katika maeneo mengine ya nchi hii hawajapata elimu hii ya *SACCOS/SACCAS* na kadhalika na hata suala la mikopo yenyewe hawajapata elimu hii. Kwa hiyo, tungeomba kwa makusudi kabisa Wizara hii ifanye mpango itoe elimu kwa baadhi ya maeneo ambayo hayafahamu masuala haya ya *SACCOS/ SACCAS* na kadhalika, kwa sababu hawa wananchi hawataweza kukopa kama hawana elimu ya kukopa. Hawataweza kufanya masuala ya *SACCOS* kama hawana elimu ya *SACCOS*. Kwa hiyo, tungeomba kwa makusudi kabisa, suala hili lisaidiwe katika maeneo ambayo hawafahamu masuala ya *SACCOS* na *SACCAS* na kadhalika. Inataka kwanza elimu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la sarafu za Shilingi mia moja mia moja. Suala la sarafu ya Shilingi mia moja, nyingi zimefutika sana nchini Tanzania. Ukichukua sarafu ile ya chuma ile ya Shilingi mia, utakuta sehemu nyingi zimefutika. Sasa ukienda dukani kununua kitu, wafanyabiashara wanakataa kuchukua ile pesa. Kwa hiyo, unabaki nayo wewe mwenyewe nyumbani. Sasa wengine hawana elimu ya kurudisha hela ile Benki, anakaa nayo nyumbani, hawawezi kuitumia. Sasa tungeangalia upya pesa zetu, Shilingi mia moja na kadhalika, kwamba: Je, zinaendelea kuwa na zile alama za maandishi au zimefutika? Ili ziweze kurekebishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la mishahara ya Afrika Mashariki. Hapa sasa hivi katika ukurasa wa 34 tunaambiwa kwamba bado watu 26,841 ambao bado hawajalipwa, lakini pesa zipo. Sasa tujue kwamba tatizo hilo lipo na watu hawa wapo na pesa zipo, tatizo ni nini? Tuangalie tatizo ni nini? Pesa za kulipa zipo hawa watu wapo, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba basi sisi Wabunge tuchukue majina yao tuwaleteeni kwa sababu wapo katika maeneo yetu. Kero hii ipo na malalamiko bado yanaendelea, tutafanyaje sasa? Tunaomba basi suala hilo sisi kama Wabunge tulete majina yao kama vile tulivyosema kwamba tutaleta majina ya watu wanaodai mirathi, basi na hili tulifanyie kazi kwa sababu kero hii ipo. Mimi nawafahamu fika watu ambao wamefanya kazi katika Afrika ya Mashariki na mpaka sasa bado hawajalipwa bado. Katika Wilaya yangu wapo wengi tu, katika Mkoa wangu wapo wengi tu. Kwa hiyo, mbinu ya makusudi ifanywe kusudi kero hili iweze kutoweka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niendelee kumalizia suala moja tu kuhusu mishahara ya Walimu. Mishahara ya Walimu au madai ya baadhi ya Walimu ya marupurupu yao kwamba kuna baadhi ya Walimu wanaendelea kulalamika kutopewa marupurupu yao au madai yao na Walimu hao wapo katika maeneo yetu tunayoishi na kumbukumbu zao zililetwa katika Ofisi zetu ambazo zinahudumia Walimu. Tatizo hili naomba tuliangalie kwa macho makini sana ili liweze kutoweka kwa sababu bado lipo. Kumbukumbu hizi inasemekana kwamba zilipotea katika Ofisi zetu. Sasa Walimu wanafanyaje? Turudi tena upya tuangalie suala hili, ili Walimu wetu waweze kupewa mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakupongeza tena wewe, Naibu Spika, Wenyeviti na Mawaziri wote waliopokea hoja mbalimbali kutoka kwa Wabunge wetu. Kwa kweli wamepokea hoja nzito na wengi wamejibu na sisi kama Wabunge, tumeridhika na majibu yetu ya maswali mbalimbali ambayo tumeweza kuyatoa mbele yako.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii muhimu ya Fedha.

Kwanza kabisa, napenda nimpongeze Waziri wa Fedha kwa jinsi alivyoweza kuandaa hotuba yake na Bajeti ya Wizara yake na pia ningependa nichukue nafasi hii, kwa sababu tunafikia mwisho wa Bunge hili, nimhakikishie Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, timu yao inafanya kazi nzuri ya kuongoza nchi, lakini pia ya kuongoza Bunge kwa sababu nilikuwa Jimboni kwa muda wa siku mbili hivi na kila nilikopita niliambiwa nifikishe salamu. Wanafurahishwa na Wabunge, mijadala ya Bunge, wanafurahishwa na jinsi Serikali inavyojibu na wanafurahishwa hasa na Spika wetu anavyomudu Kiti chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii inaonesha kwamba, ndani ya Bunge basi hii mihimili mitatu imekaa barabara na kwamba sisi tuliopewa jukumu la kuwakilisha wananchi, tunaifanya kazi yetu vizuri. Nimelisema hili ili wale wanaosikia *critics* wachache wasije wakafikiria hiyo ndiyo hali halisi. Kwa sababu mawazo yanayotolewa hapa ni ya kuboresha tu.

Ningependa nianze kwa kusema hivi, Rais katika Katiba ya Jamhuri ana madaraka makubwa sana na anapotoa maelekezo siku ya kuvunja Katiba ya nchi ni kwa kuviagiza vyombo vinavyohusika vianze kufanya kazi. Kwa hiyo, Rais alipotamka kwamba fungu la pesa linaongezeka kutoka milioni mia tano kwenda bilioni moja kila Mkoa, maana yake ametoa agizo halali la maandalizi ya kuleta hapa, aidha *by viring or* kwa kuleta kwa *re-allocation* ama hata kwa zile *supplimentary.*

Kwa hiyo, silioni la ajabu ambalo Rais kama walivyosema wenzetu Kambi ya Upinzani, amekosea lipi na hasa pesa hizi zinapokwenda kwa wananchi. Hawa ndiyo waliotuchagua, leo katokea Rais anayeweza kutumia kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya kuwawezesha, halafu sisi tulione ni baya! *(Makofi)*

Mimi nadhani huku ni kutoelewa kazi ya Serikali iliyo na falsafa ya hali ya juu ya kwamba hatungojeani tukabembelezana, Rais akiona wananchi wanahitaji kuwezeshwa analifanya mara moja. Kwa hiyo, tunamuunga mkono. Nasi tunajiandaa kurudi kwenye majimbo kwenda kuhamasisha hasa *SACCOS*.

Napenda nimshukuru sana Afisa wa Ushirika katika Wilaya ya Ukerewe, amehamasisha *SACCOS* na sisi wenyewe wakati wa Kampeni kwa kutumia Ilani,

tumehamasisha sana *SACCOS*. Sasa kuna *SACCOS* ambazo sasa hivi nyingine zimefikia hasa kiwango cha milioni 29 zinasubiri kwa hamu kuwezeshwa zaidi ili tuweze kujikomboa kutoka katika umaskini. Bado nasema, wananchi wote tunaowawakilisha hapa watanufaika. Kwa hiyo, watusaidie sisi Wabunge waanzishe *SACCOS.*

Hii pia itatukomoa Wabunge kutokana na shida tulizonazo kwa pesa kidogo tunazojaribu kuwawezesha wapiga kura wetu. Kwa hiyo, sasa hivi tunaweza tukawaambia ukiingia *SACCOS* unaweza kupata mkopo ambao ni wako hukupewa na mtu mwingine, wewe mwenyewe umechangia, Serikali imekuchangia na sasa unapambana kuondoa umaskini. Kwa hiyo, naomba niishukuru Serikali kwa kazi hiyo nzuri ambayo imefanywa.

Sasa ninayo machache tu ya kusema kwamba, Bajeti yetu nchi nzima sasa hivi tumejitahidi, tumefika asilimia 61 ambayo ni pesa za humu ndani. *TRA* imetuwezesha kufika hapo, tunaomba tuwapongeze. Tumezoea kuwaambia watu hawakufanya vizuri, lakini *TRA* wamefanya vizuri na sasa wasiwe kama mgema wakalitia tembo maji.

Mheshimiwa Spika, pia, tumepunguza kufika asilimia 39 na ni matumaini yangu kwamba katika utegemezi, katika Bajeti ijayo tutakuwa tumepunguza zaidi ili kuweza kuifanya nchi yetu iweze kujitegemea na uwezo huo tulionao. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, takwimu sijazipata barabara za kuona: Je, ongezeko la bei ya dhahabu duniani limerudisha kiasi gani ndani ya hazina yetu? Kwa sababu tulipokubaliana kwenye mikataba, bei ilikuwa chini na sasa hivi imeongezeka karibu mara mbili na nusu.

Ni kiasi gani na sisi kama Taifa tumenufaika na kuongezeka kwa bei ya dhahabu duniani na tungeweza kuangalia hata katika maeneo mengine kiasi gani tunanufaika na minofu ya samaki, ambayo ina bei kubwa nje ya nchi. Huenda eneo hilo hatujalitazama vizuri. Watu wa *TRA*, watazame viwanda vya samaki, ni kiasi gani wanachangia *in really terms* na sio tu zile ambazo wanatumbia wenyewe, kwa sababu kiasi kikubwa wanachopata, hakilingani na kile wanachowalipa wavuvi na kodi wanayolipa ni ndogo. Kwa hiyo, wale wenye viwanda, ni vizuri wakafanya hivyo. (*Makofi*)

Kuna eneo lingine la utalii. Utalii, tuna makampuni mengi ya nje ambayo yanauza *package* za utalii nje ya nchi na watalii wakija hapa *package* zimelipwa nje, tunapoteza kiasi cha pesa kiasi gani na hizo nazo tuzibane ili malipo yaje nchini na tuweze kunufaika. Kwa kufanya hivyo, basi na tukitizama maeneo mengine, tutajikuta ya kwamba tumepunguza kiasi kikubwa cha kuwa tegemezi kwa kutumia rasilimali zetu. *(Makofi)*

Kuhusu pensheni, nami naomba nichangie kidogo. Kati ya mambo ambayo mimi kwa miaka mitano yamenipa matatizo ni pensheni. Watu wanaokuja katika Ofisi ya Mbunge ya Wilaya ni watu wa pensheni na wanatia huruma. Kwa hiyo, sitaki kuongea mengi, nadhani Mheshimiwa Waziri ataweza tu kulitazama na kuweka utaratibu ambao

unafika mpaka ngazi za chini Wilayani, kuweza kuwatazama wote, badala ya wale watu kuhangaika baada ya kulitumikia Taifa hili.

Ningependa pia niongeze kwamba, kuhusu masuala ya usimamizi wa pesa katika maeneo yote, hizi pesa tutakazozipata hapa ni nyingi na mifano ipo ya *NGOs* ndogo ndogo zinapata pesa kidogo, lakini matokeo yake ni makubwa kuliko pesa za Serikali na hii ni kwa sababu ya usimamizi mzuri.

Kwa hiyo, ningemwomba Waziri, najua kuna jitihada za kuwaelimisha wahasibu. Wizara hii ingekuwa miongoni mwa Wizara ambayo ina nguvu zake zinazofika mpaka Wilayani ili kuweza kusimamia pesa zinazofika huko. Mara nyingi tunaambiwa sisi Wabunge kama Madiwani, lakini wale watumishi walioko kule ni vichwa ngumu, wanaweza hata wasiseme ni kiasi gani cha pesa kimeingia. Hapo ningeomba nisisitize ya kwamba ni vyema Wizara ya Fedha iendelee kutupa taarifa Wabunge, wanapotoa migao, ili tuwe tunafahamu kiasi gani kimeingia katika sekta ipi, na tuweze kusimamia pamoja nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kati ya watu ambao wanahitaji malipo ya haraka ni Walimu. Kutolipwa kwao kunajitokeza katika matokeo ya mitihani. Wakati mwingine wanapoteza muda wao kutafuta pesa, au wanapata *frustration* ya kuwatosha, wanaona kwamba ile kazi haina thamani na hasa wakati huu ambao tunawahitaji zaidi, tumefungua Sekondari, *Community Secondary Schools* mpaka vijijini na kwa maana hiyo, hili wimbi la Walimu ndio litakuwa la kwanza la watu wenye ma-*degree* kwenda vijijini. Wengi wamekuwa wakikwepa kwenda vijijini, lakini Walimu hao watakwenda mpaka vijijini kwa sababu shule tulizojenga kwenye *Communities* ziko vijijini, sisi wa visiwani, nyingine ziko katika visiwa kama vya Irugwa. Mwalimu anatumia saa saba kwenye mtumbwi kabla hajafika kwenye shule hiyo.

Kwa hiyo, mwalimu kama huyo hahitaji tena ababaishwe na mshahara wake ama ababaishwe na pesa zake za malipo. Kwa hiyo, mimi ningemsihi Waziri aweke utaratibu mzuri wa malipo na asisitize Wizara zinazohusika kuwafikia watu wa namna hii.

Ningependa pia niseme tatizo moja. Kumekuwa na utaratibu wa kutoa adhabu kwa Halmashauri ambazo hazitekelezi wajibu wao, tuseme waweka fedha. Kwa sababu Halmashauri haiwezi kuwa kila mtu, unakuta kwamba Bwana Fedha mliyenaye hajui mahesabu.

Kwa hiyo, vitabu vinapovurugika, wanatoa adhabu. Kwa mfano, *the capitation grant,* kuna Wilaya ikiwemo na ya kwangu, ambazo hazipati *capitation grant*. Pesa za *grant* bure, sasa wengine wanapewa bure kwa sababu walipata Mhasibu mzuri. Ukerewe na Wilaya nyingine hawapati kwa sababu walituletea Mhasibu *bogus*. Sasa unapoinyima Wilaya, umeacha kumwadhibu yule asiyejua kazi yake, unamwadhibu mwananchi ambaye hana uhusiano kabisa na suala hilo. Kwa hiyo, hilo mimi ningeomba liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, sisi Ukerewe tuna *experience* nyingine ya kwamba, kuna wakati Waziri aliyehusika alisimamisha ujenzi wa barabara kwa sababu kuna mhasibu alikula Shilingi milioni 14. Mpaka leo hajachukuliwa hatua yoyote, anahamishwa kituo mpaka kituo, lakini sisi tunahangaika na barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani Wizara hii itaangalia wakati wa kugawa pesa hii. Ni mifano michache tu nimeitoa, wakati wa kugawa pesa, watu wasiadhibiwe kwa ubovu wa mtumishi. Mtumishi mbovu anachukuliwa hatua na watu hawa wanapewa kitu ambacho ni haki yao. Tusipofanya hivyo, hasa sisi tunaotoka Wilaya za pembezoni ambapo watu wanapelekwa kama adhabu, kila siku tutaadhibiwa pamoja na watumishi wabovu. Kwa hiyo, hilo ninaomba nimsihi Waziri kwamba aliangalie kwa makini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningeomba tu azingatie pia watu walio katika *cadre* ya kusimamia pesa; wahasibu, *internal auditors* wawe kweli *professional*, wasipokuwa *professional*, hii kazi yote tunayoifanya, ya kwenda kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya, itakuwa imepunguzwa kasi kutokana na hao wabovu ama watu ambao sio *committed* katika kazi hii tunayoifanya.

Mimi nataka nimalizie kwa kusema kwamba, kazi inayofanywa ni nzuri na kusiwe na mtu wa kudanganya na wala wale wanaokosoa, nadhani wanaongezea tu uzito katika kazi nzuri inayofanywa. Sisi tunatoka hapa kwa nguvu moja, tunarudi vijijini tukiwa tumewezeshwa, kama tulivyowezeshwa katika Ilani ya Uchaguzi tukayazungumzia haya mambo. Sasa wananchi wetu watayaona kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hapo ndipo tumefika mwisho wa mpangilio wa shughuli za leo. Kama tulivyopitisha Azimio ili tuweze kuwahi katika hafla ambayo mgeni rasmi Mheshimiwa Waziri Mkuu na mnamjua jinsi anavyotunza muda, ataingia saa 2.10, itakuwa ni aibu sana sisi wengine tena tuwe tunajivutavuta, ndio unakuja kuja.

Spika atakuwa tayari saa 2.00 kumpokea mgeni rasmi. Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa ile saa 1.30 iliyotajwa, ndio hasa inastahili mtu ufike pale. Hafla hii ni ya aina yake. Leo tumepata *briefing* kutoka kwa Kamati husika, kuna zawadi nyingi sana zinazotambua vipaji mbalimbali vilivyomo ndani ya Bunge letu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, licha ya kumuaga Spika mstaafu, Mheshimiwa Pius Msekwa, lakini kutakuwa na zawadi za kila namna zinatambua vipaji, vingine vya papo kwa papo, kwa mfano muimbaji mzuri wa taarabu, mchezaji mzuri wa *twist* na kwa umri mbalimbali. Kwa hiyo, kuna matukio mengi. Isitoshe, wale mabinti zetu waliomaliza mashindano ya urembo kule Dar es Salaam, wa kwanza wa pili na watu watakuwepo.

Kama mnavyofahamu, huwa tunawaenzi kwenye hafla kama hizo. Kwa hiyo mtaweza kuwaona. Msisahau kwamba mshindi wa urembo safari hii ni matunda mazuri ya Muungano kwa sababu ana damu ya Tabora na Zanzibar. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna Mheshimiwa ambaye amesahau miwani kwenye ukumbi tulipokuwa tukifanya mkutano wa *briefing*, tunaomba hebu nyoosha Katibu, ni miwani maalum sana hii, ina rangi nyeusi ina dhahabu. (*Makofi*)

Lingine, nataka kukumbusha tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, pale nje kuna wenzetu wamejenga tabia ya kufanya *parking* kuzunguka ile *round about* pale, inaleta shida/kero kubwa sana kwa wengine wote.

Ni kweli dereva anaweza kuitwa kumchukua Mheshimiwa ili waondoke, lakini wengine sasa wanapaki. Asubuhi, mpaka saa saba hapo hapo tu karibu na *round about.* Inaweka nafasi ni ndogo na tumeelekezwa na watu wa usalama kwamba, hata kwa utaratibu wa usalama, hiyo hairuhusiwi. Kwa hiyo, nawasihi tuzingatie hilo.

La mwisho, nitangaze matokeo, kwa sababu hatuna nafasi yoyote nyingine. Tulifanya Uchaguzi kwa *CPA*, kupata mjumbe wa Baraza letu, kama ya utendaji ya Tawi la Tanzania. Nadhani kwa kuwa ni hadhara ya kiasi hiki, nisitaje kura. Nadhani niseme tu kwamba, aliyechaguliwa ni Mheshimiwa Tatu Ntimizi. *(Makofi)*

Baada ya tangazo hilo, naomba niwatakie maandalizi mema ya muda mfupi huu, ili tukutane sasa kwenye hafla. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12:42 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 15 Agosti, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*